Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao cha Kumi – Tarehe 9 Februari, 2009

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) alisoma Dua

HATI ZA ZILIZOWASILISHWA MEZANI

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:

Mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika Mwaka wa Fedha wa 2009/2010.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 122

Uhamishaji wa Makao Makuu Kwenda Dodoma

MHE. ZUBEIR ALI MAULID aliuliza:-

Kwa kuwa, nchi nyingi zilizoamua kuhamishia Makao Makuu ya nchi kutoka Makao ya zamani kwenda makao mapya (Nigeria, Malawi) ziliarifu nchi marafiki kuhamishia Balozi zao kwenda miji mipya na zoezi lilitekelezwa vizuri:-

(a) Je, ni kwa nini Tanzania haizishawishi nchi marafiki kuhamishia Balozi Dodoma?

(b) Je, Serikali imezitayarishia nchi marafiki maeneo ya kujenga ofisi zao hapa Dodoma na kama jibu ni ndiyo. Je, ni maeneo gani yametengwa kwa nchi zipi?

(c)Je, kuna uwezekano wowote kuwa Balozi hizi hazihamii Dodoma kwa sababu Serikali yenyewe haijawa na uamuzi thabiti wa kuhamia Dodoma?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mbunge wa Kwamtipura, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kuamua kuhamishia Makao Makuu ya Nchi Dodoma mwaka 1973 pamoja na mambo mengine ilichukua hatua za kuzishawishi nchi marafiki na taasisi za Kimataifa kuhamishia Balozi na ofisi zao Dodoma. Kutokanana hatua hiyo Balozi za Zimbabwe, Canada, Denmark, Switzerland, Ujerumani, Japan, Uganda, Iran, India na Kenya zilipewa maeneo ya kujenga ofisi zao. Aidha, Mashirika ya Kimataifa ya *UNDP, USAIDS* na kadhalika yalichukua maeneo.

(b) Mheshimiwa Spika, katika miaka ya 1980, Serikali ilitenga viwanja katika meneo ya Mlimani, Mendeli Mashariki na Mlimwa Mashariki kwa ajili ya Ujenzi wa Ofisi za Balozi na Taasisi za Kimataifa. Aidha, eneo la *National Capital Centre (NCC)* lilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za Wizara mbalimbali.

Kutokana na kucheleweshwa kwa ratiba ya uhamishaji Serikali kwenda Dodoma kulitokana na kutokamilika kwa matayarisho yaliyotakiwa kwa sababu mbalimbali zikiwemo za kiuchumi. Baada ya maeneo hayo kukaa zaidi ya miaka 20 bila kujengwa, yalianza kuonyesha mapengo katika Mji na pia kuwa finyu kutokana na kukua kwa Taasisi hizi. Hali hii ilifanya Serikali kuamua kuyapangia matumizi mengine.

Hivi sasa Serikali imeanza upya mchakato wa kuangalia maeneo yanayofaa kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Ikulu, Wizara mbalimbali, Taasisi za Makazi ya Viongozi na Wafanyakazi wa Serikali. Katika hatua hii, utengaji wa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Balozi za nchi mbalimbali litajumuishwa.

(c) Mheshimiwa Spika, Uwezekano wa Balozi za nchi marafiki kuhamia Dodoma ni dhahiri baada ya jitihada zinazofanywa na Serikali kukamilika. Hivi sasa Serikali iko katika mpango wa kuendesha mjadala wa kitaifa juu ya kuharakisha changamoto mbalimbali na namna ya kuharakisha Serikali kuhamishia Makao Makuu ya Nchi Dodoma Mchakato wa kuandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri juu ya mjadala huu umeanza na uko kwenye hatua za mwisho.

MHE. ZUBEIR ALI MAULID: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa inaonyesha dhahiri pamoja na kwamba viwanja hivyo vilikuwa vimetolewa mapema sana kwa ajili ya hizo nchi ambazo amezitaka lakini wengi wao

hawakufanya hivyo kwa sababu serikali yenyewe haionekani kama inalo kusudio hasa la kuhamia Dodoma na kuifanya Dodoma kuwa Makao Makuu.

Je, ni nchi zipi ambazo zimeonyesha nia ya kutaka kujenga kwa sababu hivi karibuni Marekani baada ya kupata lile tatizo la Ubalozi wao wa zamani walipewa kiwanja kingine kulekule Dar es Salaam na walijenga na kukamilisha jengo lao.

Je, ni nchi zipi ambazo zina nia ya kweli ya kuhamia Dodoma kama ambavyo Serikali ina nia ya kweli ya kuifanya Dodoma kuwa Makao Makuu?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Mbunge swali lake kama ifuatavyo:-

Serikali bado ina nia ya dhati kabisa ya kuhamia Dodoma, tatizo nimelielezea ni la kiuchumi. Balozi za nchi rafiki zilizoamua pale awali kuhamia Dodoma au kujenga makao yake Dodoma na ofisi nyingine nilizitaja katika jibu langu la msingi.

Ifahamike kwamba Serikali ikishahamia Dodoma hakuna namna ya Mabalozi kubaki Dar es Salaam, ni lazima wawe na Serikali ili shughuli zao za kila siku ziweze kufanyika kwa urahisi.

MHE. EPHRAIM NEHEMIA MADEJE: Kwa kuwa ni dhahiri kabisa kwamba Balozi za nje haziwezi kuhamia Dodoma kabla Serikali yenyewe haijahamia na kwa kuwa katika Ilani ya Uchaguzi wa mwaka 2005 CCM tuliahidi kwamba Sheria ya kuitambua Dodoma rasmi kama Makao Makuu ya Serikali ilitungwa.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutueleza ni lini hiyo sheria italetwa kwenye Bunge hili Tukufu?

SPIKA: Mimi nimefupisha hata kuendelea kuuliza swali hili, ninyi wenyewe mnaambiwa mjadala utaanza tena kitaifa bado mnataka kuuliza.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi majibu tafadhali!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Ephrahim Nehemia Madeje, Mbunge wa Dodoma Mjini, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza nashukuru kwa ufafanuzi wako lakini pia Mheshimiwa Ephrahim Nehemia Madeje kama Mkurugenzi wa *Board* ya Mamlaka ya Uhamishaji Makao Makuu anafahamu hatua tulizochukua hadi kufikia sasa ili kufanikisha Sheria ya kutambua Dodoma kuwa Makao Makuu na taarifa ya mara ya mwisho tuliyoitoa kwenye *Board* ni kwamba mchakato umeshatufikia katika Ofisi ya Waziri Mkuu na kwa kupitia ngazi ya Makatibu Wakuu na kwa upande wa utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi bado

tuna muda wa miaka miwili. Kwa hiyo, tuna hakika kwamba Sheria hii itatungwa kabla ya mwaka 2010.

Na. 123

Kamati za Tenda za Wilaya Kuta Maelezo Kuhusu Tenda

MHE. MGANA I. MSINDAI aliuliza:-

Kwa kuwa, Sheria ya Fedha sasa imewatoa Madiwani katika vikao vya kutoa Tenda.

Je, Serikali haioni kuwa ni busara Kamati ya Tenda itoe maelezo ya tenda husika kwa mwenyekiti au Meya wa Halmashauri husika mara wanapomaliza kutoa Tenda kuliko ilivyo sasa ambapo hakuna maelezo ya kina yanayotolewa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, ili kuweka kumbukumbu sawa, kile Mheshimiwa Mbunge anachokiita Kamati ya Tenda ni Bodi za Zabuni yaani (*Tender Board*). Bodi za Zabuni ni vyombo vya Halmashauri ambavyo vimepewa majukumu ya kushughulikia manunuzi ya vifaa na huduma katika Halmashauri za Wilaya na Miji kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Manunuzi. Waheshimiwa Madiwani hawakuondolewa kuwa Wajumbe wa Kamati za Tenda kwa Sheria ya Fedha, bali ni kutokana na kupitishwa kwa Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 21 ya Mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, Bodi za Zabuni zinatakiwa kwa mujibu wa Kanuni za Manunuzi za mwaka 2007 kutoa taarifa za utekelezaji wa kazi zake kwenye vikao vya Kamati za Fedha, Uongozi wa Mipango kila baada ya miezi mitatu. Madhumuni ya kufanya hivyo ni kuwezesha Waheshimiwa Wajumbe wa Kamti hizi kuelewa na kujiridhisha iwapo taratibu zote za kutoa zabuni hizo zilizingatiwa kama zinavyoelekezwa katika Sheria na Kanuni za Manunuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wenyeviti na Mameya wa Halmashauri ni Wajumbe na Wenyeviti kwenye Kamati za Fedha, taarifa zinazohusu Tenda huzipata kupitia vikao hivyo vya Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango. Aidha, baada ya mchakato wote kukamilika kabla ya Mzabuni/Mkandarasi hajapewa kazi, Kitengo cha Manunuzi cha Halmashauri (*Procurement Management Unit*) huandaa Mkataba ambao husainiwa na Mwenyekiti au Meya wa Halmashauri na Mkandarasi au Mzabuni husika baada ya kusomwa pande zote mbili.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, miradi hasa ya ujenzi wa barabara na majengo yanafanyika kwenye Kata zetu na kwa kuwa kazi hizo haziendi kama inavyotakiwa. Je, Serikali haioni umuhimu wa kutoa *bill of quantities* kwa Madiwani ili miradi inayoendelea kwenye Kata wajue ni nini kinatakiwa kufanyika?

Ka sababu Wenyeviti wetu wengi hawaelewi wao wanapelekewa tu kusaini kabla hajaelezwa kinini kimetokea, Waziri haoni kwamba kuna umuhimu wa kuitisha mikutano kwa ajili ya Mameya na Wenyeviti kuwaelekeza wanayotakiwa kufanya?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TMISEMI): Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mgana I. Msindai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mimi naelewa anachozungumza hapa Mheshimiwa Mgana I. Msindai ni kwamba Mamlaka ile ya chini pale kwenye Kata inao utaratibu wake ambao unatumika kwa ajili ya kuweza ku-*award* na kusema huyu ndiye ambaye amechaguliwa kupewa kazi ile.

Lakini utaratibu ule hauwezi kuruka hatua yoyote yeye hapa anazungumzia *Bill of Quantities. Bill of Quantities* ni kile kinachoonyesha kwamba ni kazi gani ambayo inategemewa kwenye kufanyika kule ambayo itapewa yula Mzabuni au Mkandarasi ambaye ameomba kazi pale.

Mwenyekiti wa Halmashauri atayajua haya yote kupitia katika Kamati ya Fedha ambayo nimeizungumzia hapa ataona kila kitu kilichopo pale.

Sasa hii *Bill of Quantities* tunaiandaa sisi na Halmashauri ndiyo zinaandaa pale, kwa hiyo mimi sioni tatizo lolote pale sasa kinazungumzwa hapa katika swali namba mbili kwamba liko tatizo hapa na kwamba Wenyeviti wetu wanapelekewa na kusaini. Ndivyo Sheria inavyosema, Sheria inasema kwamba atakayesaini mkataba ule ni Mwenyekiti wa Halmashauri au Mwenyekiti wa Manispaa hata kama wakati walipokuwa wanafanya maamuzi yale yeye hakuwepo pale.

Sasa ipo hoja iliyoletwa na Mheshimiwa Mgana I. Msindai na ninatambua kwamba Mheshimiwa Mgana I. Msindai amewahi kuwa Mwenyekiti wa *Local Authorities Accounts Committee* na hivyo tunapozungumza hapa Mheshimiwa Mgana Msindai ndiye Makamu Mwenyekiti wa *Local Authorities Accounts Committee* kwa hiyo yuko conversant sana jambo hili analozungumza hapa. *(Makofi)*

Anachozungumza ni suala la kutoa elimu kwa hawa Wenyeviti wetu wa Halmashauri pamoja na Manispaa. Mimi siwezi kukataa hapa kutoa elimu kwa ajili ya watu hawa, kutoa elimu maana yake unatoa afya ya ubongo yaani watu wajue mambo.

Kama wanafanya maamuzi yale bila kuwa wanafahamu mimi nakubaliana na Mheshimiwa Mgana I. Msindai kwamba iko haja ya kutoa elimu kwa ajili ya Wenyeviti hao.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali la nyongeza.

Kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba mwenyekiti anapelekewa mikataba kusaini pamoja na kwamba hakuhudhuria kwenye *Tender Board.* Je, Mheshimiwa Naibu Waziri utakubaliana na mimi kwamba hiyo Sheria ya Manunuzi ina mapungufu kwa sababu kama itatoa matatizo kwenye mkataba na Mwenyekiti amesaini au Meya wanaweza kupata matatizo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TMISEMI): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:

Mheshimwa Spika, Sheria hii ndivyo inavyosema, inamtaka Mwenyekiti ahakikishe kwamba na ninataka hapa nieleze vizuri ili tuelewane.

Mwenyekiti wa Halmashauri jambo hili anakutana nalo katika Kamati ya Fedha ambalo yeye ni Mjumbe, anapokaa katika ile Kamati ya Fedha pale taarifa hii ya Wazabuni na taarifa ambayo imefanyika katika ile *Procurement Unit* pamoja na *Tender Board* inaletwa katika ile Kamati pale. Anakuja kukutana nao tena atakapokuwa anapata taarifa zinazokuja *quartely* katika *Full Council,* akienda pale napo ataipata.

Sasa Mheshimiwa George M. Lubeleje, anasema hivi, bado huyu Mwenyekiti anaweza akafika mahali akawa amepitisha jambo ambalo hana uhakika nalo.

Kwanza Mwenyekiti anatakiwa ajiridhishe. Mimi nitashangaa sana Mwenyekiti ambaye anakwenda anasaini mkataba pale, anasaini tu hivihivi bila kuwa na uhakika na kitu anachosaini pale.

La pili, anasema hivi, je, huoni kwamba kuna haja ya kumsaidia Mwenyekiti huyu ili asije akaitumbukiza Halmashauri katika mpango huu. Kwa hiyo, tuangalie utaribu ambao utaiweka Sheria hii isaidie.

Mheshimiwa Spika, Sasa, suala la kubadilisha Sheria ni suala la kikao chako cha Bunge hapa, mimi nasema kwamba Mheshimiwa George. M. Lubeleje, kama ana mapendelezo yoyote ayalete sisi tutayashughulikia kwa taratibu zilizowekwa ili kuondoa hilo tatizo ambalo anafikiria kwamba linaweza likajitokeza.

Na. 124

Ujenzi wa Ukuta wa Mto Pangani

MHE. MOHAMMED RISHED ABDALLAH aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Wilaya ya Pangani kuna ukuta ambao ulijengwa zaidi ya miaka 100 iliyopita ili kuzuia maji ya Pangani kusambaa kwenye mji huo, na kuwa kuwa, Serikali imekuwa ikiagiza kuwa Halmashauri iandae makisio kwa ajili ya ujenzi mpya wa ukuta na Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi huo.

(a)Je, Serikali imefikia wapi katika kupata fedha hizo kwani makisio yalikwisha kuwasilishwa?

(b)Je, Serikali itakuwa tayari kutembelea Pangani ili kujiridhishia hali halisi ya ukuta huo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU W ARAIS (MAZINGIRA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira imeandaa mradi ambao pamoja na mambo mengine utagharimia ujenzi wa ukuta wa Pangani. Mradi huo una Bajeti ya jumla ya dola za Marekani milioni 3.0 takribani shilingi bilioni 3 za Kitanzania. Mradi huo tayari umekwisha wasilishwa Makao Makuu ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira *(UNEP)* kwa ajili ya kupata fedha chini ya mfuko wa mabadiliko ya tabianchi wan chi maskini duniani (*Least Developed Countries Fund (LDCF)*. Tunatarajia fedha hizo zipatikane kabla ya mwisho wa mwaka huu. Utekelezaji wa mradi huu utasaidia kuimarisha juhudi za uhifadhi wa mazingira ya mwambao wa Pwani pamoja na kukuza weledi wa wananchi katika Wilaya za Pangani, Bagamoyo na Rufiji na maeneo mengine kuhusu changamoto za mabadiliko ya tabianchi na athari zake.

(b) Tarehe 18 Novemba hadi tarehe 22 Desemba, 2007, Wataalam wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Baraza la Taifa la Usimamizi wa Hifadhi ya Mazingira na Wizara ya Miundombinu walitembelea Pangani na kujionea hali halisi ya ukuta huu, pamoja na athari zingine za mabadiliko ya tabianchi.

Aidha, wakati wa maandalizi ya mradi huu wataalamu walikaa na Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Pangani ili kuhakikisha kuwa tunapata makisio sahihi ya gharama za kukarabati wa ukuta huo.

MHE. MOHAMMED RISHED ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimwa Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Pangani ilileta makisio katika Ofisi ya Makamu wa Rais na kinachoonekana hapa ni tofauti kubwa kati ya makisio ya Halmashauri ya Pangani na Ofisi ya Makamu wa Rais, kumaanisha kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Pangani imekisia pesa kidogo sana.

Je, Serikali wamekwisha sawazisha hilo pamoja na Halmashauri ndiyo maana mkafikia hii dola milioni tatu?

La pili, Serikali imesema kwamba wanategemea kupata hizi pesa hivi karibuni au kabla ya mwisho wa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaweza ikatuambia kwamba iwapo pesa hizi hazitafika kwa wakati ambao umetajwa Serikali itakuwa tayari kuleta pesa kwa ajili ya kufanya ukarabati mzuri zaidi kuliko unavyofanyika hivi sasa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU W ARAIS (MAZINGIRA): Napenda kujibu swali la nyongeza la Mohammed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, kama ifuatavyo.

Ni kweli kabisa Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira pamoja na Halmashauri ya Pangani tulikaa pamoja na tukakubaliana kiwango cha gharama za kukarabati ukuta ule kiasi cha shilingi milioni 578 na ndiyo maana fedha hizi shilingi milioni tatu (3) dola ambazo ni takribani bilioni 3 za Kitanzania zitasaidia katika ukarabati wa eneo la ukuta wa Pangani.

Lakini pia katika maeneo mengine ya mwambao ambayo yameathirika kutokana na kuongezeka kwa maji katika bahati maeneo mengi ya ukanda wa Pwani visima vyake vimeingia chumvi na hivyo basi visima vya maeneo ya Bagamoyo, Rufiji, Mafia na hata Zanzibar vitaweza kufaidika. Ama kuhusu kama tutakosa fedha hizo sisi tunakuhakikishia kwamba fedha hizo tutapata mwakilishi wetu kutoka Wizara yetu ni Mwenyekiti wa Board kubwa ya Umoja wa Mataifa inayoshughulika katika kugawa fedha hizi, kwa hiyo kwa makubaliano ya msingi yalishatengwa kwa ajili ya fedha hizi.

Kwa hiyo, tunawahakikishia kwamba fedha tutapata na kama tusipopata kutokana na umuhimu tutaona jinsi gani tunaweza tukatafuta mahali pengine.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Na. 125

Ahadi ya Kuwapa Wananchi Uwezo wa Kupambana na Rushwa

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali iliahidi kuwajengea wananchi mazingira mazuri zaidi yatakayowapa uwezo, ari na ujasiri wa kupambana na rushwa (Ufisadi).

Je, Serikali imetekeleza kwa kiasi gani ahadi yake hasa ikizingatiwa kuwa, rushwa ni tatizo linaloendeshwa Kisayansi hapa nchini?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Sera ya Tanzania kuhusu mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa na ufisadi ni ya kutoivumilia kabisa rushwa (*zero tolerance*). Kwa hiyo, mapambano haya yanashirikisha jamii yote ya Tanzania kwa maana ya Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia, Taasisi za Dini, Vyombo vya Habari na Wananchi kwa ujumla. Katika kuwapa uwezo wananchi na wadau wengine wa mapambano dhidi ya rushwa kushiriki kikamilifu katika Kupambana na Rushwa Serikali imefanya mambo yafuatayo:-

· Serikali imeiwezesha Taasisi za Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kupanua huduma zake kwa kuanzisha ofisi zake hadi katika Wilaya zote za Tanzania Bara. Lengo ni kupeleka huduma karibu na wananchi ili waweze kushirki kikamilifu katika mapambano dhidi ya rushwa.

· Serikali pia inaendelea na kusimamia na kufuatilia mpango wake wa Awamu ya Pili wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa *(NACSAP II)* ambao inashirikisha sekta zote za umma, Asasi zote zisizo za Kiserikali na Asasi za Kidini, Sekta Binafsi, Vyombo vya Habari na Wananchi kwa ujumla.

· TAKUKURU imekuwa ikishiriki katika matamasha na maonyesho mbalimbali nchini kwa lengo la kutoa elimu na uelewa kwa wananchi wa jinsi ya kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa.

Baadhi ya maonyesho ambayo TAKUKURU hushiriki ni :-

· Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Saba Saba ya Dar es Salaam.

· Maonyesho ya Sikuku ya Wakulima (Nane Nane).
· Sikukuu ya Wafanyakazi (Mei Mosi).

· Wiki ya Utumishi wa Umma (Juni kila mwaka).

· Siku ya Uadilifu wa Kimataifa (*Integrity Day*).

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU kwa niaba ya Serikali, imekuwa na inaendelea kutoa mafunzo kwa njia ya warsha na makongamano, usambazaji wa vipeperushi, kuendesha vipindi vya radio na televisheni katika kutoa elimu kwa umma kuhusu dhana ya rushwa na jinsi ya kushirikiana na Serikali katika kuipiga vita rushwa.

Aidha, wananchi wanaruhusiwa kupiga simu maalum (*Hotline*) Namba 113 bila kulipia kwa Viongozi wa TAKUKURU katika kufichua vitendo vya rushwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007 Serikali, kupitia Bunge lako Tukufu ilifanya marekebisho makubwa ya Sheria ya Rushwa, ili kuiboresha, kuimarisha na kuipa nguvu na meno zaidi ili TAKUKURU iweze kuwashughulikia ipasavyo wala rushwa.

Hivi sasa Serikali imeanzisha mchakato wa kuweka mfumo mzuri wa kuwalinda mashahidi wa kesi za rushwa na wale wote watakaotoa taarifa matukio au vitendo vya rushwa kwa kutung aSheria *Whistleblowers.*

Serikali pia imeidhinisha mchakato wa kufanya utafiti nchi nzima kwa kuwashirikisha wananchi na Sekta zote ili kupata picha ya hali halisi ya rushwa na maendeleo ya mapambano dhdi ya rushwa na ujenzi wa Utawala nchini. Mpango huu wa utafiti unaitwa *National Governance and Corruption Survey* na utasimamiwa na TAKUKURU.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya hatua zilizochukuliwa na Serikali kama zilivyoainishwa hapo juu zimebadilisha kwa kiwango kikubwa mtizamo wa wananchi kuhusu tatizo la rushwa nchini. Suala la rushwa sasa limekuwa ajenda muhimu kwa wananchi na linazungumzwa na kujadiliwa kwa uwazi zaidi kuliko wakati wowote ule katika historia ya nchi yetu.

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niulize maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, rushwa ambazo huwa ziliendeshwa Kisanyansi katika nchi yetu ni pamoja na rushwa ile ya *EPA* na kwa kuwa, kuna watu ambao walirejesha fedha za *EPA* na wengine wakashindwa kurejesha fedha.

Sasa hawa walioshindwa kurejesha fedha mimi sina haja nao kwa sababu wako Mahakamani. Sasa mimi pamoja na wananchi wengine tunataka kujua hawa waliorejesha fedha ni akina nani na kwa nini hawatajwi wananchi wakawafahamu? Je, kuwaficha hawa si kuendeleza kuilea rushwa?

SPIKA: Kiwango kile swali hili limeulizia swali la *EPA* ambalo liko Mahakamani kwa kesi kadhaa siwezi kuliruhusu kwa mujibu wa Kanuni. Kwa hiyo, tunaendelea!

Mheshimiwa Grace S. Kiwelu swali la nyongeza tafadhali!

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Pamoja na mikakati mingi Serikali ilikuwa nayo naomba kujua ni lini Serikali itaanzisha somo la kupambana na rushwa kuanzia shule za msingi mpaka za sekondari?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA)): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, kama ifuatavyo:-

Kwa sasa tunachofanya ni kupita katika shule na Asasi mbalimbali na kuwafundisha au kuwaelimisha wahusika kuhusu matatizo ya rushwa. Bado hatujawa na mkakati wa kuliweka somo la mapambano dhidi ya rushwa katika *curriculum* ya shule hizi.

Lakini ni wazo zuri na mimi nalichukua, pengine wenzangu wakishalijadili tunaweza tukaamua nini tufanye au lini tutafanya shughuli hiyo.

Na. 126

Mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii Kuhusu Mkopo

MHE. MARTHA J. UMBULLA aliuliza:-

Kwa kuwa, sehemu kubwa ya mikopo inayotolewa na Halmashauri za Wilaya hapa nchini kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto haifanyi vizuri kuirejeshaji; na kuwa, Maafisa Maendeleo ya Jamii hao hawana ujuzi katika mikopo:-

(a) Je, kwa nini Serikali isibadili mwelekeo na kupeleka fedha hizo kwa kutoa mafunzo ya kina kuhusu mikopo kwa maafisa hao?

(b) Je, kwa nini Serikali isipeleke fedha hizo kwenye *SACCOS* au taasisi nyingine za fedha zinazofanya vizuri katika Halmashauri husika?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi, Umbulla, Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatvyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu naomba nitoe maelezo mafupi. Maafisa ya Maendeleo ya Jamii wote wana ujuzi na kuhamasisha jamii, kutoa na kufuatilia

mikopo, kwani mafunzo haya ni sehemu ya masomo yao wanapokuwa vyuoni. Vilevile Wizara yangu inatoa mafunzo rejea kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii kila mwaka kwa awamu. Kwa mfano, mwaka huu wa fedha 2008/2009 Wizara imetenga fedha ya mafunzo rejea kwa ajili ya Maafisa Maendeleo ya Jamii 200 wa ngazi ya Kata. Baada ya maelezo haya, napenda kumjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, madhumuni ya fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (*WDF*) ni kwa ajili ya kuwakopesha wanawake wenye kipato kidogo ili kuinua kipato chao na kuboresha hali zao za maisha hivyo kuzitumia kutoa mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii, ni kinyume na madhumuni ya Mfuko huu. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekuwa ikitoa fedha hizo kupitia Halmashauri na ni Halmashauri husika zilizokuwa zikikopesha vikundi vya wanawake katika maeneo yao.

Aidha, Wizara yangu baada ya kupata ushauri kama huu wa Mheshimiwa Mbunge kutoka kwa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, iliwasiliana na TAMISEMI kwa barua ya tarehe 10 Juni, 2008 kuhusu kupitisha fedha hizo za mikopo kwenye *SACCOS.* Hivyo ninakubaliana na ushauri wa Mbunge na tayari tumeshaanza kuufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na Madiwani kuwahamasisha wanawake na jamii kwa ujumla katika uundaji wa *SACCOs* ili kurahisisha utoaji na upatikanaji wa mikopo na hatimaye kuondokana na umaskini.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali ndogo la nyongeza pamoja na majibu mazuri na ya kuridhisha ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa kujiunga na *SACCOS* kunahitaji mtaji mdogo wa kujiandikisha na kuendelea kuchangia *SACCOS;* na kwa kuwa katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu kuna umaskini uliokithiri kiasi kwamba baadhi ya jamii zinashindwa hata kupata mitaji ya aina hiyo.

Je, Wizara inakabilianaje na changamoto hiyo ili kusaidia jamii za aina hizo? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba imekuwa ni kikwazo kubwa kwa wanawake walio wengi hasa kwenye maeneo ya vijijini kuweza kuungana na kutengeneza *SACCOS* kwa kufuata *strictly* na yale masharti ya *SACCOS* ambayo ni lazima kuwe na kiingilio na kuweka amana na kuendelea kujiwekea akiba.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa sasa hivi kwenye zile Halmashauri ambako hakuna akinamama ambao wana uwezo wa kuanzisha *SACCOS* Maafisa Maendeleo wa Jamii kwenye ngazi ya Kata wana wajibu wa kuhamasisha wanawake kujiunga kwenye

vikundi vya wanawake 5 mpaka 15 wanawapa mafunzo ya ujasiriamali na hao akinamama wanapata mkopo.

Nasema pale ambapo kuna *SACCOS* ambazo zipo *strong* zinaweza zikafanya kazi vizuri ndipo ambako tunaangalia uwezekano wa kupitisha fedha, na pale ambapo hakuna Maafisa Maendeleo wa Jamii watafanya kazi ya kuwahamasisha na kutengeneza vikundi, kuwapa mafunzo ya ujasiriamali na watapata mkopo. Nashukuru.

MHE. ANTHONY M. DIALLO: Mheshimiwa Spika, ahsaten kwa kuniona. Naomba niulize swali moja la nyongeza. Kulingana na utafiti ambao hatujaukamilisha kuhusu fedha za mabiliboni ya JK, inaonyesha kwamba *rate* au kiwango cha marejesho hasa kwenye Benki ya *CRDB* hata Benki ya *NMB* kilikuwa ni kizuri sana ukilinganisha na marejesho ya fedha ambazo zilikopeshwa kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Sasa nauliza kwa vile Programu hiyo ni nzuri; na kwa vile kutumia Wizara moja tu au kutumia njia moja haitoshelezi ukilinganisha na ukubwa wa nchi yetu, wana onaje Wizara hii nayo wakaiga utaratibu huo uliotumika kupitia ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana wakati wa kutoa fedha kupitia mabenki niliyoyataja *NMB* na *CRDB?*

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge una hisa katika mabenki hayo! (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba fedha za Mheshimiwa Rais mabilioni ya JK ni fedha zilizo nyingi.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme utangulizi ni kwamba fedha za mabilioni ya Mheshimiwa Rais zinazopitia mabenki ya *CRDB* na *NMB* ni fedha zilizo nyingi ukilinganisha na fedha ambazo sisi Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto tunazitoa ambazo ni kati ya shilingi milioni 4 na shilingi milioni 8, na lengo la milioni 4 na milioni 8 ni kupeleka mikopo midogo midogo kwa wanawake ambao hawana uwezo wa kukopa kwenye Taasisi kubwa za fedha kama Benki.

Kwa hiyo, ningependa tu nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi uwezo wetu wa kupeleka hiyo fedha kidogo sana kwenye mabenki ya *CRDB* na *NMB* zitakuwa zinaishia kwenye makaratasi na kwenye *operation cost.* Hivyo, imekuwa ni jambo la busara tuendelee kutoa hizo fedha zetu kidogo kdogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nafikiri kama tutapata mtaji mkubwa tutafikiri hivyo, lakini kwa sasa ni vikundi vidogo vidogo kupitia Halmashauri pamoja na kupitia pale ambapo kuna *SACCOS* za wanawake ambazo zinafanya vizuri. (*Makofi*)

Na. 127

Utamaduni wa Kukeketa

MHE. HAFIDH ALI TAHIR aliuliza:-

Kwa kuwa, mara nyingi Serikali imekuwa ikiungana na Jumuiya za Kimataifa kupinga utamaduni wa ukeketaji ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikizingatiwa kuwa, katika Mikoa mingi hapa nchini kama vile Manyara, Singida, Dodoma, Mara na Arusha bado tabia hiyo inaendelezwa; na kwa kuwa, semina nyingi zimekuwa zikitolewa kwa Wabunge juu ya athari za tendo hilo na Serikali pia imekuwa ikisisitiza suala nzima la kudumisha utamaduni wa Tanzania:-

(a)Je, kukeketa sio utamaduni wa baadhi ya Watanzania?

(b)Je, pamoja na kutoa tahadhari kuwa tendo lina athari, Serikali imefanya uchunguzi gani wa kugundua sababu zinazofanya baadhi ya makabila kuwa wakaidi na kutokuacha tendo hilo?

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatvyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa ukeketaji ni sehemu ya utamaduni wa baadhi ya makabila hapa Tanzania. Lakini utamaduni huu unaleta madhara makubwa kwa wanawake na watoto wa kike hivyo haufai kuendelezwa. Ni vyema jamii husika ikatambua kuwa ukeketaji ni ukatili dhidi ya wanawake na watoto wa kike na husababisha madhara makubwa kisaikolojia na kiafya. *(Makofi)*

Kwa upande wa kiafya husababisha matatizo wakati wa kujifungua, huharibu maumbile na huweza kusababisha maambukizi ya UKIMWI kutokana na vyombo vinavyotumika. Mara nyingine husababisha kifo kutokana na mwathirika kupoteza damu nyingi au kwa kupata maambukizi ya magonjwa mengine. *(Makofi)*

(b) Utafiti uliofanywa na Serikali kupitia *Demographic Health Survey (HDS)* 2004/2005 na nyingine zilizofanywa na mashirika yasiyo ya Kiserikali zimeonyesha sababu kubwa zinazofanya baadhi ya makabila kutoacha tendo hilo zinazotokana na imani potofu kama zifuatavyo:-

(i) Usafi – kama njia moja ya kumweka mwanamke au msichana katika hali ya usafi.

(ii) Ni ishara ya kumtoa msichana kutoka utotoni kuingia ukubwani.

(iii) Kuweka utayari kwa kuolewa.

(iv)Kupunguza hamu ya tendo la kujamiana.

(v)Msichana kutambulika na kukubalika na jamii.

(vi)Kuwaandaa wasichana kuhimili uchungu wa kuzaa.

(vii)Fikra kuwa huzuia ugonjwa wa lawalawa.

(viii)Wazazi kupata heshima katika jamii.

(ix)Imani ya kuwafurahisha wahenga.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu naomba nichukue fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, viongozi na Serikali ngazi za Mkoa, Wilaya Kata hadi Vijiji, wakiwemo Waheshimiwa Madiwani, Viongozi wa kimila, viongozi wa dini na vyama vya siasa na jamii nzima kuunga mkono juhudi zinazofanywa na Serikali yetu na Mashirika yasiyo kuwa ya Kiserikali katika vita vya kuutokomeza ukeketaji hapa nchini.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa sababu Serikali inazijua imani potofu tisa zinazofanywa na baadhi ya makabila, lakini Serikali hiyo hiyo imewaomba Waheshimiwa Wabunge kuendelea kutilia mkazo ukatazaji wa suala hili.

La kwanza, inapotokea Mbunge ametilia mkazo suala hili na amekosa Jimbo kwa sababu. Je, Serikali ipo tayari kumpatia nafasi ili arudi hapa Bungeni? (*Makofi/Kicheko*)

La pili, Mheshimiwa Spika, ukeketaji ni kitendo kibaya katika tamaduni zetu. Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kuiambia jamii ya Watanzania hivi sasa kuna utaratibu gani mwingine ambao pia unafaa kukataza ukeketaji usifanyike hapa Tanzania?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali yetu inatilia mkazo kupambana na suala la ukeketaji kwa sababu linaleta madhara makubwa ya kiafya na kisaikolojia kwa wanawake, hivyo ni unyanyasaji wa kijinsia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wetu tunapokwenda kusimama kuomba kura tunawaambia wananchi kwamba tutafanya kazi pamoja na wao kuleta maendeleo kuondoa maovu katika jamii, na ovu kubwa ambalo lipo katika jamii linalotuletea aibu kama nchi ni ukeketaji wa wanawake.

Hivyo, Mheshimiwa Mbunge kama atasimama ukawaelimisha watu na siyo kutumia lugha chafu ukaanza kuwaelezea vizuri matatizo yanayotokana na ukeketaji na heshima ya mwanamke Mheshimiwa Mbunge wanawake wote watakupigia kura usiwe na wasiwasi. (*Makofi*)

La pili, pamoja na ukeketaji kuna mila nyingine potofu. Napenda tu kuzungumzia mbili au tatu ambazo zinafikiri kwamba zikiondolewa zitaweza zikapunguza matatizo yaliyo makubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mila moja potofu ambayo kweli inawakandamiza wanawake ni ile mila ya kuwanyima wanawake haki ya kupata urithi hususan wanaume zao wanapofariki. Inamfanya mwanamke anakosa utu wake kama mbia muhimu katika kuleta maendeleo ndani ya familia na katika Maendeleo ya nchi hii. Hiyo ni mila moja potofu. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge mshirikiane na akinamama ambao wanapambana kuwasaidia wajane wasikose haki yao ya urithi pamoja na watoto yatima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mila nyingine potofu ni ya urithi wa wanawake, unapomrithi mwanamke unamfanya mwanamke kama ni kitega uchumi tu ambacho kinaweza kikatoka kwa mtu moja kwenda kwa mtu mwingine, tunamnyima utu wake. Pamoja na kumnyima mwanamke utu wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kuna matatizo mengine ya maradhi ya UKIMWI yapo siku hizi na hili limechangia sana kuwepo kwa UKIMWI katika jamii nyingine za nchi hii.

La mwisho, ni lile la kutokumpa mtoto wa kike fursa ya kusoma kama mtoto wa kiume. Naomba nichukue fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kwamba mwanamke ni sehemu kubwa ya kuleta maendeleo na akipata elimu atachangia zaidi katika kuondoa umaskini katika nchi hii. Ahsanteni. (*Makofi*)

SPIKA: Sikutazamia swali la nyongeza baada ya majibu mazuri kama haya. Swali la mwisho la nyongeza, Mheshimiwa Switi.

MHE. ELIETTA N. SWITI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba sasa niulize swali moja ndogo tu la nyongeza. Kwa kuwa ukeketaji ni kumdhalilisha mwanamke. Je, Serikali haioni kwamba ile Jimbo *allowance* ingeelekezwa huko katika kupiga marufuku kitendo hii ingefaa? Ahsante.

SPIKA: Hilo ni jambo la hiari kwa Mbunge ambaye yupo tayari kupeleka posho yake huko. Sasa ni zamu ya Maliasili na Utalii, swali linaulizwa na Mheshimiwa

Rosemary Kirigini, Viti Maalum Mara, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o kwa niaba ya Mheshimiwa Rosemary Kirigini. *(Makofi)*

Na. 128

Malalamiko na Maslahi ya Wafanyakazi Katika Hoteli za Kitalii

(MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O (K.n.y. MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI) aliuliza:-

Kwa kuwa yamekuwepo malalamiko mengi ya wafanyakazi waliopo kwenye hoteli za kitalii ikiwemo hoteli ya Seronera *Wildlife Lodge* na kwamba wafanyakazi kwenye hoteli hizo hufanya kazi kwa saa nyingi huku wakilipwa mishahara midogo; na kwa kuwa, miongoni mwa wafanyakazi hao wapo walioajiriwa kwa miaka mitatu hadi minne kama vibarua:-

(a)Je, Serikali haioni kuwa zipo sababu zote kumchukulia hatua mmiliki wa hoteli hiyo kwa kutofuata sheria na haki za wafanyakazi?

(b)Je, kwa nini mmiliki huyo ameondoa *service charge* waliyokuwa wanapata wafanyakazi kama ilivyo katika hoteli nyingine?

SPIKA: Katika hatua hii napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa kazi nzuri sana anayoifanya ya kujibu maswali haya, na mimi yananipa afueni hata nyumbani. (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kisheria waajiri wote nchini wana uhuru wa kujipangia viwango vya mishahara ili mradi isiwe chini ya kima cha chini kinachowekwa na Serikali. Hoteli nyingi za kitalii, ikiwemo hoteli ya Seronera hulipa mishahara pamoja na nyongeza inayotokana na mauzo *(service charge).* Nyongeza hii ni motisha kwa wanyakazi na mara nyingi huwa ni makubaliano kati ya uongozi wa Hoteli kulipa au kutolipa wafanyakazi wote *service charge* ambayo ni asilimia 5 ya mauzo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kulikuw ana malalamiko kuhusu maslahi ya wafanyakazi wa hoteli mbalimbali ikiwemo *Seronera Wildlife Lodge*. Malalamiko haya yalifikishwa mbele ya Chama cha Wafanyakazi wa Hoteli (CHODAWU) kufuatia hali hiyo, tarehe 24 Januari, 2009, CHODAWU na mmiliki wa Hoteli ya Seronera *(Hotel and Lodges)* walisaini mkataba wa makubaliano ya hali bora na maslahi ya wafanyakazi wa hoteli ukijumuisha malipo yanayotokana na *Service Charge.*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo katika jitihada za kuhakikisha kuwa wafanyakazi katika hoteli mbalimbali wanapatiwa haki zao, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, ilifanya uchunguzi hivi karibuni na kubaini kuwa hoteli nyingi hazina matawi ya chama cha wafanyakazi, CHODAWU. Hali hii inawapunguzia wafanyakazi nguvu ya kudai maslahi yao ikiwemo mishahara bora na stahili nyingine. Serikali inaendelea kuhimiza wafanyakazi wa mahoteli kujiunga na chama chao cha wafanyakazi chenye jukumu la kutetea maslahi yao na vile vile waajiri kuheshimu na kufuata sheria za nchi.

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa swali la msingi linauliza mambo ambayo yanagusa maslahi ya Watanzania wengi ikiwemo ni pamoja na mishahara midogo, kufanyishwa kazi kwa muda mrefu kama vibarua na manyanyaso ya aina mbalimbali. Na kwa kuwa tangu tumeanza uwekezaji katika nchi yetu hatujafanya tathimini ya kina.

Je, Serikali sasa iko tayari ili kuondoa manyanyaso haya na kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania hasa wafanyakazi wetu kufanya uchunguzi na utafiti na tathimini ya kina kubaini jinsi wawekezaji wetu wanavyowajali Watanzania waajiriwa kwa mujibu wa sheria zilizoko katika nchi yetu?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Mbunge kwamba wawekezaji wanakuja kwenye sekta mbalimbali na utafiti au tathimini imekuwa ikifanyika kwa nyakati tofauti kwa sekta husika, nitatoa kwenye sekta ya madini si muda mrefu Mheshimiwa Rais aliunda Tume ambayo ilifanya utafiti wa mazingira ya uwekezaji pamoja na maslahi ikiwemo suala la maslahi ya wafanyakazi. Taarifa kama hizo zinafanyika pia kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo sekta ya utalii kama ambavyo nimesema hapa kwamba sisi kama Wizara tunazungumza na wawekezaji wanaowekeza kwenye sekta yetu.

Kwa hiyo, kimsingi ninadhani si lazima sana kusema tufanye tathmini ya kijumla ya kitaifa kwenye sekta zote kwa sababu kila sekta kumekuwa kukifanyika tathmini na mara nyingi wawekezaji hawa wanapewa miongozo inayohusu sheria za nchi yetu na wanazizingatia.

Na. 129

Wananchi Kupatiwa Ardhi ya Kulima

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE alijibu:-

Kwa kuwa wananchi wengi wanakosa ardhi ya kutosha kutokana na kuzuia kulima zaidi kwa madai ya kupatikana na hifadhi ya misitu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi hao wanaopakana na mipaka ya hifadhi wapate maeneo ya kulima?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sheria ya misitu namba 14 ya mwaka 2002 sehemu ya (v), kifungu cha 26 kifungu kidogo (h) inakataza kufyeka, kulima au kumega ardhi yoyote ambayo ni msitu wa hifadhi kwa ajili ya kilimo au kwa kusudio jingine lolote.

Aidha, kifungu namba 17 cha *one life conservation bill* ambayo Bunge lako Tukufu lilipitisha hivi juzi nacho kinakataza shughuli za kilimo kwenye maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanaopatikana na misitu ya hifadhi kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria ya misitu wanaweza kufanya shughuli kama vile ufugaji nyuki, utalii ikolojia, kilimo cha uyoga, kutengeneza mapambo na vikapu, kutokana na malighafi za msituni badala ya kutegemea kilimo pekee.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanaopakana na hifadhi za misitu wanatakiwa waelimishwe umuhimu wa kuwepo kwa hifadhi hizo na kwamba waone kuwa ni mali yao na wasaidie kusimamia na kuzilinda.

Wizara yangu kupitia mpango shirikishi na jamii katika kuhifadhi rasilimali za misitu inawezesha wananchi wa maeneo haya kusimamia na kufanya shughuli mbadala ambazo ni endelevu ndani na nje ya hifadhi.

Aidha, nashauri Mheshimiwa Mbunge, pamoja na Watanzania wote kwamba ni vizuri tukazingatia utaratibu wa *(land use Plan)* kwenye vijiji ili kuepuka uvamizi katika maeneo ya hifadhi za misitu.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika Wilaya ya Kasulu idadi ya watu imeongezeka tofauti na siku za nyuma na kwa kuwa wananchi wanahitaji ardhi kwa ajili ya kilimo si kwa ajili ya ufugaji nyuki pamoja na uyoga na kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Kasulu chakula chao kikuu ni mahindi, maharage na kadhalika:-

Je, katika kusaidia wananchi si vema mipaka ya hifadhi ingeongezwa ili wananchi waweze kupata ardhi kwa ajili ya kilimo?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwepo na ongezeko kubwa la binadamu na mahitaji ya ardhi yamekuwa yakiongezeka na hili limekuwa likijitokeza kila wakati hasa kwenye mazingira ambayo kuna hifadhi zinazopakana na wananchi.

Mheshimiwa Spika, mtazamo wetu kama Serikali ni kwamba ni vizuri tukazingatia matumizi bora ya ardhi na mpango huu wa matumizi bora ya ardhi ni vizuri ukaratibiwa kwenye ngazi zote za utawala kuanzia vijijini hadi Mikoani.

Kwa hiyo, mimi naamini kwamba ongezeko la binadamu tulionao halijafikia kiwango cha kuwaza kumega maeneo yaliyohifadhiwa kwa sababu kufanya hivyo tutakuwa tunaathiri sana uendelevu wa kizazi kijacho. Aidha, nitoe tu mfano kwamba tusipokuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi, tatizo hili litaendelea kutusumbua.

Nchi ya Burundi kwa mfano ni ndogo kuliko Mkoa wa Morogoro lakini ina wananchi zaidi ya milioni 6 wanalima, wanaishi na kuna sehemu ambayo imehifadhiwa na hawaingilii. Kwa hiyo, naamini kwamba bado tunaweza tukawapanga wananchi wetu tukaweka maeneo ya hifadhi, yakawepo maeneo ya kilimo na yakawepo maeneo ya hifadhi.

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Spika, ni kweli majibu ya Mheshimiwa Niabu Waziri kwamba ni lazima yawepo matumizi mazuri ya ardhi. Lakini hifadhi nyingi za misitu zimewekwa miaka kadhaa iliyopita kabla nchi hii haijapata uhuru. Kwa mfano hifadhi ya Msitu wa Msagenya kule Mpanda wakati idadi ya watu ilikuwa ni kidogo. Je, Serikali sasa itakuwa tayari kupanua mipaka ya hifadhi hizi ambazo zimezingirwa na makazi ya watu?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ni kweli hifadhi nyingi za misitu zilitangazwa miaka mingi sana iliyopita na kwa kiasi kikubwa hifadhi nyingi zimezingirwa na kusongwa sana na watu ni nyingi zimevamiwa kwa kiasi kikubwa. Tatizo hili ni kubwa lakini utaratibu wa ku- *de-gazette* hifadhi ya misitu umeelezwa kwenye sheria. Kwa hiyo, nafikiri kwamba pengine njia nzuri ya kufuata ni kufuata utaratibu uliowekwa kisheria sisi kama Wizara tutafanya tathimini kujua hali halisi ya misitu yetu na kwa kufuata taratibu za sheria zilizowekwa jambo hili tunaweza tukazungumza kuona namna gani tuweze ku-*manage* misitu yetu effectively.

MHE. TEDDY L. KASSELA – BANTU: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika majibu yake ya msingi amekiri kwamba elimu hiyo haijawafikia wananchi vizuri kujua mipaka ya hifadhi. Na kwa kuwa katika *television* jana tumeona sehemu za Rombo watu wamefyekewa mazao yao ya chakula kama mahindi na maharage kwa sababu wamelima katika hifadhi.

Je, Serikali haioni kwamba sasa wangeachia mazao yao ya chakula, wakavuna wakizingatia hali halisi ya sasa duniani chakula hakuna? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba pamoja na nia yetu nzuri ya kudhibiti uvamizi katika maeneo ya misitu. Nikiri kabisa kwamba kuna mambo mengine ambayo yanafanyika *they are not acceptable* kwa maana kwamba watu wanapokuwa hadi wameingia wamelima mtu hawezi akalima na mazao yakakua kwa siku moja.

Kwa hiyo, haya ni mapungufu ya kiundaji *specifically* hili la Rombo tutalifuatilia, lakini utaratibu ni kwamba tunawajibika kudhibiti kabla hawajaingia. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili, ahsante kwa jibu zuri. *(Makofi)*

Na. 130

Ujenzi wa Mabwa Kwa ajili ya Mifugo

MHE. BUJIKU P. SAKILA aliuliza:-

Kwa kuwa, upungufu wa maji ni moja ya matatizo ya msingi yanayowakabili wafugaji; na kwa kuwa katika maeneo yao yapo maeneo mengi yanayoweza kutumika kwa kuchimba mabwawa ya kutunzia maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali:-

(a) Je, kwa nini Serikali isiweke na kutekeleza mpango kabambe kama wa *MMEM* na *MMES* kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa nchini na utoaji wa elimu ya kilimo cha nyasi kwa ajili ya mifugo?

(b) Je, wafugaji wanaoishi karibu na shamba la Mifugo la Mabuki wanaweza kunufaika vipi kutokana na elimu inayotolewa kituoni hapo?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:- Mheshimiwa Spika, kwanza naomba radhi kwa sauti yangu, naumwa kikohozi na mafua.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bujiku Sakila - Mbunge wa Kwimba lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inakubali kuwa mipango kama iliyotumika katika kuinua ubora wa viwango vya elimu kwa Shule za Msingi na Sekondari ingeweza kutumika kutatua tatizo la maji kwa mifugo na matumizi ya binadamu ikiwa ni pamoja na kumwagilia malisho ya mifugo. Hata hivyo ujenzi wa mabwawa na mabirika kwa ajili ya mifugo umehusishwa kwenye Mipango ya Maendeleo ya Kilimo Wilayani *(DADPs)* kama Mkakati wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo *(ASDP)* nchini. Mwaka huu 2008/2009 mipango ya *DADPs* imelenga kujenga na kukarabati malambo 104 nchini kote, ambapo mapya ni 93 na yatakayonyiwa ukarabati ni 11.

Miradi mingine inayojihusisha na ujenzi wa malambo ya maji kwa mifugo nchini ni pamoja na *DASIP, PADEP, TASAF*. Kwa mfano katika kipindi cha Julai – Desemba, 2008 ujenzi wa malambo mapya 34 na ukarabati wa malambo 21 umefanyika kupitia *DADPs, DASP, PADEP* na *TASAF*. Aidha, Wizara ya Maji na Umwagiliaji inakamilisha taratibu za kupata Wakandarasi wa kujenga mabwawa 13 sehemu mbalimbali za nchi yetu ambayo pia yatatumika kunyweshea mifugo.

(b) Mheshimiwa Spika, Shamba la Uzalishaji Mifugo la Mabuki pamoja na kuwa huzalisha mitamba ya chotara kwa ajili ya kuwauzia wananchi wanaopenda kufuga, huzalisha pia mbegu za malisho, hufanya utafiti na pia hutoa mafunzo ya ufugaji kwa vitendo. Mafunzo yanayotolewa hapo ni pamoja na ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa, mbuzi wa maziwa na nyati maji ambao wapo hapo shambani. Aidha, mafunzo mengine ni ya matumizi ya uhamilishaji, matumizi ya wanyamakazi, uzalishaji wa malisho bora na mafunzo mengine ambayo yataonekana kuwa ni muhimu kwa wafugaji.

(c) Mheshimiwa Spika, pamoja na chuo hicho cha mafunzo kuanzishwa hapo shambani, Wizara imeanzisha huduma za uhamilishaji katika Shamba la Mabuki ambapo wafugaji kutoka Mikoa ya Kanda ya Ziwa hupata mafunzo ambayo ni muhimu kwa ajili ya kuboresha mifugo. Mwaka 2008 wanafunzi 20 walihitimu mafunzo hayo. Wafugaji wanaozunguka shamba la mifugo la Mabuki hunufaika kwa kujifunza kutoka shamba hilo kwani lengo mojawapo la shamba ni kuwa mfano wa kuigwa na wafugaji wanaozunguka, hususan katika kudhibiti magonjwa yatokanayo na kupe kwa kutumia majosho, matumizi ya madume bora ili kubadili mifugo kwa lengo la kuzalisha maziwa na nyama zaidi. Wafugaji wa Mabuki wana nafasi ya kufaidika zaidi ukilinganisha na wananchi wanaoishi mbali na shamba kwa kuwa wanaweza kufika shambani na kupata elimu ya ufugaji bora kutoka kwa wataalamu walioko shambani hata kama kwa wakati huo hakuna vipindi chuoni.

MHE. BUJIKU P. SAKILA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nina maswali mawili tu ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, kwa kuwa elimu inatokana na mafunzo yaliyotolewa katika shamba hilo imefungiwa kama wale ng'ombe wenyewe waliokuwa katika shamba hilo kwa muda wa miaka mingi kiasi kwamba hata wale wafugaji ambao wako kandokando ya shamba hilo mifugo yao haijabadilika kwa miaka mingi sana: Je, Serikali inaweza kuelezea utaratibu unaoweza kutumika kuziwezesha Halmashauri kupeleka wananchi wake na hasa wafugaji kuingia ndani ya shamba na kujifunza elimu inayotolewa pale?

La pili, swali langu la msingi lilikuwa linaongelea mabwawa, jibu limejikita kwenye malambo, lakini nilichokuwa nataka kufahamu, mabwawa yanaweza kutumikaje katika kilimo cha nyasi za mifugo? Je, haya yaliyotajwa yanayo miradi ya kilimo cha nyasi kwa ajili ya mifugo na kama hayana kwa nini?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, ukweli katika kile chuo kuna wakati kilifungwa, lakini sasa hivi tumekifungua na kiko wazi kwa yeyote yule anayetaka kuja kukitumia. Mfano katika mwaka wa 2006/2007 wananchi 288 walipata mafunzo mbalimbali. Vile vile mwaka 2007/2008 wanafunzi 90 walichukuliwa ambao ni wananchi wanazunguka na wengine wanatoka Halmashauri, na mwaka 2008/2009 mafunzo yametolewa kwa watu 46. Mafunzo yanayohusu magonjwa ya kupe, homa ya bonde la ufa, kichaa cha mbwa, uundwaji wa vikundi vya wafugaji, utunzaji wa ng'ombe wa maziwa, uendelezaji nyanda za malisho, shamba la darasa na uhamilishaji. Kwa hiyo, hiki chuo kiko pale kusaidia wananchi na yeyote atakayekuja. Kama ukitokana na wananchi ambao wamenyimwa nafasi hiyo tunaomba Wizara iarifiwe na tutahakikisha kwamba wananchi wa Halmashauri wanapewa hiyo elimu.

Pili, haya mabwawa ambayo yanaandaliwa ni kwa ajili ya maji ya kunywa na maji ya mifugo. Kwa hiyo, kama italazimika yakatumika kwa ajili ya kumwagilia majani ya malisho hilo litafanyika itategemea na hali ya huko yalipo.

Na. 131

Ripoti ya Wafugaji wa Ihefu Kuwasilishwa Bungeni

MHE. MOHAMMED HABIB MNYAA aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilishaunda Tume ya Kuchunguza suala la uhamisho wa wafugaji kutoka bonde la Ihefu na ripoti yake kuwasilishwa kwa Mheshimiwa Rais na kwa kuwa, ripoti ya Tume hiyo haijawasilishwa Bungeni:-

(a) Je, ni sababu zipi zinazopelekea ripoti ya Ihefu isiwasilishwe Bungeni?

(b) Je, hali hiyo haivunji utaratibu wa Utawala Bora kwa kubagua ripoti za kupeleka na kutokupelekwa Bungeni?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu maswali (a) na (b) ya Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni kama ifuatavyo:-

(a) Suala la ripoti ya Tume ya Ihefu iliyoundwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano limekuwa likijitokeza mara kwa mara hapa Bungeni. Itakumbukwa hata wakati wa kuhitimisha Bajeti ya Wizara ya mwaka 2008/2009 Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo Mifugo na Uvuvi alilitolea maelezo suala hilo akinukuu maelezo ambayo tayari yalishatolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba Rais ana mamlaka kikatiba kuunda Tume.

Aidha, Katiba pia haimlazimishi Mheshimiwa Rais kuleta ripoti zote za Tume hapa Bungeni. Naamini Mheshimiwa Rais akiona kuna ulazima wa kuleta hiyo ripoti atafanya hivyo. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Mnyaa na sisi wote tumuachie Mheshimiwa Rais wetu aifanyie kazi ripoti hii.

(b) Mheshimiwa Spika, ripoti kutoletwa Bungeni haivunji utaratibu wa utawala bora bali inaudumisha. Kwa kuunda Tume na kukubali ripoti ni ishara tosha kwamba Mheshimiwa Rais wetu ni mtu wa utawala bora siku zote na wote ni mashahidi wa utendaji wake ulitukuka.

MHE MOHAMED HABIB MNYAA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nami nikiri kwamba hiyo ni *decision* ya Rais kuleta Bungeni au kutoleta. Sasa swali ni kwamba: Kwa kuwa Raia amechaguliwa na wananchi na sisi Wabunge pia tumechaguliwa na wananchi na kwa kuwa wananchi ndio wanaotutuma na wana hamu kubwa sana ya ripoti hii kujadiliwa Bungeni hasa baada ya kuona Ripoti ya Jaji Bomani na ile Ripoti ya Richmond ya Mheshimiwa Mwakyembe ilipojadiliwa Bungeni: Je, Wizara yako sasa itafanya nini ili kukidhi kiu hii ya wananchi?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa Mheshimiwa Mnyaa, Mheshimiwa Rais amechaguliwa kwa Katiba na tumempa uwezo na tulimpa *mandate* ya asilimia 80, kwa nini tusimwachie mwenyewe aamue? Hivi mimi kama Wanyancha hapa kuweza kumwendea Rais, si anajua kazi yake! Mfano, sisi tunapotoka, kama baba ameamua jambo, ni utovu wa nidhamu wewe mtoto kwenda kumwambia baba afanye hivi. Naomba tumwachie Rais wetu. (*Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Mwera hiyo ni kweli? Basi ahsante.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa nataka kumwomba Waziri Mkuu amsaidie Elias Ndofu aliyelipa shilingi milioni 42 na sasa mifugo yake yote imezuiliwa Morogoro na inakufa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, naomba kuuliza swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa sababu ya kuanza Tume ile ilikuwa ni kwa sababu ya malalamiko mbalimbali ambayo ni pamoja na vifo vya Mifugo na watu kutojua wanakokwenda na mambo hayo na kwa Serikali kutojiandaa mahali pa kuwapeleka hawa ng'ombe: Je, jambo hili linafanana na linalotokea sasa hivi Kilosa, Ifakara na Ulanga? Isingekuwa busara kwa Serikali kungojea kwanza kujifunza yaliyotokea kule Ihefu na kwa kusitisha zoezi la sasa ili watakapofanya liweze kuleta tija kuliko kuua ng'ombe?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba matatizo yalipotokea kule Ihefu sio kwamba Serikali ilikaa ikanyamaza ilichukua hatua ambazo ni mahsusi kabisa. Kwanza ilihakikisha kwamba ng'ombe wamepelekwa sehemu ambazo ng'ombe sio wengi, kwa mfano ng'ombe 15,100 zilipelekwa Mkoa wa Lindi. Pili Ruvuma walipelekwa ng'ombe 22,000. Mbeya - Chunya walipelekwa ng'ombe 100,000. Mkoa wa Pwani - Kisarawe

ng'ombe 6,600, Rufiji walipelekwa ng'ombe 110,000, halafu sio kwamba tuliwaacha, walipofika pale tumewachimbia malambo. Kwa mfano Kilwa tumechimba malambo katika vijiji vya Naliandeko, Matandu, Nangurukuru na Lindi tumechimba katika Mjimwema na majosho vile vile tumefuatilia.

Kwa hiyo, kama matatizo yanajitokeza na ambayo ni mabaya, lazima Serikali ichukue hatua. Kama hawa watu wanafanya matatizo sehemu hizo nyingine, lazima washughulikiwe. Huwezi kungojea Ihefu! Hii ya Ihefu imeshughulikiwa. Vile vile sio kwamba Serikali imenyamaza, sasa hivi tunajua kwamba tuna tatizo na tunasikitikia wakulima na wafugaji. Kwanza mimi natoka katika sehemu ya wafugaji. Sasa hivi Serikali imejiandaa Kiwizara kuanza kuleta Muswada wa Sheria ya Kusajili na Kutambua Mifugo; mifugo mingapi ipo katika sehemu mbalimbali. Hiyo itasaidia Kamati hiyo kama mtu anakwenda kuvamia pale itafahamika.

Pili, rasimu ya Muswada wa Sheria unaohusu Usimamizi wa Maeneo ya Malisho na Vyakula, *Dressing Land Act and Animal Feed* tunaleta hapa kwa ajili ya hayo maeneo yaweze kulindwa watu wasiwaondoe wafugaji kiholela.

Tatu, tunajaribu kwa kupitia *DADPs* kwenda miundombinu kwa sababu watu wengi wanahama kwa sababu hamna malambo ama hamna majosho. Hayo tunayaweka na fedha nyingi zimetolewa kwa *DADPs*, kwa hiyo, Serikali yetu inafanya kazi kwa uimara.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, napenda kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa migogoro nchini imekuwa mikubwa sana kati ya wakulima na wafugaji na wakulima wanaweka mashamba kuzungusha maeneo ya maji na ng'ombe kukosa mapitio ya kuja kunywa maji. Je, Serikali haioni kwamba wafugaji wanaponyangw'anywa mifugo na kuuza bila utaratibu huu ni unyanyasaji mkubwa na ni lini Serikali wataweka mpango kabambe wa kuwaokoa wafugaji wanaokimbiakimbia na kunyanyasika katika nchi yao?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, wakulima na wafugaji ni Watanzania na mfugaji hatakiwi kunyanyaswa na hakuna sheria inayosema mkulima amnyanyase mfugaji. Sasa kama kuna sehemu watu wananyang'anya wafugaji ng'ombe zao na kuuza, huo ni uvunjaji wa sheria na sheria inatakiwa kuchukua mkondo wake. Kama watu wanatakiwa kuhama lazima waondolewe kwa heshima na taadhima kuonyeshwa sehemu ya kwenda.

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunahamia sasa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; naomba utulivu, tafadhili utulivu. Swali linalofuata linaelekezwa Wizara ya Mambo ya Nchi na linaulizwa na Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mbunge wa Tumbatu.

Na. 132

Mpango wa Ulinzi Shirikishi Jamii

MHE. RAJABU HAMAD JUMA aliuliza:-

Kwa kuwa, mpango wa Ulinzi Shirikishi Jamii wa Jeshi la Polisi unaonyesha mafanikio katika baadhi ya Mikoa:-

(a) Je, ni Mikoa gani inaongoza kwa kufanikisha mpango huo?

(b) Je, ni Mikoa gani inaonyesha mafanikio hafifu katika mpango huo?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rajabu Hamad Juma, Mbunge wa Tumbatu lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ulinzi shirikishi au Polisi jamii ni ushirikiano wa Jeshi la Polisi na jamii kufanya kazi kwa pamoja, kwa kupanga mikakati na kutafuta njia sahihi na endelevu za kudumisha usalama wa watu na mali zao ili kuleta amani na utulivu katika jamii. Huu ni mkakati mpya wa utendaji wa Jeshi la Polisi wenye lengo la kuweka mazingira ya ushirikiano wa dhati baina ya wananchi na Jeshi la Polisi. Wizara ipo kwenye mchakato wa kuunda sera ya Usalama wa raia ambapo ulinzi shirikishi ni miongoni mwa mikakati ya kutekeleza sera hii.

Mheshimiwa Spika, viongozi wa Serikali na wa kisiasa wako mstari wa mbele katika himaya zao kuendelea kuwahamasisha wananchi kutekeleza mpango huu. Mwitikio katika Mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani ni mzuri, hivyo kwa sasa ni mapema mno kutamka kwa uhakika ni Mikoa gani inayoongoza kwa kufanikisha mpango huu na ni Mikoa gani inayoonyesha mafanikio hafifu. Hivi sasa Mikoa yote inaendelea kuboresha mpango huo, kwa kuanzisha vikundi shirikishi vya ulinzi kati ya wananchi na Polisi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wadau mbalimbali ambao kwa namna moja au nyingine wamekuwa wakijitokeza kwa dhati kuunga mkono mpango huu kwa kujenga vituo vya Polisi kutoa vitendea kazi ikiwemo pikipiki, baiskeli, makoti ya mvua na fedha taslimu.

MHE. AL-SHYMAA JOHN KWEGYIR: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nina swali moja dogo la nyongeza.

Je, Mikoa inayoongoza kwa kufanikisha mpango wa ulinzi shirikishi ndio iliyofanikisha kupunguza mauaji ya vikongwe na albino na ile Mikoa ambayo haifanyi vizuri ndiyo inayoongoza kwa mauaji hayo?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika majibu yangu ya msingi, katika kipindi hiki ni mapema mno kutamka kwa uhakika ni Mkoa gani unaoongoza na kufanikisha mpango huu na ni Mikoa gani inayoonyesha mafanikio hafifu. Lakini ningependa kusisitiza kwamba Wizara yangu

itaendelea kushirikiana na wananchi kwa ujumla kuhakikisha kwamba Mikoa ambayo inayoongoza katika mauaji ya albino na vikongwe mpango wa ulinzi shirikishi utaimarishwa na Wizara yangu itajitahidi kuhakikisha kwamba mauaji haya yanasimamishwa.

Na. 133

Mkakati wa Kuwatambua Watanzania Halisi

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali iko katika mchakato wa kutoa vitambulisho vya uraia kwa Watanzania wote:-

Je, kuna mkakati gani wa awali wa kuwatambua Watanzania halisi hasa ukitilia maanani katika Mikoa ya Mipakani kama vile Kigoma, Kagera, Mbeya na kadhalika, kuna tatizo la kuwatambua wahamiaji haramu wa muda mrefu?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambila, napenda kutoa ufafanuzi kwamba vitambulisho vinavyotarajiwa kutolewa ni vitambulisho vya Utaifa na sio vya Uraia.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya ufafanuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambila kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka utaratibu wa muda mrefu wa kuwaorodhesha wageni waishio nchini hasa katika maeneo ya mipakani. Wageni hao huorodheshwa kwa lengo la kuwatambua raia, wageni na wahamiaji haramu. Zoezi hili husimamiwa na viongozi wa Serikali za Mitaa na Vijiji na huratibiwa na Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, utaratibu mwingine wa kuwatambua Watanzania halisi ni kupitia taarifa za vizazi ambazo zinatunzwa na *RITA* kwa upande wa Tanzania Bara na Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali chini ya Wizara ya Katiba na Utawala Bora kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aidha, Serikali pia inaandaa mpango maalum wa kuhakikisha kwamba vitambulisho vya Utaifa vitatolewa kwa kila mkazi aliyepo nchini kwa mujibu wa hadhi yake ya uwepo wake hapa nchini.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Spika, kwanza kwa kumbukumbu sahihi naomba niseme ni Mbunge wa Mtambile sio Mtambila, baada ya hapo naomba kuuliza suala moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imekiri kwamba zoezi hili huendeshwa na viongozi wa Serikali za Vijiji na Mitaa. Kwa kuwa wananchi

walioko mipakani bado wanakamatwa ovyo ovyo kwa kudhaniwa kwamba wao ni wageni: Je, Serikali ina mkakati gani wa ziada wa kuhakikisha Watanzania hawa walioko mipakani hawakamatwi ovyo ovyo na viongozi wa Vijiji na Mitaa wanaowakamata watu hawa wanapewa adhabu inayostahili?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza namwomba radhi Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim nitamke kwamba jimbo lake ni Mtambile na sio Mtambile.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ikishirikiana na vyombo vingine haisimamii kukamata watu katika mpango ovyo ovyo kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge. Wizara yangu inakamata wale watu ambao kutokana na taarifa tulizonazo, sio Watanzania na wameingia Tanzania kinyume cha sheria na taratibu za Taifa letu. Kama kutakuwa kuna eneo ambapo imebainika kwamba watu wameonewa iwe na wafanyakazi wa Wizara yangu au Taasisi yoyote nyingine ya Serikali ningemwomba Mheshimiwa Mbunge anifahamishe ili Wizara yangu ichukue hatua ipasavyo.

Na. 134

Miradi ya Wafadhili Katika Mikoa

MHE. JUMA ABDALLAH NJWAYO aliuliza:-

(a) Je, ni Mikoa gani inaongoza katika kupata miradi ya wawekezaji na ipi ina idadi ndogo ya miradi ya aina hiyo?

(b) Je, kwa nini kuna tofauti miongoni mwa Mikoa katika kupewa miradi hiyo?

(c) Je, ni hatua gani zinazochukuliwa na Serikali katika kurekebisha tofauti hizo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR Y. MZEE): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mpaka kufikia Juni, 2008, Mikoa inayoongoza kwa idadi kubwa ya miradi ya uwekezaji ni Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Kilimanjaro na Tanga na Mikoa yenye idadi ndogo ni Mikoa ya Singida, Manyara, Ruvuma, Rukwa, Kigoma, Lindi, Tabora, Dodoma na Mtwara.

(b) Mheshimiwa Spika, kutofautiana kwa miradi ya uwekezaji katika Mikoa kunatokana na sababu mbalimbali. Baadhi ya sababu hizi ni upatikanaji wa malighafi na kuwepo kwa miundombinu ya uhakika, kama vile umeme, barabara, maji na

mawasiliano. Aidha, kuwepo kwa soko la kutosha kwa ajili ya bidhaa au huduma zitakazotolewa na mwekezaji, urahisi wa kusafiri au kusafirisha bidhaa nje ya nchi au kuingiza bidhaa au malighafi kutoka nje. Kadhalika, mwekezaji mwenyewe anaweza kuwa na sababu zake binafsi zilizompelekea kuchagua Mkoa husika.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua na inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuweza kuwashawishi wawekezaji kuanzisha miradi ya uwekezaji katika Mikoa ambayo ina idadi ndogo ya miradi ya uwekezaji. Baadhi ya hatua hizo ni kama zifuatazo:-

(i) Kuboresha na kujenga barabara zinazounganisha Mikoa na kuhakikisha kuwa huduma za maji na umeme zinapatikana katika Mikoa yote.

(ii) Kuanzishwa kwa mpango shirikishi wa kuibua na kutangaza fursa za uwekezaji zilizoko katika Mikoa. Mpango huu unatarajia kuanza kwa majaribio katika Mikoa ya Rukwa, Singida, Tabora na Tanga. Mpango huu utatoa fursa ya kuitangaza Mikoa yetu.

(iii) Mwekezaji atakayeanzisha miradi mkubwa katika Mkoa ambao hauna miradi mingi atapatiwa vivutio vingi zaidi kuliko ilivyo kawaida baada ya yeye mwenyewe kuomba. Hadhi hii itasaidia kuwavutia zaidi wawekezaji kuwekeza katika Mikoa ambayo haina miradi mingi ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa wito kwa Mikoa kwa kushirikiana na kituo cha uwekezaji, kuandaa kongamano na kuwaalika wawekezaji wa ndani na nje ili kutangaza fursa zilizomo ndani ya Mkoa.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Lakini hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Mtwara imetajwa kuwa ni miongoni mwa Mikoa yenye miradi midogo ya uwekezaji, lakini Mkoa huo una rasilimali nyingi za kutosha kama vile Bandari yenye kina kirefu na ya asili, uwanja wa ndege wa kuaminika, umeme wa kuaminika, gesi ya Mnazibay, barabara inayokamilika kati ya Dar es Salaam na Mtwara sasa na kadhalika: Je, Serikali ina mpango gani mahsusi wa kuwashawishi na kuwashauri wawekezaji ili waweze kuwekeza Mtwara? (*Makofi)*

Pili, kwa kuwa Serikali iliahidi nyakati kadhaa hapa kwamba inatoa kipaumbele katika maeneo yaliyoko pembezoni mwa nchi ukiwemo na Mkoa wa Mtwara: Je, ni miradi gani ya kimaendeleo inatarajaiwa kuwekezwa Mkoani Mtwara katika muda wa miaka miwili ijayo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR Y. MZEE): Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kwamba tunaandaa mpango ili kuweza kuitangaza Mikoa iliyopo nyuma katika suala zima la uwekezaji na Mkoa wa Mtwara ukiwa ni mmojawapo, mpango huu utakapokamilika utaweza kuvutia wawekezaji kwa lengo la kuwaelekeza na kuwaonyesha fursa zilizomo katika Mkoa wa

Mtwara. Namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira, mpango utakapokamilika utavutia wawekezaji wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, la pili, nataka nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba itakapofika mwezi wa Juni, 2009, Mkoa wa Mtwara utakuwa tayari umeshapata umeme Mkoa mzima. Hali kadhalika katika kipindi cha miezi 15 inayokuja tutakuwa ile barabara inayotoka Dar es Salaam kuelekea Mtwara imeshakamilika. Kwa maana hiyo, *infrastructure* zitakapokuwa zimekamilika itatoa nafasi nzuri zaidi kuwavutia wawekezaji. Lakini nataka nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba hivi sasa kuna mpango wa kujenga kiwanda kikubwa sana cha mbolea pale Mtwara. Kiwanda hiki kitazalisha tani zisizopungua 600,000 za mbolea na kitatoa ajira isiyopungua vijana 1,000. Nataka nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba mipango ipo, avute subira mambo mazuri hayataki haraka.

Na. 135

Wananchi wa Nyamongo Kutengewa Eneo la Kuchimba Dhahabu

MHE. MWERA C. NYANGURU aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Nyamongo ambao ni wachimbaji wadogo wadogo wa madini hawana maeneo ya kuchimbia dhahabu hali inayosababisha mahusiano mabaya kati yao na Kampuni ya Barrick: Je, ni lini sasa wananchi hao watatengewa maeneo ya kuchimba dhahabu maeneo ya Nyabigena?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwera Charles Nyanguru Mbunge wa Tarime kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Barrick* inamiliki Mgodi wa Dhahabu wa *North Mara* katika Wilaya ya Tarime. Mgodi huo uko kwenye eneo la Nyabigena chini ya leseni *Special Mining Licence* SML 18/1996. Aidha, eneo la leseni ya uchimbaji madini limezungukwa na leseni za utafutaji mkubwa wa madini zinazomilikiwa na Kampuni ya Barrick. Hivyo kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 1998 leseni nyingine ziwe za utafutaji au uchimbaji madini mkubwa au mdogo haziwezi kutolewa katika maeneo ambayo tayari yako chini ya leseni zilizotangulia kutolewa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli pamekuwepo na mahusiano yasiyoridhisha kati ya baadhi ya wananchi wa Nyamongo hususan wachimbaji wadogo na wamiliki wa mgodi wa *North Mara* (*Barrick*) kutokana na maingiliano katika umiliki wa maeneo ya utafutaji na uchimbaji madini. Hivyo, kama Sera ya Madini na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 zinavyoelekeza Wizara yangu imeandaa mkakati wa kuwaendeleza wachimbaji wadogo wa madini nchini ikiwemo kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya uchimbaji mdogo.

Mheshimiwa Spika, maeneo yaliyotengwa na Serikali kwa ajili ya wachimbaji wadogo ni pamoja na Kilindi, Morogoro na Kilosa yenye jumla ya ukubwa wa kilomita za mraba 2,698.42 ambapo yalitangazwa kwenye Gazeti la Serikali GN No. 359 ya tarehe 26 Julai, 2002, Maganzo lenye jumla ya kilomita za mraba 148.7 lilotangazwa kwenye Gazeti la Serikali GN No. 528 la tarehe 3 Desemba, 2004 na Mererani lenye jumla ya kilomita za mraba 104.9 lililotangwa kwenye Gazeti la Serikali GN No. 120 ya tarehe 8 Septemba, 2009.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na utaratibu wa kuzungumza na kampuni zenye leseni za utafutaji mkubwa wa madini ili ziachie kisheria maeneo ambayo kampuni zimeshafanyia utafutaji wa madini wa kina kubaini kuwa haziwezi kuendesha uchimbaji wa madini kwa faida, lakini wachimbaji wadogo wanaweza kuchimba madini hayo na kujiongezea kipato. Utaratibu huu wa mazungumzo umewezesha kupatikana kwa maeneo yafuatayo ambayo kwa sasa yametengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Rwamgaza (Geita) hekta 710 kutoka Kampuni ya *IAMGOLD (T) Ltd*, Nyarugusu (Geita) hekta 540 kutoka ya Kampuni *IAMGOLD (T) Ltd*, Sekafi na Mumbwi (Handeni) hekta 25.84 kutoka ya Kampuni *ya Shadhilu Group (T) Ltd*, Malolo-Winza (Mpwapwa) hekta 3,900 kutoka maombi kampuni ya *Luguruni Mining Co. Ltd* na Makoro (Mbinga) ambapo *PML 53* zimetolewa kutoka *PL 513* na *517* ya Kampuni ya *World Gem Supplies Ltd.*

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo yako kwenye mchakato wa kutengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo ni Ngasamo Wilayani Magu (Hekta 229), Matabe Wilayani Chato (hekta 880) pamoja na Nyasenero (hekta 172) na Rwabasi (hekta 449) Wilayani Musoma Vijijini.

MHE. CHARLES NYANGURU MWERA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu ya kukatisha tamaa wananchi wa Nyamongo: Je, ni lini sasa Serikali itaanza mchakato kwa ajili ya kugawa maeneo kwa wachimbaji wa Nyamongo?

SPIKA: Kwa msaada tu badala ya kusema kwa kuwa hukubaliani na jibu ungesema kutokana na majibu yasiyoridhisha, badala ya kusema pamoja na majibu yasiyoridhisha. Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naheshimu sana maoni ya Mheshimiwa Mbunge, lakini nadhani kwa mkakati na taratibu zilizopo hatuamini kwamba majibu haya tunayotoa yanakatisha tamaa wananchi wa Nyamongo. Tunasema hivi kwa sababu nchi yetu inaongozwa kwa taratibu za kisheria, kanuni na misingi iliyokubalika. Tumesema tukifafanua hasa maalum kwa ajili ya wananchi wa Nyamongo, tumesema eneo lile limemilikishwa kisheria. Wote tunafahamu na Mheshimiwa Mbunge akiwa ni mmojawapo wa watu wanaoelewa kama mwakilishi wa wananchi, nchi hii haiwezi kuongozwa kwa misingi ya hisia, vinginevyo tutakuwa

tunaishia katika vurugu. Ndiyo maana tunasaema kwa kufafanua kwamba eneo la Nyamongo limegawiwa kihalali.

Nchi haiwezi kuendeshwa kwa hisia ndiyo maana tunasema Serikali imekuja na mkakati maalum, tunatenga maeneo maalum ili wananchi ambao wanahitaji kufanya shughuli za uchimbaji mdogo waende kwenye maeneo ambayo tumeyatenga kisheria pasipokuwepo na vurugu. Lakini pia cha ziada kwa wananchi wa Nyamongo hasa maeneo ya Tarime, Mheshimiwa Mbunge anafahamu vizuri kwamba kampuni ya Barrick mwaka jana mwezi wa saba na nane imezindua mradi maalum wa kuwasaidia wachimbaji wadogo katika maeneo yale ya Nyabigena. Mheshimiwa Mbunge anafahamu kuna vikundi zaidi ya 20 ambavyo tayari vishasajiliwa na ule mradi unagharimu takribani bilioni tatu. Wanufaika wakubwa ni wananchi wa Nyabigena wanaozunguka maeneo yale.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba tuendelee kutoa taarifa za kuwatia matumaini wananchi badala ya kuwakatisha tamaa kwa sababu sote tunawatumikia Watanzania. *(Makofi)*

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Kuhusu utaratibu.

SPIKA: Kuhusu utaratibu Mheshimiwa Shellukindo, Kanuni.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu, Kanuni ya tatu, katika kipindi hiki cha Maswali na Majibu nimeshuhudia maneno haya yakitamkwa; baba yangu, mama yangu, kaka yangu, dada yangu, ndugu yangu; lakini nimetazama kwenye Kanuni ya Tatu sikuyaona hapa. Ni tofauti na kutangaza wageni, sizungumzii wageni; kuna ndugu zetu kule, ni hili la humu ndani. Naomba mwongozo wako.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mwongozo wangu ni kama ifuatavyo: Hakuna athari yoyote kwa watu ambao wanatambulisha mahusiano yao humu Bungeni kama mtu anajua ni kaka yake ni suala la heshima tu. Kwa hiyo tusipate taabu sana hakuna tusi hapo, hakuna tatizo. Mtu akisema mzee wangu au kaka yangu, mama yangu kwanza mama ni suala la heshima tu. Kwa hiyo Mheshimiwa Shellukindo najua wewe ni mtaalam wa mambo ya itifaki ndani ya Bunge lakini Bunge linazidi kukua na utamaduni wake lazima upanuke na utanuke kwa hiyo haya yote ambayo yanatamkwa kwa heshima yanaruhusiwa.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujamaliza kipindi cha maswali Mheshimiwa Josephine Genzabuke aliniandikia swali lake la nyongeza, alivyoliuliza linaweza likaleta hisia mbaya sana kule Kigoma. Kwa hiyo, nampa nafasi asahihishe kwa muda mfupi sana. Mheshimiwa Josephine.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Wakati nauliza swali nilisahau nikasema mipaka iongezwe badala ya mipaka ipunguzwe. Naomba wananchi waelewe kwamba niliomba mipaka ipunguzwe.

Naomba na *Hansard* warekebishe, mipaka iwekwe ili waendelee kupata mashamba ya kulima.

SPIKA: Ahsante, nashukuru. Waheshimiwa sasa ni matangazo naanza na wageni. Wageni wa Mheshimiwa Abdulkarim Shah ni wawili, Ndugu Nuru Yakub - Mkurugenzi Mkuu wa *SoftNet* na Bi. Amne Bafadhil mkewe wa huyo Mkurugenzi wale pale karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wapo wageni, kikundi cha *TAWE* kinamama wajasirimali nadhani ni wa Dodoma, lakini wana mgeni wao na wao. Bi Anna Kosak kutoka Chicago Marekani, *welcome to Dodoma specifically to Bunge, you have come a long way, we are happy to have you with us here in Dodoma.* Wengine ni Ndugu Atupakisye Mtafya, yule pale; Ndugu Salome Kiwaya, mama huyu ni hodari ana bendi yake ya burudani na mnajua vitu alivyovitoa jumamosi na Ndugu Happy Mtoa, wale pale. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Morogoro, wana wageni wao, orodha ni ndefu, kwa hiyo, sitaisoma nitasoma tu viongozi na baada ya hapo wote wasimame. Hawa ni wawakilishi kutoka Mkoa wa Morogoro wanaongozwa na ndugu Masasila Kabisa - Mwenyekiti na Cosmas Majaliwa, basi na wengine wote naomba wasimame. Karibuni sana kutoka Mkoa wa Morogoro, tunafurahi kuwaona hapa, ni haki yenu kuja kushuhudia shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Vita Kawawa ameniomba nimtambulishe mdogo wake ambaye ni Mwakilishi wa Kampuni ya Mazingira inayoitwa inayoitwa *Pollution to Water* Twaha Alli Kawawa, yule pale. Karibu sana.

Matangazo ya kazi, Mheshimiwa William Shellukindo anahitaji Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini mkutane leo saa saba mchana Ukumbi Na. 219. Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o - Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, anaomba Wajumbe wote wa Kamati hiyo wakutane saa 5.00 asubuhi leo katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib - Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba kutakuwa na Kikao saa 5.00 asubuhi hii Ukumbi Na. 227. Mheshimiwa Mohamed Misanga - Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu naye anaitisha Kikao cha Kamati saa tano asubuhi Ukumbi wa zamani wa *Speaker's Lounge* saa 5.00 asubuhi hii. Mheshimiwa Balozi Paul Kimiti - Patron wa Mabalozi wa zamani anaomba Wabunge wote ambao ni Mabalozi wa Amani Duniani na wale wanaopenda kujiunga na taasisi hii wakutane mara baada ya Kikao kuahirishwa kwa maana hiyo mchana na Mkutano huo utafanyika kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge siku ya Alhamis iliyopita Mheshimiwa Naibu Spika, alitoa ufafanuzi kuhusu maswali kwa Waziri na utaratibu wake. Napenda kuthibitisha hapa kwamba utaratibu huo ndiyo tulikubaliana. Naibu Spika, ama Mwenyekiti yoyote anaposema hapa, muelewe anayo ridhaa ya Spika. Kama kuna mabadiliko ya utaratibu,

isionekane kwamba mambo haya kwa viwango na mipango, hatuendi hovyo hovyo, kila mtu anatamka lake. Kwa hiyo, nilikuwa pale kwenye kiti changu cha Urambo Mashariki nikaona watu wanalalamika. Tatizo lililotupa katika kuwapatia nafasi Waheshimiwa Wabunge tulipokuwa tunasema anayewahi, yalikuwa yanatokea mambo ya hatari kidogo. Sasa saa 10.30, saa 10.45 alfajiri na saa hizo ilitokea vitu ambavyo sio vizuri kwa sababu hata Afisa anayepokea maswali anakuwa hayupo. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wanajikuta wanamsubiri Afisa wa Bunge. Kwa hiyo, sisi tulikutana tukaona ushauri mzuri, tufanye ni saa 1.30, ni muda wa kistaarabu. Kwa hiyo, Naibu Spika alipotamka sio kwamba ulikuwa ni uamuzi wake yeye, ni uamuzi wa Spika baada ya mashauriano.

Kesho asubuhi baada ya saa kama hizi za matangazo nitakuwa na ufafanuzi wa kikatiba kuhusu malalamiko ya Jaji Mkuu juu ya mambo fulani fulani aliyoona yeye yana matatizo. Ni suala la Kikatiba, hatuwezi kama taasisi tukakaa kimya. Lakini niseme tu kuhusu maamuzi mbalimbali ya Mahakama zetu. Kupitia ningependa nafasi hii kuwaomba mfumo mzima wa Mahakama wajue kwamba wanaishi miongoni mwa jamii, maamuzi mengine ambayo yanatoa fursa kwa mtu mmoja badala ya kuzingatia haki za jamii yanawakera wananchi wengi sana na kuleta usumbufu mkubwa sana.

Nilipolalamika kuhusu kitendo cha Hakimu mmoja kuizuia *EWURA. EWURA* ilipofanya ukaguzi wa vituo vya mafuta ikagundua vituo kadhaa ambavyo vinachanganya mafuta kwa mfano *diesel,* vinachanganya mafuta kwa mfano *diesel* inawekewa mafuta ya taa, sehemu nyingine *petrol* inawekwa maji kidogo. *EWURA* kwa Kanuni zake zinazotokana na Sheria tuliyoitunga hapa ikavifungia vituo hivyo. Matajiri wakaenda Mahakamani, vituo hivyo vikafunguliwa kwa amri ya Mahakama, lakini matokeo ya hayo ni kwamba nchi inasema ni ruksa kuuza mafuta machafu ili mtu ajipatie faida. Sasa sisi wengine inapokuja mgongano baina ya maslahi ya wengi na ya wachache daima mtanikuta nasimamia ya wengi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hatuna nia mbaya lakini Mahakama wazingatie kwamba jamii inawaangalia wale wanaotoa maamuzi kidogo hata mtu wa kawaida tu anashangaa. Sasa Mahakama isije ikalalamika kwamba inaingiliwa uhuru wake wakati maamuzi mengine hayaingii akilini yanakua ni ya ajabu ajabu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, na hapa pia watasema naingilia Mahakama! Potelea mbali! *(Makofi)*

Wajeshimiwa Wabunge, mpangilio wa *Order Paper* nawaomba kwa mujibu wa Kanuni ya 30 fasili ndogo ya nne. Tunaweza kufuata mpangilio kwa kuubadilisha kidogo kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge. Nimepewa taarifa kwa upande wa Serikali kwamba Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi anahitajika kwenda Dar es Salaam saa 6.00 kwa shughuli maalum ambayo ameitwa kule Ikulu. Kwa hiyo, ni dhahiri imebidi nishauriane na Katibu. Kwa hiyo, mpangilio wa shughuli wa leo utakuwa kama ufuatavyo:-

Nitamruhusu Waziri wa Fedha atangulie awasilishe mapendekezo Mpango wa Taifa kwa mwaka wa fedha, baada ya hapo badala ya kuwasilikiza Mwenyekiti na Kambi

ya Upinzani nitamwita Waziri wa Maji kwa sababu kauli yake haina mjadala ni kauli tu ya Waziri na baada ya hapo tutaendelea na utaratibu wa kawaida. Kwa hiyo, nayahamisha maazimio ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama yawe ni kesho asubuhi. Kwa mpangilio huo, basi namwita Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi aweze kuwasilisha Mpango wa Taifa wa Uchumi kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

HOJA ZA SERIKALI

Mapendekezo ya Mpango wa Taifa kwa Mwaka waFedha 2009/2010

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Mipango kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maelezo kuhusu Mwongozo wa kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha muda wa kati (2009/2010 – 2011/2012).

Aidha, napenda kuishukuru Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, kwa kupitia muhtasari wa mwongozo na kutoa maoni na mapendekezo ambayo yameboresha muhtasari huu. Nawasilisha muhtasari wa Mwongozo katika Kamati yako ili uweze kujadiliwa kwa kina na kutoa maoni ambayo yataboresha Mwongozo utakaotumiwa na Wizara, Idara, Mikoa na Serikali za Mitaa katika kuandaa Mipango na Bajeti zao kwa mwaka wa fedha ujao na kipindi cha muda wa kati. Mpango na Bajeti utawasilishwa Bungeni mwezi Juni, 2009 baada ya kupitiwa na Kamati mbalimbali za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Mwongozo umetayarishwa kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025; Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Mchakato wa maandalizi ya mwongozo umewashirikisha wadau muhimu katika kuainisha maeneo ya vipaumbele na umejumuisha mwongozo uliokuwa ukitolewa kwa Serikali za Mitaa. Hali ya mwenendo wa uchumi duniani ambao umekumbwa na misukosuko hasa katika sekta ya fedha nayo pia imezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Mwenendo wa Uchumi na Bajeti ya mwaka 2008/2009, imelenga kutekeleza sera za uchumi jumla ikiwa ni pamoja na kukuza pato la Taifa kwa asilimia 7.8 (2008) na asilimia 8.1 (2009), kukusanya mapato ya ndani sawa na asilimia 18.5 ya pato la Taifa na kuhakikisha kasi ya upandaji wa bei haizidi asilimia 7.5 ifikapo Juni, 2009. Aidha, malengo ya akiba ya fedha za kigeni ni kuwa na akiba isiyopungua uwezo wa uagizaji wa bidhaa na huduma wa miezi mitano.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya utekelezaji wa sera za uchumi jumla katika kipindi cha nusu mwaka inaonesha uchumi wetu unatarajiwa kukua kwa asilimia 7.5 katika mwaka 2008 ikiwa ni chini ya lengo kwa asilimia 0.3.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mfumuko wa bei, hali sio ya kuridhisha. Tumeshuhudia ongezeko kutoka asilimia 9.3 mwezi Juni, 2008 hadi kufikia asilimia 13.5 mwezi Desemba, 2008. Sababu kubwa zilizochochea hali hii ni pamoja na kupanda kwa bei za vyakula kulikosababishwa na kupanda kwa gharama za usafirishaji zinazotokana na bei kubwa ya mafuta ya petroli. Aidha, ukosefu wa mvua za kutosha za vuli umesababisha uhaba wa chakula katika maeneo kadhaa nchini. Kutokana na hali hii, malengo ya kudhibiti mfumuko wa bei hadi kiwango cha asilimia 7.5 ifikapo Juni, 2009 yaelekea hayataweza kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka unaoishia Desemba, 2008, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) ulikua kwa asilimia 28.4 ikilinganishwa na lengo la asilimia 18.2. Kuongezeka kwa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana kumetokana na kukua kwa kiwango cha mikopo inayotolewa kwa sekta binafsi.

Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)1 ulikwenda sambamba na mwenendo wa sera za fedha zilizotekelezwa na Benki Kuu katika kipindi hicho. M3 ilikua kwa asilimia 24.0 mwezi Desemba, 2008 ikilinganishwa na lengo la asilimia 17.7. Pale chini tumetafsiri M1, M2 na M3 ni kitu gani.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2008/2009, kiwango cha mikopo kwenda sekta binafsi kimezidi wastani wa mwezi wa shilingi bilioni 86.1 kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita. Katika mwaka ulioishia Desemba, 2008, mikopo iliyotolewa kwenda sekta binafsi ilikua kwa asilimia 47.0 sawa na shilingi bilioni 4,376.4 ikilinganishwa na shilingi bilioni 2,093.6 zilizotolewa Desemba, 2007. Ukuaji huu wa mikopo unatokana na uamuzi wa Serikali kutokopa kutoka vyombo vya fedha vya ndani, kuongezeka kwa uaminifu kwa wakopaji, kuongezeka kwa dhamana ya mikopo (credit *guarantee schemes*) na kuongezeka kwa mikopo kwa makampuni.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa riba katika mwaka unaoishia Desemba 2008, unaonyesha kuwa riba za amana zimeongezeka hadi asilimia 2.68 kutoka asilimia 2.26 mwezi Julai, 2008, wakati ambapo kiwango cha riba za muda maalum kimepungua kutoka asilimia 6.58 Julai, 2008 hadi asilimia 6.39 Desemba, 2008. Riba za mikopo katika mabenki ya biashara zimeendelea kuwa za juu na kufikia asilimia 16.05 mwezi Desemba, 2008 kutoka asilimia 15.05 mwezi Julai, 2008.

Mheshimiwa Spika, thamani ya Shilingi ya Tanzania kwa Dola ya Kimarekani ilikuwa ni wastani wa shilingi 1,280.30 mwishoni mwa Desemba, 2008 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 1,132.09 mwishoni mwa mwezi Desemba, 2007. Hali hii inatokana na mahitaji makubwa ya Dola za Kimarekani kwa makampuni yanayoingiza bidhaa nchini pamoja na baadhi ya makampuni kutaka kuhodhi fedha za kigeni kutokana na ubahatishaji wa kupata faida zaidi *(speculation).*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kinachoishia Desemba, 2008 kulikuwa na nakisi ya dola za Kimarekani milioni 2,818.2 ikilinganishwa na milioni 2,100.6 mwaka 2007 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 34.2. Kukua kwa nakisi kumetokana na uuzaji nje kuwa mdogo ikilinganishwa na uagizaji nje.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka unaoishia Desemba, 2008 mauzo ya bidhaa nje yalifikia dola za Kimarekani milioni 2,608.5 ikilinganishwa na dola za Kimarekani milioni 2,024.2 Desemba, 2007. Mapato haya yalichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa asilia na zisizo asilia. Biashara za mazao asilia na yasiyo asilia ziliongezeka hadi dola za Kimarekani milioni 414.0 na milioni 2,194.5 kutoka dola milioni 319.7 na milioni 1,704.5 mwezi Desemba, 2007 kwa mtiririko huo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kinachoishia Desemba, 2008, uagizaji bidhaa kutoka nje uliongezeka kwa asilimia 31.7 kufikia dola za Kimarekani 6,327.9 milioni (fob) kutoka dola milioni 4,806.0 mwezi Desemba, 2007. Ongezeko hili lilitokana na uagizaji wa bidhaa za kati hasa mitambo ya usafirishaji, vifaa vya ujenzi, mashine mbalimbali na mafuta.

Mheshimiwa Spika, hadi Desemba, 2008 akiba ya fedha za kigeni ilifikia Dola za Kimarekani 2.89 bilioni sawa na uwezo wa uagizaji wa bidhaa na huduma kwa miezi 4.3 ikilinganishwa na dola za Kimarekani bilioni 2.76 mwezi Desemba, 2007 sawa na uwezo wa uagizaji wa bidhaa na huduma kwa miezi 4.9.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa mapato ya ndani kwa kipindi cha Julai – Desemba, 2008 unaonesha kwamba jumla ya Sh. 2,162,202/= zilikusanywa, sawa na asilimia 93 ya lengo la kukusanya Sh. 2,334,966, sawa na upungufu wa shilingi milioni 172,764. Upungufu huu umetokana na baadhi ya vyanzo vya kodi kutofanya vizuri.

Maeneo ambayo hayakufanya vizuri ni pamoja na Ushuru wa Forodha, Kodi ya Mapato kwa Makampuni, Ushuru wa Bidhaa za ndani na kutoka nje, pamoja na mapato yasiyo ya kodi. Maeneo ambayo yamefanya vizuri ni Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa mauzo ya ndani na nje. Serikali imeandaa mipango maalumu ya kuongeza makusanyo ya kodi na yasiyo ya kodi. Kwa upande wa mapato yatokanayo na ubinafsishaji, jumla ya shilingi bilioni 45 zilipatikana, sawa na makadirio katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, matumizi halisi katika kipindi cha Julai - Desemba 2008 yalikuwa Sh. 3,475,920/= sawa na asilimia 101.8 ya makadirio ya Sh. 3,415,587/= katika kipindi hicho. Kati ya fedha hizo, Sh. 2,313,490/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Malipo ya mishahara ya watumishi wa Serikali kwa kipindi cha Julai – Desemba yalikuwa Sh. 872,322,000,000/= sawa na asilimia 102 ya makadirio ya Sh. 855,269,000,000 kwa kipindi hicho. Kiasi hiki kimejumuisha malipo ya marekebisho ya ongezeko la mishahara ya watumishi wa Serikali pamoja na malimbikizo ya mishahara ya miezi sita kutoka Januari hadi Juni, 2008.

Mheshimiwa Spika, malipo ya riba kwa madeni ya ndani katika kipindi cha Julai - Desemba, 2008 yalifikia Sh. 81,006,000,000/= sawa na asilimia 83 ya lengo la kulipa Sh. 97,613,000,000/= katika kipindi hicho. Kwa upande wa madeni ya nje, jumla ya Sh. 15,169,000,000/= zilitumika kulipia riba sawa na asilimia 104 ya makadirio. Kwa ujumla matumizi ya madeni mengine *(Consolidated and Services)* yalikuwa ni Sh. 161,295,000,000/= sawa na asilimia 94 ya makadirio.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya Utafiti wa Matumizi ya Kaya *(Household Budget Survey, 2007)* yanaonyesha kuwa kiwango cha umaskini kimepungua kwa kiwango kidogo. Tathimini inaonyesha kuwa kwa ujumla tumepunguza kidogo sana hali ya umasikini wa kipato nchini kutoka asilimia 35.7 (2000/2001) hadi asilimia 33.3 (2007). Kutokana na utafiti huu, kumekuwepo na mafanikio hasa katika elimu na matumizi ya vyombo vya afya vya umma. Aidha, mafanikio katika maeneo haya hayawezi kuonyesha kupunguza umasikini wa kipato katika kipindi cha muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utekelezaji MKUKUTA, kumekuwepo na mafanikio karibu katika kila sekta. Mafanikio hayo yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji mzuri wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi 2005. Mafanikio hayo ni pamoja na ujenzi wa barabara, utekelezaji wa programu za elimu ya msingi, sekondari na elimu ya juu,; utekelezaji wa programu za kilimo, uzalishaji wa maziwa na nyama, uwezeshaji wananchi kiuchumi, huduma za mawasiliano na huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika maeneo hayo, changamoto zilizopo ni pamoja na kuhakikisha kwamba matokeo ya ukuaji wa uchumi jumla yanawanufaisha wananchi katika ngazi ya kaya; kuendelea kuimarisha miundombinu muhimu katika sehemu za uzalishaji, kuwawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji, kuendelea kuboresha huduma za jamii na kuendelea kudumisha misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Spika, msukosuko katika uchumi wa dunia na madhara kwenye uchumi wa Tanzania, wakati nilipowasilisha maelezo kuhusu hali ya msukosuko wa fedha na uchumi duniani na Gavana wa Benki Kuu kufafanua zaidi kuhusu hali ya mfungamano wa masoko ya fedha ya ndani na yale ya kimataifa, nilieleza kuwa, madhara kwenye uchumi wa Tanzania, ambayo yameanza kujitokeza ni pamoja na haya yafuatayo:-

(i) Kupungua kwa kiasi *(volume)* na bei ya bidhaa muhimu, mfano pamba, kahawa, karafuu, korosho na baadhi ya bidhaa zisizo asilia (mfano, maua na madini ya *tanzanite*) ambazo Tanzania inauza kwenye nchi zilizoathirika na msukosuko huo, hasa Marekani na Ulaya;

(ii) Kupungua kwa idadi na matumizi ya watalii wanaokuja Tanzania;

(iii) Kupungua kwa ajira kwenye makampuni;

(iv) Upatikanaji na kupanda kwa bei za chakula;

(v) Kupungua kwa kiwango cha fedha (*remittances*) ambazo Watanzania wanaoishi katika nchi zilizoathirika zaidi hutuma kwa ndugu na jamaa zao hapa Tanzania;

(vi) Kupungua kwa misaada tunayopata kutoka kwa wahisani; na

(vii) Kupungua kwa uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje *(Foreign Direct Investment).*

Mheshimiwa Spika, Serikali inajiandaa ipasavyo kukabiliana na hali hii, hatua zitakazochukuliwa ni pamoja na kuwa na mpango wa dharura na wa muda wa kati wa kujihami na matatizo hayo. Aidha, Kamati Maalum imeundwa kuchambua kwa kina athari za msukosuko kwa uchumi wa Tanzania na kupendekeza mikakati ya kukabiliana nazo.

Mheshimiwa Spika, mpango wa dharura ni:-

(i) Kuhakikisha kuwa tuna chakula cha kutosha katika kipindi cha miezi 12 ijayo, hivyo sekta zinazohusika zitalazimika kuweka mkakati maalum wa kufanikisha hilo. Hii ni pamoja na kuishirikisha Mikoa sita ya Morogoro, Iringa, Ruvuma, Mbeya, Rukwa na Kigoma ambayo ina uwezo wa kuzalisha chakula kwa wingi.

Vile vile, Serikali imejiandaa kuchukua hatua ili kukabiliana na upungufu wa chakula katika maeneo mbalimbali kwa kupeleka chakula maeneo yenye uhaba kutoka kwenye maeneo yenye ziada. Serikali tayari imetoa fedha kwa ajili ya kusafirisha chakula hicho.

(ii) Wizara ya Fedha na Uchumi pamoja na Benki Kuu kuendelea kusimamia sekta ya fedha ipasavyo ili kujihami na madhara yanayoweza kujitokeza. Aidha, mabenki yatahamasishwa ili yaendelee kukopesha sekta za uzalishaji.

(iii) Mikopo iliyotolewa na mabenki kama *CRDB, NMB* na *EXIM* kwa wanunuzi wa mazao ya biashara huenda isilipwe kwa wakati kama ilivyotarajiwa kutokana na kupungua kwa kiasi cha mazao kinachouzwa nje na kushuka kwa bei. Hali hii imesababisha mlundikano wa baadhi ya mazao kama vile pamba. Inabidi hatua zichukuliwe ili kukabiliana na hali hiyo.

(iv) Kuimarisha juhudi za kukusanya mapato ya ndani na kupunguza utegemezi wa misada kutoka nje. Hii itahusisha kuangalia upya misamaha ya kodi;

(v) Kanuni za *leasing and mortgage*– Kukamilisha kanuni za *lease financing and mortgage financing* ili huduma hizi ziweze kupatikana kwa wananchi kwa kukopa zana na vifaa vya ujenzi waweze kujiendeleza kiuchumi;

(vi) Kuahirisha mpango wa Serikali kukopa kwenye masoko ya mitaji ya kimataifa kwa kutumia *Sovereign Bonds* na badala yake kutumia hatifungani za ndani; na

(vii) Kuendelea kubana matumizi ya kawaida ili kutoathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Muda wa Kati ni:-

(i) Kujenga na kuboresha miundombinu ikiwemo barabara, reli, bandari, umeme na maji;

(ii) Kutafuta vyanzo vingine vya kugharamia miradi ya miundombinu, kilimo, viwanda na kadhalika. Vyanzo hivyo ni pamoja na mikopo ya ndani, misaada na mikopo kutoka katika nchi na taasisi za nchi za Mashariki ya Kati, China, India, Korea Kusini na Japan;

(iii) Kuongeza juhudi za kutangaza vivutio vyetu vya utalii pamoja na kuhamasisha utalii wa ndani;

(iv) Mazao ya biashara – Mkakati utaandaliwa kurekebisha hali ya ukosefu wa soko la mazao ya biashara. Hii itajumuisha kutafuta masoko mengine ya Asia na kwingineko. Aidha, juhudi mahsusi zitafanyika katika kuwezesha viwanda vya ndani kutumika katika kuongeza thamani ya mazao hayo kama vile viwanda vya kusindika korosho, matunda na mboga mboga na viwanda vya kufuma nyuzi na kutengeneza nguo na viwanda vya ngozi; na

(v) Kuendelea na mikakati ya kuongeza tija *(productivity)* kwenye sekta muhimu za uchumi kwa mfano kuimarisha mtaji wa Benki ya Rasilimali (TIB), kufungua dirisha la mikopo ya kilimo katika Benki ya Rasilimali na hatimaye kuanzisha Benki ya Kilimo, kuhamasisha kilimo cha kisasa kama vile kilimo cha umwagiliaji na kutumia zana bora, kuhamasisha na kuboresha shughuli za uvuvi.

Mheshimiwa Spika, malengo ya uchumi - jumla kwa kipindi cha mwaka 2009/2010 - 2011/2012 ni kama ifuatavyo:-

(i) Kasi ya ukuaji wa pato halisi la Taifa itapungua kutoka asilimia 7.5 mwaka 2008, hadi asilimia 7.0 mwaka 2009. Kasi hiyo inatarajiwa kuongezeka kufikia asilimia 7.1 mwaka 2010, asilimia 7.3 mwaka 2011 na asilimia 7.5 mwaka 2012;

(ii) Kuwa na kiwango cha kasi ya upandaji bei kisichozidi asilimia 7.5 ifikapo mwezi Juni, 2010;

(iii) Kuwa na mapato ya ndani kutoka lengo lililorekebishwa la asilimia 17.7 la pato la Taifa mwaka 2008/2009, hadi asilimia 17.0 mwaka 2009/2010, asilimia 17.2 mwaka 2010/2011 na kuongezeka zaidi kufikia asilimia 17.5 mwaka 2011/2012;

(iv) Kudhibiti ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) kwa viwango vinavyowiana na malengo ya ukuaji wa uchumi na kupunguza kasi ya upandaji bei; na

(v) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi mitano.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa bajeti ya serikali mwaka 2009/2010 – 2011/2012: Misingi ya Mpango na Bajeti ya Serikali Kwa Kipindi cha 2009/2010 - 2011/2012 itakuwa kama ifuatavyo:

(i) Kuendelea kuimarisha utengamavu wa viashiria vya uchumi jumla ikiwamo ukuaji wa uchumi;

(ii) Kuongeza rasilimali katika utekelezaji wa MKUKUTA kwa kutenga rasilimali za kutosha katika maeneo machache yenye kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi;

(iii) Kuongeza kiwango cha ukuaji wa sekta ya kilimo (mazao, mifugo, uwindaji na misitu) kwa kuweka mikakati mahususi ya kuimarisha barabara hasa zile za vijijini na kuwezesha upatikanaji wa mikopo na zana za kilimo;

(iv) Kuendelea na utekelezaji wa maboresho ya kiuchumi na kijamii;

(v) Kuendelea kuboresha mfumo wa makusanyo ya mapato ya ndani;

(vi) Kuendelea kuboresha mazingira ya kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje;

(vii) Kuendelea kuoanisha sera ya fedha *(monetary policy)* ili iwiane na sera ya mapato na matumizi *(fiscal policy)* zitakazosaidia kupunguza mfumuko wa bei na riba na kuongeza mikopo kwa sekta binafsi;

(viii) Kuendelea kuzijengea uwezo Serikali za Mitaa ili ziweze kutekeleza kwa ufanisi maamuzi ya kupeleka madaraka kwa wananchi;

(ix) Kuendelea kuwawezesha wananchi kiuchumi;

(x) Kuendelea kuimarisha mifuko ya pensheni na kuongeza kima cha chini cha pensheni;

(xi) Kuendelea kuimarisha mfumo wa usimamizi na ufuatiliaji pamoja na tathmini; na

(xii) Kuendelea na mikakati ya kupunguza utegemezi wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya kipaumbele katika mpango na bajeti yataendelea kutekelezwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005, Malengo ya Milenia na MKUKUTA. Maeneo ya vipaumbele ni yafuatayo:-

(i) Kuchukua hatua mahsusi za kujihami na matokeo ya msukosuko wa kifedha na uchumi duniani katika uchumi wa Tanzania kama ilivyobainishwa katika mpango wa dharura katika aya ya 21;

(ii) Miundombinu:

(a) Kuelekeza rasilimali zaidi katika miundombinu ya usafirishaji na mawasiliano ili kuifanya Tanzania kuwa kituo na sehemu muhimu ya biashara ya usafirishaji na mawasiliano kikanda na kimataifa, kwa kuendeleza na kuboresha bandari za Dar es Salaam, Mtwara na Kigoma, reli ya kati, barabara na viwanja vya ndege;

(b) Kuimarisha miundombinu ya nishati ya umeme katika Mikoa na Wilaya zilizobaki kwa kuunganishwa katika gridi ya Taifa, kuimarisha na kupanua miundombinu ya matumizi ya gesi ya *Mnazi Bay*, Songo Songo, Mkuranga na kadhalika katika kuzalisha umeme na matumizi ya magari na majumbani, kuongeza juhudi katika utafiti wa mafuta, kuanzisha hifadhi ya mafuta (ghala la *TIPPER)*, kuliwezesha Shirika la Mafuta *(TPDC)* kushiriki katika biashara ya mafuta kwa kusambaza na kuwezesha ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza, na kukifufua kiwanda cha usafishaji wa mafuta ghafi;

(c) Kujenga Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano *(TEKINOHAMA)* kwa ajili ya kuongeza kasi na upatikanaji wa mawasiliano ya ndani na kimataifa; na

(d) Kuongeza kasi ya kupima ardhi ili kusaidia utambuzi na matumizi yake;

(iii) Uzalishaji:

(a) Kuimarisha na kupanua miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji, kuwekeza katika miradi mikubwa ya kilimo, kuendelea kutoa ruzuku ya pembejeo na kuanzisha benki ya kilimo, kuimarisha mashamba ya mbegu bora, kudhibiti milipuko ya magonjwa, kufanya utafiti na kutoa huduma za ushauri wa masuala ya kilimo, kuboresha kilimo kwa kutumia zana za kisasa ikiwa ni pamoja na matrekta makubwa na madogo, majembe ya kukokotwa na wanyama kazi na kuwezesha viwanda vidogo vidogo kutengeneza bidhaa.

(b) Kuboresha utoaji wa ruzuku ya madawa ya mifugo na chanjo, miundombinu ya mifugo hususan majosho, malambo na masoko, kuboresha vituo vya huduma ya madume bora, kupima maeneo ya wafugaji na kuajiri wataalam wa ugani.

(c) Kuboresha uvuvi kwa kuhimiza matumizi ya zana bora na za kisasa, kudhibiti uvuvi haramu na kuhamasisha ufugaji wa samaki *(aquaculture)*.

(d) Kuwezesha viwanda vidogo na vya kati *(SMEs)*, kuongeza uzalishaji, kuongeza thamani ya bidhaa, kuimarisha uwezo wa wafanyakazi na matumizi ya teknolojia rahisi.

(e) Kuendeleza ujuzi na utaalam katika nguvukazi ili iweze kusaidia na kukidhi mahitaji ya kuleta mapinduzi ya viwanda nchini na ushindani wa kimataifa.

(f) Kuelekeza nguvu katika kuongeza thamani ya madini kwa kusafisha dhahabu hapa nchini na vito vinginevyo.

(iv) Huduma za jamii:

(a) Kuongeza upatikanaji wa maji safi, salama na ya kutosha katika umbali mfupi vijijini na mijini;

(b) Kuendeleza utekelezaji wa miradi inayoendelea;

(c) Kuendeleza utekelezaji wa miradi inayoendelea;

(d) Kuendeleza juhudi za kuongeza ajira nchini; na

(e) Kuharakisha mchakato wa kuandaa Vitambulisho vya Taifa.

(v) Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kushirikisha sekta binafsi katika uwekezaji na utoaji wa huduma mbalimbali nchini *(Public Private Partnership - PPP).*

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Bajeti unaonesha matarajio ya awali ni kukusanya asilimia 17.0 ya pato la Taifa mwaka 2009/2010 ikilinganishwa na makisio ya asilimia 17.7 (kwa takwimu zilizorekebishwa) mwaka 2008/2009. Misaada na mikopo ya bajeti inatarajiwa kuwa asilimia 2.9 mwaka 2009/2010 ikilinganishwa na asilimia 3.0 mwaka 2008/2009; misaada na mikopo ya miradi inatarajiwa kuwa asilimia 3.5 mwaka 2009/2010 ikilinganishwa na asilimia 4.0 mwaka 2008/2009; michango ya pamoja ya wafadhili *(basket fund)* inatarajiwa kuwa asilimia 1.6 sawa na ilivyokuwa mwaka 2008/2009.

Hata hivyo, michango hii huenda ikapungua kutokana na wasiwasi wa hali ya kuyumba kwa uchumi katika nchi za Ulaya na Marekani. Serikali itaendelea kutafuta mikopo ya nje na ndani pamoja na misaada kutoka nchi marafiki kama China, India na nchi za Kiarabu kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Aidha, Serikali itaendelea na azma yake ya kutokukopa kwa ajili ya kugharamia bajeti ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, mgao wa fedha unaopendekezwa kwa mwaka 2009/2010 ni kama ifuatavyo:-

(i) Kiasi cha asilimia 7.1 ya Pato la Taifa kimetengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo;

(ii) Asilimia 5.6 ya Pato la Taifa imetengwa kwa ajili ya kulipia mishahara;

(iii) Mfuko Mkuu wa Serikali umetengewa asilimia 2.3; na

(iv) Serikali imetenga asilimia 9.1 kwa ajili ya bajeti ya maendeleo. Kiwango hiki kinatarajiwa kuongezeka iwapo Serikali itafanikiwa kupata mikopo na misaada kutoka nchi marafiki kama ilivyoelezwa katika aya ya 25.

Mheshimiwa Spika, Maeneo matatu ya MKUKUTA ambayo ni Ukuaji wa Uchumi na Kupunguza umaskini wa Kipato, Uimarishaji wa Huduma za Jamii na Utawala Bora na Uwajibikaji yametengewa asilimia 73.5 ya matumizi yote ukiondoa matumizi ya mishahara na matumizi maalum.

Kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi yasiyo ya MKUKUTA asilimia 55 ni kwa ajili ya Mfuko Mkuu wa Serikali ambao unajumuisha ulipaji wa pensheni ikijumuisha ongezeko la kima cha chini cha pensheni, madeni, riba na malipo mengine ya kimkataba.

Mheshimiwa Spika, mwongozo wa utayarishaji wa Mpango na Bajeti wa mwaka 2009/2010 - 2011/2012 unaelekeza upangaji wa mipango uzingatie rasilimali chache tulizonazo na kuzielekeza katika vipaumbele vichache vitakavyoleta msukumo wa haraka katika ukuaji wa uchumi. Watekelezaji wameagizwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuhakikisha mpango wa dharura unatekelezwa ipasavyo;

(ii) Kuzingatia vipaumbele vya mpango na bajeti kama vilivyoainishwa katika mwongozo;

(iii) Wizara, Mikoa na Serikali za Mitaa kuendelea kudhibiti kwa dhati matumizi ya fedha zilizoidhinishiwa, ili kuweza kutoa huduma na uendeshaji wa shughuli za Serikali kwa ufanisi;

(iv) Viongozi katika ngazi zote waongeze jitihada za kuhamasisha na kuratibu ukusanyaji wa mapato ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa katika maeneo yao;

(v) Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, ziendelee kubaini na kuendeleza fursa za maendeleo zinazovutia uwekezaji wa sekta binafsi pamoja na kuwahamasisha wananchi wawekeze kwa lengo la kuchochea maendeleo.

Aidha, vyombo vinavyohusika katika mchakato wa uwekezaji viondokane na urasimu usio wa lazima kwa kutekeleza kikamilifu programu ya MKUMBITA;

(vi) Kudhibiti matumizi yasiyo na tija na kutoa kipaumbele katika kulipa madeni na kutolimbikiza madeni;

(vii) Kusitisha ununuzi wa magari na samani zisizo za lazima na ubora unaostahili katika bajeti ya mwaka 2009/2010;

(viii) Kusitisha Semina na Makongamano yote isipokuwa kwa kibali maalum kutoka kwa Waziri Mkuu;

(ix) Wizara kuhakikisha mashirika na taasisi za umma zilizo chini yao zinazokusanya maduhuli na kuchangia ipasavyo katika Mfuko Mkuu wa Serikali;

(x) Kurejesha utaratibu wa kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa sheria;

(xi) Wizara, Idara, Mikoa na Serikali za Mitaa wajiwekee malengo yanayopimika na kuandaa viashiria vya utendaji kazi *(Performance Indicators);* na

(xii) Kuendelea kuimarisha taratibu za kufuatilia utekelezaji wa mpango na bajeti *(Monitoring of Plan and Budget Execution).*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bunge na Kamati zake ni vyombo muhimu vya kuhakikisha kwamba mpango na bajeti inatekeleza sera za kitaifa, Serikali iko tayari kupokea maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge ili kuboresha mwongozo. Aidha, napenda kusisitiza kuwa huu ni muhtasari wa mwongozo, mpango na bajeti kamili vitakuwa tayari baada ya taasisi husika kuandaa mipango na bajeti zao kwa kuzingatia mwongozo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Muhtasari wa Mwongozo wa utayarishaji Mpango na Bajeti ya 2009/2010 – 2011/2012 kwa matumaini kwamba Waheshimiwa Wabunge wataushabikia kuujadili na kutupa mawazo mengi zaidi ili mpango wa mwaka huu uwe bora kuliko mipango yote ya miaka iliyopita.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha! *(Makofi)*

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naafiki!

SPIKA: Asante sana Mheshimiwa Waziri. Amekwishatoa hoja na imeungwa mkono. Lakini kama nilivyoeleza, ili twende vizuri na baada ya hapo sasa twende sasa moja kwa moja, tupate kauli ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2007, Kanuni Na. 49, naomba kutoa Kauli ya Serikali kuhusu Utekelezaji wa Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tarehe 9 Julai, 2008 nilitoa Kauli ya Serikali katika Bunge lako Tukufu kuhusu utekelezaji wa miradi ya maji vijijini. Katika kauli hiyo, nilitoa maelezo kuhusu mipango ya Serikali ya kutoa huduma ya maji vijijini, tangu mwaka 1971 hadi sasa. Nilitoa maelezo kuhusu Programu ya Maji Vijijini ya miaka 20 iliyotekelezwa kati ya mwaka 1971 na 1991. Vile vile, nilitoa maelezo kuhusu Sera ya Maji ya mwaka 1991 na ile ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuandaa Sera ya Maji ya mwaka 2002, mwaka 2007 Serikali ilianza utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

Programu hiyo itatekelezwa hadi mwaka 2025. Programu hiyo kuu imegawanywa katika Programu tatu ambazo ni Rasilimali za Maji, Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini na Majisafi na Majitaka Mijini.

Mheshimiwa Spika, Kauli ya Serikali ya mwezi Julai, 2008, iliainisha utaratibu unaotumika katika kutekeleza miradi ya maji vijijini kupitia Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini.

Miradi hiyo ni ya aina mbili. Ile inayoweza kutekelezwa na Halmashauri zenyewe na yenye kuleta matokeo ya haraka na ile inayohitaji nguvu zaidi kutoka nje ya Halmashauri katika usanifu na usimamizi.

Mheshimiwa Spika, Kauli ya Serikali ya mwezi Julai, 2008 pia iliainisha suala la Wahandisi wa Maji walioajiriwa kwa ajili ya Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa ili kuimarisha utendaji na usimamizi wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, tangu waka 2007/2008 Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira imekuwa ikitekelezwa kupitia aina tatu za miradi:

Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini;

Miradi inayoleta matokeo ya haraka (*quick wins*);

Miradi mikubwa ya maji vijijini (maarufu kama mradi wa vijiji 10 katika kila Halmashauri).

Mheshimiwa Spika, Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini inatekelezwa na makundi makuu matatu ya wadau. Wananchi, Taasisi zisizo za kiserikali na Madhehebu ya dini na Halmashauri. Mchango wa wananchi katika ujenzi wa miradi ya maji unatolewa kwa njia ya fedha taslimu au/na nguvu kazi. Lengo ni kuimarisha umiliki wa miradi na uendelevu wa huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini ni matokeo ya utekelezaji wa Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Mradi ulianza kutekelezwa mwaka 2002 kwa ufadhili wa Benki ya Dunia na mchango wa Serikali. Mradi huo ulitekelezwa katika Wilaya 14.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Mradi ulihitimishwa mwezi Juni, 2008. Vijiji 119 kati ya 138 vilinufaika. Watu wapatao 521,630 kati ya 559,030 waliokusudiwa (sawa na asilimia 93) wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mradi haukutekelezwa katika vijiji 19 kutokana na kutopatikana kwa vyanzo vya maji. Vijiji hivyo sasa vimewekwa katika Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafi wa mazingira, mafundi binafsi 535 walipewa mafunzo ya kutengeneza mabamba ya vyoo vya shimo. Vyoo vya mfano 1,208 vilijengwa katika shule za msingi na kwenye taasisi za umma.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kupitia miradi ya maji inayotarajiwa kuleta matokeo ya haraka kulingana na mipango na vipaumbele vya Halmashauri zenyewe.

Kulingana na taarifa zilizotolewa na Halmashauri, hadi kufikia mwezi Juni, 2008 miradi ya maji 1,246 kati ya 1,478 (sawa na asilimia 84) iliyokusudiwa kujengwa katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 ilikuwa imekamilika.

Katika miradi iliyokamilika, vituo vya kuchotea maji 2,603 vimejengwa na watu wapatao 650,750 wananufaika na huduma ya maji.

Wananchi 885,867 wamehamasishwa kuhusu usafi wa mazingira na vyoo vya shimo 1,392 vimejengwa. Ofisi 42 kati ya 60 za Idara za Maji za Halmashauri

zimekarabatiwa. Ofisi 11 mpya kati ya 23 zimejengwa. Halmashauri 32 kati ya 84 zilizopewa fedha za miundombinu ya maji zilikamilisha utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na Halmashauri kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa 2008/2009, miradi ya maji 175 kati ya 1,328 iliyokusudiwa kujengwa (sawa na asilimia 13) ilikuwa imekamilika.

Watu 215,018 wamehamasishwa kuhusu usafi binafsi na uoshaji wa mikono, ambapo vyoo vya shimo 51 vimejengwa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, mwezi Juni, 2007, Serikali ilituma shilingi bilioni 19.25 kwenye Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa. Fedha hizo zilitokana na mkopo wenye masharti nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika. Kati ya Halmashauri 121, Halmashauri 84 zilipewa fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa Miradi ya Maji na kujijengea uwezo. Halmashauri 37 ambazo hazikutimiza masharti ya kupewa ruzuku, zilipewa fedha kwa ajili ya kujijengea uwezo tu.

Mwezi Juni, 2008 Serikali ilituma shilingi bilioni 11.95 kwenye Halmashauri zote nchini. Fedha hizo, zilitokana pia na mkopo nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Halmashauri 120 zilipewa fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa Miradi ya Maji pamoja na kujenga uwezo. Halmashauri 12 hazikuweza kutimiza masharti hivyo, zilipewa fedha kwa ajili ya kujenga uwezo tu.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009, Serikali imetenga shilingi bilioni 62.39 kwa ajili ya utekelezaji wa Programu. Fedha hizo, kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miradi, pamoja na kujenga uwezo, zinatumwa kwa Halmashauri ambazo zimetimiza masharti ya kupewa ruzuku ya maendeleo.

Halmashauri tano (5) ambazo hazijatimiza masharti ya kupewa ruzuku ya maendeleo, zimepewa fedha kwa ajili ya kujenga uwezo tu. Halmashauri hizo ni Masasi, Shinyanga, Kwimba, Manispaa ya Shinyanga na Jiji la Tanga. Serikali tayari imepeleka shilingi bilioni 23.5 kwenye Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, kati ya Juni, 2007 na Desemba, 2008, jumla ya shilingi bilioni 54.7 zilikuwa zimetumwa kwenye Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Jedwali Na. 3). Kiwango hicho kikubwa cha fedha ambazo zimetolewa kati ya mwezi Juni, 2007 na Oktoba, 2008 ni uthibitisho kwamba, Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, tayari imeanza kutekelezwa. Utekelezaji wa miradi katika vijiji kumi katika kila Halmashauri ni sehemu tu ya Programu hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza miradi mikubwa ya maji vijijini, maarufu kama Mradi wa Vijiji kumi katika kila Halmashauri, Halmashauri zitaajiri wataalam washauri ambao watasaidia kusanifu na kusimamia utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kupata Wataalam Washauri umefikia hatua zifuatazo, kwa makundi matatu ya Halmashauri niliyoyaainisha nilipowasilisha Kauli ya Serikali mwezi Julai 2008.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri 82: Hizo ni Halmashauri ambazo zilipata ridhaa mapema kutoka Benki ya Dunia ili kampuni zilizoorodheshwa (*shortlisted*), ziandae mapendekezo ya kiufundi ya miradi hiyo. Tathmini ya mapendekezo ya kiufundi iliwasilishwa Benki ya Dunia ili kupata ridhaa ya kufungua mapendekezo ya gharama za kifedha *(financial proposals).*

Mheshimiwa Spika, nafurahi kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Halmashauri zote 82 zimepata ridhaa hiyo. Halmashauri 30 zimefungua na kufanya tathmini ya mapendekezo ya kifedha. Halmashauri hizo ni Bahi, Chamwino, Manispaa ya Dodoma, Manispaa ya Iringa, Kilolo, Ludewa, Mji wa Njombe, Biharamulo, Manispaa ya Bukoba, Wilaya ya Bukoba, Karagwe, Muleba, Kasulu, Wilaya ya Kigoma, Manispaa ya Kigoma, Hanang, Mbulu, Manispaa ya Musoma, Wilaya ya Mbeya, Bariadi, Nanyumbu, Jiji la Mwanza, Sengerema, Mji wa Kibaha, Wilaya ya Kibaha, Rufiji, Wilaya ya Mpanda, Iramba, Manispaa ya Singida na Wilaya ya Singida, Lushoto na Jiji la Tanga.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri hizo zimeshauriwa kufanya majadiliano na kampuni husika na hatimaye kusaini mikataba ya kuanza kazi. Halmashauri 45 zilizobaki zipo katika hatua za kufanya tathmini. Halmashauri hizo zinashauriwa kukamilisha tathmini mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kasi ya Halmashauri katika kufanya tathmini na kuandaa taarifa na kupitisha zabuni kwenye bodi zao, matarajio ni kwamba, wataalam washauri watapatikana kuanzia mwezi Machi, 2009, tayari kuanza kazi.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri 17: Halmashauri hizo ni zile zilizorudia kufanya tathmini ya makampuni yalizopeleka maombi ya kufanya kazi za ushauri na ndizo zilizofuatia katika kupata ridhaa kutoka Benki ya Dunia. Halmashauri zote 17 tayari zimepata ridhaa ya kuendelea na hatua inayofuata ya kufungua mapendekezo ya kifedha ya kampuni zilizoomba kazi.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri hizi nazo zinaendelea na mchakato wa kufungua mapendekezo ya kifedha na kuyafanyia tathmini. Halmashauri mbili (Wilaya ya Babati na Wilaya ya Kilosa), tayari zimefungua na kufanya tathmini ya mapendekezo ya kifedha.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, Halmashauri zote 99 zilizopata maombi kutoka kwa kampuni mbalimbali, zimepata ridhaa ya kufungua mapendekezo ya kifedha.

Halmashauri zinatakiwa kuharakisha kufanyia tathmini hizo *proposals* ili hatimaye kusaini mikataba ili wataalam washauri waanze kazi mwezi Machi, 2009.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri 33: Hizo ni Halmashauri ambazo zilitakiwa kuanza upya zoezi na zilitoa matangazo ili kuyataka makampuni kupeleka maombi. Taarifa za Halmashuri hizo ziliwasilishwa Benki ya Dunia, ambayo tarehe 9 Desemba, 2008, ilitoa ridhaa kampuni husika (*shortlisted*) ziandae mapendekezo na kuwasilisha kwa ajili ya tathmini ya kiufundi.

Kampuni hizo zimetakiwa kuwasilisha mapendekezo yao ifikapo tarehe 18 Februari, 2009. Matarajio ni kwamba, wataalam washauri kwa ajili ya Halmashauri hizo, watapatikana kuanzia mwezi Juni, 2009. Orodha ya Halmashauri katika makundi yote matatu imeonyeshwa kwenye Jedwali Na. 4.

Mheshimiwa Spika, Wahandisi wa Maji; kama nilivyoeleza katika Kauli ya Serikali mwezi Julai, 2008, mwezi Novemba, 2006, Wizara yangu iliajiri wahandisi wa maji 96 kwa mkataba wa mwaka mmoja. Walipangiwa vituo vya kazi kwenye Halmashauri mbalimbali na Sekretarieti za Mikoa, ambazo zilikuwa hazina Wahandisi. Zoezi hili lilifanyika kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini na Sekta ya Maji kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, baada ya muda wa mkataba kumalizika, ilibidi Wizara iongeze mkataba mwingine wa mwaka mmoja kwa Wahandisi ambao walikuwa hawajaajiriwa na Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa. Ilipofika mwezi Novemba, 2008, Wahandisi 15 walikuwa wameacha kazi, wahandisi 48 waliajiriwa kwenye Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa na wahandisi 33 bado hawajapata ajira. Taratibu za Halmashauri kuwaajiri Wahandisi waliobaki zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha ufanisi wa utekelezaji wa Programu, nyenzo za kufanyia kazi zitanunuliwa na kusambazwa kwenye Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa. Nyenzo hizo ni pamoja na magari, pikipiki na vifaa vya ofisi. Kuhusu vifaa vya ofisi, matangazo yalitolewa, zabuni zimefunguliwa na tathmini ya zabuni imefanyika. Matarajio ni kwamba, vifaa hivyo vitapatikana mwezi Juni, 2009. Kuhusu pikipiki, matangazo yalitolewa pia, zabuni zimefunguliwa na tathmini ya zabuni imefanyika. Benki ya Dunia imeridhia taarifa ya tathmini ya zabuni hiyo. Wizara ipo katika hatua ya kukamilisha maandalizi ya mkataba. Matarajio ni kwamba, pikipiki 252 zitapatikana mwezi Juni, 2009.

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa Magali, matangazo ya zabuni yalitolewa na zabuni zimefunguliwa. Tathmini ya zabuni inafanyika na matarajio ni kwamba, magari 111 yatapatikana ifikapo mwezi Agosti, 2009.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapenda kulithibitishia Bunge lako Tukufu kwamba, Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, imeanza kutekelezwa tangu mwaka wa fedha wa 2007/2008. Kati ya Juni, 2007 na Juni, 2009 Serikali itakuwa imetumia shilingi

bilioni 93.59 kutoka katika Mfuko Maalum wa Utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*Basket Fund*).

Katika kutekeleza Programu hiyo, Mipango ya Halmashauri ya miradi inayoleta matokeo ya haraka, itaendelea kutekelezwa. Fedha zitaendelea kutolewa kulingana na jinsi taarifa za utekelezaji wa miradi na zile za matumizi ya fedha za kila robo mwaka zitakavyokuwa zinawasilishwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kupata wataalam washauri wa kuzisaidia Halmashauri kusimamia utekelezaji wa programu ni sehemu tu ya utekelezaji wa Programu. Wataalam Washauri wataainisha vyanzo vya maji, watafanya upimaji na usanifu wa miradi na wataandaa makabrasha ya zabuni za ujenzi wa mradi wa vijiji kumi katika kila Halmashauri.

Kazi hizo zinatarajiwa kuchukua miezi 9 kukamilika. Hivyo basi, ujenzi wa miradi unatarajiwa kuanza mwezi Januari, 2010 kwa zile Halmashauri 41 zilizotangulia.

Mheshimiwa Spika, linalojitokeza katika kauli hii ni kwamba, fedha za kutekeleza Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira, pamoja na kwamba hazitoshi, ukilinganisha na ukubwa wa tatizo, zimeanza kufika kwenye Halmashauri. Wanachohitaji wananchi ni matokeo; wanahitaji maji.

Hivyo basi ni jukumu la kila mhusika, hasa katika ngazi ya Halmashauri, kuhakikisha kwamba, fedha hizi zinatumika kwa yale yaliyokusudiwa.

Kwa upande wa Serikali Kuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Wizara ya Fedha na Uchumi na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, tutaongeza juhudi katika kuhakikisha upatikanaji wa fedha, usimamizi wa matumizi yake, kuzisaidia Halmashauri katika masuala ya kiufundi na kitaalam na kuzijengea uwezo na kujaribu kufupisha muda wa kupatikana kwa ridhaa kutoka Benki ya Dunia katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya kumpatia kila Mtanzania maji ni kubwa. Lakini tunaweza kuikabili iwapo kama Taifa tutatoa kipaumbele na kuwekeza katika Sekta ya Maji, jambo ambalo Mheshimiwa Waziri Mkuu, amelihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, litafanyika.

Mheshimiwa Spika, kauli hii ina majedwali manne, ikiwa ni pamoja na orodha ya mgao wa fedha kwa kila Halmashauri kuanzia Juni, 2007 mpaka Oktoba, 2008. Kwa ukamilifu na kuweka rekodi sawa, naomba majedwali yasomeke katika *Hansard* kama sehemu ya Kauli hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, Wananchi, Taasisi za Kiserikali na zisizo za Kiserikali, Madhehebu ya Dini, Washirika wa Maendeleo na wadau wote wa Sekta ya Maji, kwa kuungana na Serikali katika juhudi zake za kuwapatia wananchi maji safi, salama na ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. Maji ni Uhai na Usafi wa Mazingira ni Utu.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, kwa taarifa ambayo inajitosheleza na kwa sisi Waheshimiwa Wabunge, itatusaidia kutathmini ni kitu gani kimefanyika kwa fedha zile ambazo zimekwisha wasilishwa kwenye Halmashauri zetu. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunarejea sasa katika mpango uliowasilishwa na Waziri wa Fedha na Uchumi na nimepata majina kama matatu na kwa sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, tupate maoni ya Kamati.

MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA - MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 94 ya Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, inaitaka Bunge kukaa kama Kamati ya Mipango katika Mkutano wake wa Mwezi Februari ili kujadili na kushauri kuhusu mapendekezo ya Mpango wa Taifa, unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka wa fedha unaofuata. Katika kufanya hivyo, Kamati yangu tarehe 6 Februari, 2009 ilipata fursa ya kuchambua mwongozo wa kuandaa mpango wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2009/2010 -2011/12 uliowasilishwa na Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, Mbunge na Waziri wa Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Spika, Taarifa iliyowasilishwa na Waziri, ilionyesha Mapitio ya Mwenendo wa Uchumi na Bajeti kwa Mwaka 2008/2009, ilionyesha uchumi wetu kukua kwa asilimia 7.5 ifikapo Juni, 2009 ikiwa ni asilimia 0.3 chini ya lengo. Hali ya mfumko wa bei si ya kuridhisha, iliyofikia asilimia 13.5 Disemba, 2008 kutokana na kupanda kwa bei ya vyakula, pamoja na ukosefu wa mvua. Riba za amana zimeongezeka hadi asilimia 2.68 kutoka 2.26 Mwezi Julai, 2008 na riba ya mikopo imeendelea kuwa juu kutoka asilimia 15.05 hadi kufikia asilimia 16.05. Uuzaji nje umekuwa mdogo.

Akiba ya fedha za kigeni inahimili uagizaji wa bidhaa na huduma kwa miezi 4.9. Mwenendo wa Bajeti ya Serikali Julai hadi Disemba, 2008, lengo la ukusanyaji limefikia asilimia 93 ya lengo, upungufu umetokana na baadhi ya vyanzo kutofanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Bajeti ya Serikali umetayarishwa kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005. Hata hivyo, mchakato wa maandalizi wa mwongozo huu umeshirikisha wadau mbalimbali, ikiwa ni pamoja na sisi Waheshimiwa Wabunge, ambapo tutaijadili taarifa hii kwa siku mbili.

Mheshimiwa Spika, katika kuchambua mpango na bajeti iliyotayarishwa na inayotarajia kutekelezwa, Kamati imetafakari hali ya sasa ya uchumi duniani, iliyokumbwa na mtikisiko mkubwa wa fedha na kiuchumi. Tanzania haiwezi kujitenga

na mazingira ya uchumi wa dunia na athari zake; hivyo, kuilazimisha Serikali kuchukua hatua zote za tahadhari hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, taarifa iliyowasilishwa na Waziri, inaonesha mapitio na mwenendo wa uchumi na bajeti kwa mwaka 2008/2009, iliyoonesha uchumi wetu kukua kwa asilimia 7.5 ifikapo Juni, 2009 ikiwa ni asilimia 0.3 chini ya lengo; hali ya mfumko wa bei si ya kuridhisha; ilifikia asilimia 13.5 Disemba 2008 kutokana na kupanda kwa bei ya chakula; pamoja na ukosefu wa mvua; riba za amana zimeongezeka hadi asilimia 2.68 kutoka 2.26 2008; riba ya mikopo imeendelea kuwa juu kutoka asilimia 15.5 hadi kufikia asilimia 16.05; uuzaji nje umekuwa mdogo; na akiba ya fedha za kigeni inahimili uagizaji wa bidhaa na huduma kwa 4.9. Mwenendo wa Bajeti ya Serikali Julai hadi Disemba, 2008, lengo la ukusanyaji limefikia asilimia 93 ya lengo, upungufu umetokana na baadhi ya vyanzo kutofanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia Mpango huu uliopo mbele yetu, Kamati ya Fedha na Uchumi, imezingatia hali halisi inayoweza kujitokeza kutokana na msukosuko wa masoko ya fedha duniani na jinsi itakavyoathiri Mipango na Bajeti yetu. Msukosuko huu unaweza au umeanza kuathiri katika maeneo yafuatayo:-

(a) Kupungua kwa kasi, bei ya bidhaa muhimu zisizo asilia ambazo tunauza nchi za nje. Takwimu zinaonesha hadi tarehe 22 Januari, 2009 marobota ya pamba 138,011 yako kwenye vinu kutokana na kukosa soko. *SHIRECU* ina tani 800 za mbegu za pamba ghalani, kwa kushindwa kuuza kutokana na bei ndogo.

(b) Idadi na matumizi ya Watalii wanaokuja Tanzania inaweza au imeshaanza kupungua.

(c) Kupungua kwa ajira kwenye makampuni, pamoja na mategemeo ya kupungua misaada tunayopata toka kwa wahisani. Hali hii ni ya kuchukua tahadhari, hasa tukielewa kuwa Bajeti yetu bado ni tegemezi kwa asilimia 34.

Mheshimiwa Spika, kutokana na sura hiyo hapo juu, Kamati imebaini kuwa msukosuko wa uchumi duniani, athari zake kwa Tanzania ni dhahiri na za kweli na tujiandae kupambana nazo. Serikali ibuni mikakati madhubuti ya kushughulikia msukosuko huu. Njia ya pekee ya kufanikisha hali hii ni kupitia utayarishaji na uaandaji wa mipango na bajeti imara na makini inayotarajiwa kutekelezwa na Serikali katika kipindi kijacho.

Mhehsimiwa Spika, Kamati inaitanabahisha Serikali kuwa, tunahitaji Mipango ambayo itatekenya uchumi wetu ili kutuepusha na kutumbukia kwenye dimbwi la kudorora kwa uchumi wetu *(recession)* na hatimaye hata kuanguka *(depression).* Serikali ijihakikishie yenyewe kuwa, inaandaa mpango wa kunusuru uchumi wetu na madhara yanayotunyemelea kutokana na msukosuko huu. Kipindi cha sasa cha kuendesha uchumi, kinapambana na mazingira tofauti ukilinganisha na miaka miwili au mitatu iliyopita. Serikali ichukulie kuwa, kipindi cha sasa si cha kawaida ili kuepuka dhana ya *business as usual.*

Mheshimiwa Spika, mantiki ya hoja ya Kamati ni kuwa, mwongozo ulioandaliwa na Serikali hautasaidia mipango ya nchi kama orodha ya vipaumbele inakuwa ni kubwa. Kamati inaishauri Serikali kuchagua vipaumbele vichache vinavyolenga yale maeneo yatakayoibua uchumi haraka, pamoja na kuzalisha mapato *(income creation)* na kuongeza ajira katika uchumi *(employment creation)*. Maeneo yafuatayo yaangaliwe na Serikali:-

(a) Eneo la Miundombinu: Katika mpango ujao, Serikali isifanye makosa ya kupunguza kasi katika eneo la kutekeleza programu zinazoendelea za miundombinu. Upo umuhimu wa kuendelea kuboresha barabara zetu kuu na zile za vijijini ili kuhakikisha mtiririko wa tija wa huduma na bidhaa katika uchumi wetu. Katika eneo hili tunapoteza fursa nyingi za kuongeza mapato yetu kwa kushindwa kutumia faida ya asili tuliyonayo ya kijiografia, ambayo inaweza kutufanya kuhudumia nchi jirani hususan katika masuala ya usafirishaji na bishara ya huduma na bidhaa *(transit trade*). Lango la biashara la nchi za Rwanda, Burundi, DRC, Uganda, Zambia na kadhalika ni bandari yetu ya Dar es Salaam.

(b) Eneo la Kilimo: Changamoto kubwa ni kuendelea kuboresha na kuiimarisha sekta hii kwa mapana yake. Moja ya kipaumbele ni Serikali ijenge mazingira bora ya kuvutia uwekezaji katika kilimo hasa kutoka sekta binafsi. Ipo haja ya kujenga mpango mahususi wa muda mfupi wa ku-*stimulate* (kuchochea), uzalishaji katika Kilimo. Ikibidi hata zile sheria ambazo zinacheleweshe sekta binafsi kujiingiza kwenye kilimo, zirekebishwe haraka. Sekta binafsi imekuwa na muda mgumu sana wakati wa uanzishaji wa *Contract Farming*, ambayo imedhihirisha kuwa aina hii ya kilimo huongeza mapato ya wakulima zaidi ya mara nne ya yale wanayoyapata wakulima wadogo. Kamati inaishauri Serikali kuongeza jitihada zake katika kuongeza upatikanaji wa mbolea, madawa, zana na pembejeo za kilimo; kuongeza huduma za ugani; na bei za usafirishaji mazao ya wakulima zilenge katika kuinua vipato vyao na waweze kuzalisha ziada. Mkakati wa Serikali wa kununua matrekta na kuyatoa au kuwauzia wakulima utekelezwe haraka.

(c) Eneo la Mifugo na Uvuvi ni eneo lingine linaloweza kuibua uchumi wetu haraka.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali halisi tuliyojifunza, mafanikio makubwa kwa upande wa Serikali katika kutekeleza Mpango wa Mwaka ujao ni kuweka mazingira ya kushirikisha sekta binafsi kikamilifu katika uzalishaji. Kwa mfano, itakuwa ni hatua ya tija ikiwa Serikali itakuwa na majadiliano ya haraka na wenye viwanda (*CTI*) na Chemba ya Wafanyabiashara na Wakulima (*TCCIA*) ili watoe ushauri juu ya uwajibikaji wao katika kusaidia kuchangia katika kuendeleza uzalishaji katika yale maeneo yanayozalisha mali moja kwa moja *(directly productive sectors).* Serikali ishirikiane na wadau hawa si katika kutoa mawazo ya mfumo sahihi wa kodi, bali waulizwe wanataka nini ili wazalishe zaidi, kama njia ya kujitosheleza ili kuhimili kipindi kigumu kilichopo mbele yetu

Mheshimiwa Spika, eneo la nne ni lile la biashara hususan ile na nchi jirani *(transit trade).* Serikali ichukue hatua za haraka za kuboresha utendaji wa bandari zetu, hasa ile ya Dar es Salaam. Inachukua hadi siku 25 sasa kwa bidhaa kupakuliwa bandarini. Wingi wa mizigo bandarini (*congestion*), pamoja na barabara hafifu ziendazo kwenye maeneo ya nchi jirani, utakwamisha juhudi zote za Serikali za kukuza uchumi na kuinua mapato. Sote tunafahamu, mikakati inayofanywa hivi sasa na nchi zote jirani za kutafuta lango lingine la kutolea na kuingizia huduma na bidhaa zao, baada ya kupata hasara inayotokana na ufanisi mdogo wa Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, aidha, matatizo ya reli yetu ya kati yanahitaji msukumo wa haraka. *Transit trade* itakua zaidi kwa kuboresha barabara zetu katika Ukanda wa Kati *(Central Coridor*). Takwimu zinaonyesha nchi jirani za Rwanda, Burundi na *DRC*, zina bidhaa zaidi ya takribani tani nne milioni, ambazo zinaweza kuhudumiwa na bandari yetu kila mwaka. Taarifa ya Serikali inaonyesha kuwa, eneo la ushuru wa forodha halikufanya vizuri. Kamati inadhania kuwa, moja la eneo lililochangia hali hiyo ni utendaji duni wa shughuli za bandari. Aidha, misamaha ya kodi pia imeweza kuchangia katika hili huko Zanzibar, misaada imefikia asilimia 54 wakati Tanzania Bara imefikia asilimia 61.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine linalobidi kupewa kipaumbele ni lile la Sekta ya Fedha, hasa katika kuendeleza upatikanaji wa mikopo na hatua nyingine za uwezeshaji. Yapo maeneo yanahitaji kuangaliwa kama ifuatavyo:-

(a) Kuanzisha na kuimarisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo, ambayo inabidi iwe na mtaji imara ili kusaidia uwekezaji. Taarifa ya Serikali inaonyesha kuwa, hadi Disemba, 2008, mikopo iliyotolewa kwenda sekta binafsi ilikuwa shilingi 4,376.4 bilioni, ikilinganishwa na shilingi 2,093.6 bilioni zilizotolewa Disemba, 2007.

Mheshimiwa Spika, swali la msingi hapa ni kujiuliza fedha hizi zimewekezwa katika maeneo gani na *impact* yake katika kukuza uchumi. Kwa maana nyingine mikopo inatumikaje; *how do we invest in wardly* kukuza uzalishaji kiwandani, kwa kuwa nchi yetu inakabiliwa na uhaba wa fedha za kigeni, lakini kumekuwa na tabia ya uagizaji wa bidhaa toka nje usio wa lazima.

(b) Serikali iwe makini katika kutoa mikopo kwa sekta binafsi, kwa kuhakikisha kuwa inaelekezwa kwenye maeneo ya uzalishaji mali, badala ya kuielekeza kwa wafanyabiashara wanaoagiza bidhaa hafifu kutoka nje.

(c) Kwa kuwa bidhaa nyingi zinazoagizwa kutoka nchi za nje, zinakuwa na hitilafu (*bidhaa feki*), Serikali iwe makini katika kudhibiti uingizaji wa bidhaa feki toka nchi za nje na hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yao. Soko letu lisiwe dampo la vifaa duni.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeipongeza Serikali kwa hatua yake ya kuendeleza zoezi zima la Uwezeshaji wa Uchumi wa Wananchi *(Economic Empowerment).* Hata hivyo, eneo moja ambalo bado halijafanyiwa kazi ni kuwafikia walengwa walio wengi.

Mfano mzuri, ingawaje mabilioni ya JK yalilenga kuwasaidia wananchi wenye uwezo mdogo na kipato cha chini, waliofaidika ni wachache sana. Utaratibu wa kupitisha fedha zile benki unawaacha nje wananchi wengi ambao wangefaidika kwa wingi na kwa kiwango kikubwa. Serikali ilirekebishe hili ili iweze kuinua vipato vya wazalishaji na wajasiriamali wadogo na hapo hapo kuongeza ajira isiyo rasmi katika kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza ushirikishwaji wa Viongozi wa Serikali, Halmashauri za Wilaya na Majimbo, ili kusaidia kuwatambua walengwa wanaopaswa kufaidika na huduma hizi nje, hasa wale ambao ni wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu, limeshapitisha Miswada ya Sheria ambayo utekelezaji wake utasaidia sana kuwezesha wananchi. Bunge bado linasubiri utekelezaji wa sheria hizo ambazo ni *Unit Title Act; Mortgage Finance Act;* na *Finance Leasing Act*. Maeneo haya, yafanyiwe kazi haraka kwani yatasaidia ngazi zote za wananchi katika kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Benki Kuu katika kuonyesha vigezo na viashiria vya usalama na umadhubuti wa sekta ya fedha, imeonyesha kuwa Benki zetu zina ukwasi wa kutosha kukidhi malipo kwa wateja *(liquidity ratio)* kwa asilimia 42, wakati kigezo kinachohitajika ni asilimia 20. Aidha, uwiano wa mikopo kwa amana *(deposits)* ni asilimia 68 wakati mahitajio ni asilimia 80.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kwamba, kwa viashiria na vigezo hivi viwili, tafsiri yake ni kuwa mabenki yanakopesha kwa viwango vidogo. Hali hii inaleta ukwasi wa ziada (*Excess Liquidity)* katika mabenki. Swali la kujiuliza ni kwa nini mabenki yetu yapo katika hali hii kwenye uchumi wenye njaa ya mikopo ? Uzoefu unaonyesha kuwa, uchumi wa nchi hauwezi kuendelea bila mikopo ambayo ni chanzo muhimu cha mitaji, kwa wajasiriamali wadogo na wale wakubwa (wawekezaji). Hili ni eneo ambalo inabidi liangaliwe na Serikali kwa karibu hasa ikizingatiwa kuwa bado viwango vya riba ni vya juu. Mipango yetu ilenge katika kupunguza riba ili kuhamasisha uwekezaji nchini, ambao utaibua uchumi wetu. Hivi sasa nchi nyingi zimeshaona umuhimu wa kupunguza riba ili ku-*stimulate* uchumi kupitia uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, utaratibu wa fedha taslimu hauwezi kuendeleza uchumi wetu kwa kasi kubwa. Mpango wetu hauna budi kutoa kipaumbele katika eneo la kuendeleza uwekezaji *(Investment Drive).*

Mheshimiwa Spika, mipango yetu haitasaidia kuboresha uchumi kama hatutaweka kipaumbele katika kuhakikisha uendelevu wa uwekezaji kwa kupunguza gharama za uwekezaji. Katika eneo hili, Tanzania tunashika nafasi ya juu katika Afrika Mashariki. Kamati inashauri kipaumbele kiwekwe kwenye mipango ya kupunguza gharama za uwekezaji na zile za kuendesha shughuli za uchumi *(reduction of costs of doing bussiness*). Kamati inaishauri Serikali kuendelea kupambana na tatizo la urasimu na lile la ucheleweshaji wa utoaji maamuzi *(delays in decision making process).* Eneo hili linaendana na kushughulikia gharama kubwa za usafiri na nishati zitokanazo na

miundombinu hafifu. Hali hii ikiendelea, uchumi utajenga mazingira ya wawekezaji kutokuwa na uhakika wa hatima ya mali na mapato yatokanayo na uwekezaji *(predictability* na *consistency).*

Mheshimiwa Spika Kamati imeishauri Serikali kuangalia kwa karibu maeneo kadhaa yafuatayo:-

(a) Suala la utulivu wa bei *(price stability),* chanzo kikubwa cha mfumko wa bei hivi sasa. Hii ni changamoto kubwa. Mfumko wa bei uliofikia asilimia 13. 5 hivi sasa sehemu kubwa inatokana na kupanda kwa bei ya chakula, yaani asilimia 8. Kinachotuletea matatizo mara nyingine uwezo mdogo wa uzalishaji na vilevile usambazaji/ugavi dhaifu wa chakula nchini. Kuyasawazisha mambo haya, inabidi kuelekeza mtaji na mikopo mingi kwenye Kilimo na kuweka vivutio vya makusudi ili kuhamasisha sekta binafsi. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuchukua baadhi ya hatua kadhaa katika Mipango iliyopita, kwa mfano, ile ya kufuta ushuru wa forodha na ile ya kufuta kodi ya ongezeko la thamani katika zana na vifaa vya Kilimo. Hata hivyo, kwa hali ilivyo sasa, vivutio hivi havitoshi tukizingatia hifadhi duni, masoko yanayoyumba, pamoja na tatizo la miundombinu iliyo laini, yaani ya kitaasisi na ile migumu, yaani ile ya barabara na nishati. Uchumi unafikia kuwa na hali ya uhaba wa chakula usiokuwepo *(artificial shortage*) na hivyo kukuza uhitaji (*demad push/pull*), ambao hatma yake ni bei kubwa ya chakula. Serikali kupitia mpango huu, haina budi kushughulikia changamoto hizi.

Swali la kujiuliza ni kwa nini bei ya chakula iko juu ambapo bei ya mafuta imeteremka?

Mheshimiwa Spika, hali ya nishati ya umeme bado haiaminiki na haitabiriki katika uchumi wetu *(unreliable and unpredictable),* Kamati inaishauri Serikali pamoja na kusingizia tatizo la uhaba wa maji hasa wakati wa ukame ni vyema Serikali ikatoa kipaumbele katika ukarabati makini wa nyenzo na mitambo iliyopo *(maintanance and upkeep).* Hivi sasa tuangalie kiasi cha umeme kinachoweza kufuliwa na mitambo yetu MW 1000 *(rated capacity)* na tukilinganisha na viwango tunavyozalisha MW 500 au 600 *(generated capacity),* lipo pengo kubwa karibu la asilimia 50. Hali hii haitakuwa endelevu. Ni vyema *financial recovery* ya *TANESCO* ilenge katika hili la *maintanance* ili tuweze kuzalisha MW 100 na hivyo kupunguza tatizo kwa kiwango kikubwa. Kamati vilevile imeishauri Serikali kuendelea na jitihada zake za kuendeleza nishati mbadala, hususan matumizi makubwa ya gesi tunayozalisha nchini.

Mheshimiwa Spika, ipo haja kubwa ya mipango yetu ijayo kujikita kwa makusudi katika eneo la kutekenya uchumi wetu kutokutegemea sana mafuta ; petroli na dizeli kama vyanzo vikubwa vya kodi. Bei ya mafuta duniani imepungua kwa asilimia 60 na inatarajiwa kufikia US$ 50 kwa pipa kwa mwaka 2009 na labda ikipanda kidogo kufikia US$ 60 mwaka 2010. Kushuka kwa bei ya mafuta kunatakiwa kujionyesha katika kupungua kwa gharama ya bidhaa hii, ambayo itapunguza gharama katika maeneo mengi mengine hususan ya uzalishaji viwandani na usafirishaji. Kamati bado inaendelea kuishauri Serikali, ipunguze kodi za bidhaa ya mafuta ziendazo Serikalini. Katika bei

iliyopo vituoni takriban shilingi 600 ni kodi iendayo Serikalini kwa kila lita. Hiki ni kiwango kikubwa ; wataalam watafute *formula* ya kupunguza kodi hii na kubakiza tozo la barabara tu (*road toll*). Hali hii itaibua uchumi kwa kiwango cha juu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kubuni njia mahususi za kuepusha uchumi kuwa na ukosefu wa nishati hii muhimu ya mafuta, kama ilivyojitokeza mwezi au miezi miwili iliyopita. Kamati inadhani hapa tatizo ni ucheleweshaji wa kutoa maamuzi kwa vile tayari Bunge hili lilikwishaamua kuwa, Serikali ianzishe hifadhi ya mafuta kupitia *TPDC,* ambayo ina ubia na *TIPER*. Katika msukosuko huu wa uchumi na bei za mafuta kushuka ni wakati sahihi sasa kujenga hifadhi yetu, kwa mantiki tu kwa gharama ndogo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine la kupewa kipaumbele haraka ni lile la kutekeleza hatua na ushauri uliotolewa na Tume ya Bomani unaohusiana na marekebisho ya kodi mbalimbali na maeneo mengine katika sekta ya madini. Hatua za muda mfupi, kati na muda mrefu, lazima zichukuliwe haraka ili kuongeza mapato ya Serikali. Msukosuko wa uchumi duniani umepunguza mapato kutokana na *exploration* kutoka US$ 90 milioni hadi kufikia US$ 45 milioni hivi sasa. Hivi sasa dhahabu ndio nyenzo ya kuimarika na inayoaminika ya kuhifadhia akiba (*safe heaven*).

Mheshimiwa Spika, Kamati imekiri kuwa, Serikali imeanzisha programu nyingi za kupunguza umaskini baina ya jamii ya Watanzania. Programu kubwa ya MKUKUTA, pamoja na vitengo vyake, vimeshirikishwa na hatua mbalimbali ambazo zote zimelenga kusaidia wananchi wenye kipato cha chini ; kwa mfano, MKURABITA, *TASAF, SELF, SACCOS, SMES, CREDIT GARANTEE SCHEME* ya Benki Kuu, Mabilioni ya JK na kadhalika. Hata hivyo, pamoja na hatua zote hizi, inadhihirika kuwa wengi wa wananachi hawajizielewa. Tafsiri ya hali hii ni kuwa elimu na uhamasishaji bado ni ndogo. Pili, walengwa hawajafikiwa kikamilifu na programu hizo na tatu *impact* ya programmu hizi hasa katika eneo la kupunguza umaskini wa kipato bado haijafikia viwango vya juu. Serikali ishughulikie changamoto hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika**,** Kamati inakiri kuwa, moja ya eneo linalohitaji kipaumbele ni Serikali kuongeza juhudi katika kusaidia, kuendeleza na kuboresha viwanda vya nyumbani vitakavyokidhi uhitaji wetu, yaani *Home Based Demand Industries.* Lengo hili tutalifikia ikiwa viwanda vya usindikaji mazao yetu vitasaidiwa ili vifanye kazi kwa ukamilifu. Kwa mfano, hatuna haja ya kuuza nje korosho ghafi. Viwanda vyetu vyote vya kubangua korosho vikiwezeshwa vitaweza, viwanda vya Pamba hivi sasa marobota zaidi ya 138,000 yapo katika maghala hatuwezi kusindika, kiwanda cha kutengeneza matairi, viwanda vyetu vya nguo, viwanda vya usindikaji matunda na kadhalika.

Mkakati uwe ni kuhakikisha viwanda vyetu vilivyopo, pamoja na vile vya kutengeneza mafuta ya kula, vinafanya kazi kwa viwango vilivyopo *(rated capacities).* Aidha, yale maeneo ambayo yataweza kupunguza matumizi ya fedha zetu za kigeni, nayo inabidi yaangaliwe. Kwa mfano, kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa Kiwanda cha Mbolea cha Minjingu, viwanda vya zana, viwanda vya gesi na kadhalika *(import*

substitution), vitapunguza viwango vya nchi vya kununua bidhaa husika toka nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vyanzo bora vya mapato ni muhimu sana katika kuongeza makusanyo ya mapato ya Serikalini, Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Bunge na wadau muhimu katika mchakato wa maandalizi ya bajeti, tujenge tabia ya kujadili kwa kina mikakati ya kuibua vyanzo muhimu vya ukusanyaji wa mapato kama tunavyotumia muda mrefu kujadili matumizi ya Bajeti ya Serikali. Bunge limekuwa linatumia muda mdogo sana kujadili vyanzo vya mapato ya Serikali.

(b) Serikali iweke mikakati bora katika kutangaza na kuvutia watalii hasa katika nchi ambazo hazizungumzi kiingereza mfano China, Japan, Korea na kadhalika.

(c) Katika suala zima la kukusanya mapato, Serikali Kuu iendelee kutoa elimu kwa Serikali za Mitaa katika suala la kukusanya mapato. Hili ni eneo linalovujisha mapato makubwa kwa Serikali na uchumi kwa ujumla.

(d) Waziri wa Fedha na Uchumi awe na utaratibu wa kuwatembelea wazalishaji na wafanyabiashara mikoani, kuzungumzia changamoto mbalimbali katika suala la kodi ili kuwapa moyo katika kulipa kodi za Serikali na kujua kodi wanayolipa inatumikaje

(e) Kwa kuwa kumekuwa na uingizaji holela wa bidhaa katika mipaka yetu na hivyo kukwepa kulipia ushuru, Serikali iweke mikakati ya kutembelea mipaka yetu na kudhibiti uingizwaji huo holela.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Tanzania inayo ardhi kubwa na yenye rutuba, tatizo ni kutokuwa na mvua za uhakika na zana duni za kilimo na wataalam. Kwa kuwa kilimo cha umwagiliaji ndio kitakuwa mkombozi wa uchumi wetu, Kamati inashauri Serikali kama ilivyosema kwenye hotuba yake:-

(a) Serikali ichague maeneo machache bora ya kilimo na kuweka mikakati bora katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji na kutumia zana za kisasa. Mfano, Bonde la Mto Rufiji ni karibu na bandari na maji ni mengi. Mikoa ya Morogoro, Iringa, Mbeya, Ruvuma na Rukwa, iwekewe mikakati maalum katika kuendeleza kilimo cha kisasa. *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa ruzuku ya mbolea ikitumiwa vizuri itasaidia sana kuboresha kilimo, Kamati inashauri Serikali kuweka mikakati ya kutoa ruzuku ya mbolea mapema iwezekanavyo (Julai, Agosti), kabla msimu wa kilimo haujaanza ili mbolea hasa ya kupandia iweze kutumika kwa wakati.

(c) Kwa kuwa kilimo cha umwagiliaji maji bado kinakabiliwa na tatizo la uhaba wa miundombinu na wataalam wa umwagiliaji, Serikali inatakiwa kuweka mikakati ya kuboresha miundombinu na wataalaam wa umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha taratibu za kufuatilia utekelezaji wa Mpango na Bajeti (*monitoring of plan and budget execution)* ni msingi mkuu katika kuhakikisha matumizi bora ya fedha na rasilimali za Serikali. Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(a) Serikali iweke mikakati ya kusimamia na kudhibiti matumizi ya Serikali na hasa kuimarisha utendaji kazi wa Bunge.

(b) Serikali itumie fedha za maendeleo kwa malengo yaliyowekwa na kwa usimamizi wa hali ya juu, kamwe Serikali wasiendelee kutumia pesa za miradi ya maendeleo, kulipa posho na gharama nyingine ambazo sio za lazima.

(c) Serikali iboreshe maadili ya utendaji kazi kwa watumishi wa Serikali na taasisi zake.

(d) Kwa kuwa maandalizi ya malengo yanayopimika *(performance indicators)* ni muhimu sana katika utendaji kazi, Serikali ianzishe utaratibu wa *contract performance*, kwani nchi nyingi sana zimeanzisha *contract performance*, kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utendaji kazi. Yote haya kwa ujumla wake, yataiwezesha Serikali kutathmini viwango vya fedha vilivyotolewa na thamani na matokeo halisi *(value for money).*

Mheshimiwa Spika, upo umuhimu wa kutengeneza Mpango Maalum wa kuinua uchumi wa Tanzania. Kwa kuwa kipindi hiki sote tunakubaliana kuwa uchumi duniani unadorora; ni lazima Serikali ijiandae na mpango mahususi wa dharura wa kujikomboa kiuchumi. Kutokana na matatizo ya uchumi duniani, hata nchi ya Marekani ambayo ina nguvu kubwa kiuchumi, imeandaa mpango wenye thamani ya dola za Kimarekani takriban milioni 750 kwa ajili ya kuweka mikakati ya kujikwamua kiuchumi. Hali hii inaishawishi Kamati kuikumbusha Serikali yafuatayo:-

(a) Serikali iandae mpango huo wake wa kuinua uchumi kama nchi nyingine zinavyofanya ili kupambana na dalili zote za kudorora uchumi wetu zitakapojitokeza. Tuondokane na tabia ya kufanya kazi kama vile hali ni shwari *(business as usual).*

(b) Kwa kuwa Rais wa Uchina anatarajiwa kuzuru nchi yetu mwaka huu, Serikali itumie ujio wa Rais wa Uchina, kuandaa Mkakati Maalum wa Kuinua Uchumi wetu kwa kushirikiana nao ili kuibua miradi, kwa mfano, Mradi wa Nishati ya Umeme wa *Stiggler's Gorge*, wenye uwezo wa kuzalisha umeme wa megawatt 2000 na mikakati ya kupata mikopo ya muda mrefu katika kilimo, viwanda, utalii na kadhalika.

(c) Kwa kuwa ni muhimu kwa Serikali kuunda chombo cha mipango katika kupanga mipango ya kiuchumi, Kamati inaishauri Serikali kuunda Tume ya Mipango kama ilivyokuwa siku za nyuma ili chombo hicho kiweze kusaidia kuinua uchumi tulionao

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha taarifa yangu, napenda kwanza, kuwatambua Wajumbe wanaounda Kamati hii ya Fedha na Uchumi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda, Mwenyekiti, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Andrew J. Chenge, Mheshimiwa Anthony Diallo, Mheshimiwa Fatma Abdulhab Fereji, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Athuman Said Janguo, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Dkt. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Monica N. Mbega, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Mossy Mussa, Mheshimiwa Devota M. Likokola, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Dkt. Omary Nibuka Mzeru, Mheshimiwa Suleiman Ahmed Sadiq, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir na Mheshimiwa Sijapata Nkayamba.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wanakamati wenzangu, naomba kukushukuru wewe binafsi, kwanza, kwa kunipa fursa ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu. Nawashukuru Naibu Spika na Katibu wa Bunge, kwa kuiwezesha Kamati hii kufanya kazi ya kuchambua Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, naomba niwashukuru Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii, pamoja na Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa michango yao katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati. Ninapenda kuwashukuru pia Mheshimiwa Mustapha H. Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi, Naibu Mawaziri ; Mheshimiwa Jeremiah Solomon Sumari na Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Katibu Mkuu na Wataalam waliotusaidia sana katika kuuchambua Mpango huu. Kamati inawashukuru sana na kuwatakia mafanikio makubwa zaidi katika kazi za ujenzi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa namna ya pekee, napenda kumshukuru Ndugu Anselm Mrema na Ndugu Lawrence Robert Makigi, kwa kazi nzito ya kuihudumia Kamati hii, ikiwa ni pamoja na kuandaa maoni ya mpango huu kwa wakati unaotakiwa.

Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI): Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kuendelea na shughuli zetu za kujenga taifa leo hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi kwa mujibu wa Kanuni ya 86(8), Toleo la Mwaka 2007 na kwa niaba ya Msemaji Mkuu Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Fedha na Uchumi, kuwasilisha maoni ya Kambi ya

Upinzani kuhusu Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2009/2010 na kipindi 2011/2012 na hali ya uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapenda kutoa pongezi na kutambua mchango wako, pamoja na Katibu wa Bunge, kwa kuwezesha na kutoa mwongozo jinsi ya kutekeleza Kanuni ya 94 ya Kanuni zetu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, inayotaka ushiriki wa Bunge katika kuangalia na kuchambua mwongozo wa mpango wa Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, mtikisiko wa uchumi utapelekea ukuaji wa uchumi kuporomoka. Sekta za Utalii; Kilimo cha Mazao ya Biashara na Kilimo cha Maua, tayari imekwisha pata madhara haya. Kwa muono wa Kambi ya Upinzani, kufuatia ukokotoaji wa takwimu za ukuaji wa uchumi, tunaona kuwa ukuaji wa uchumi utapungua na kufikia kwa 6% tu. Taarifa ya nchi ya *Economist Intelligent Unit* ya mwezi Januari, 2009 inaonyesha kuwa, mwaka 2009 uchumi wa Tanzania utakua kwa 5.7% tu, badala ya 7% kama Serikali inavyoeleza

Mheshimiwa Spika, mfumko wa bei wa 13.5%, hiki ni kiwango kikubwa sana na kinapunguza hali ya maisha ya Watanzania *(living standards).* Ilitarajiwa kuwa, kushuka kwa bei za vyakula kutapunguza mfumko wa bei, lakini taarifa za hivi karibuni za baa la njaa, zinaongeza wasiwasi wa mfumko wa bei na hivyo hili kutuzidishia Kambi ya Upinzani wasiwasi kuwa mfumko wa bei waweza kufikia 20% na kuleta machafuko ya kijamii katika nchi *(social unrest).*

Mheshimiwa Spika, njia pekee na ya haraka ambayo Kambi inashauri ni kuongeza uzalishaji wa chakula, kwa mazao yale yanayotumia muda mfupi hadi kuvunwa na mbegu za mazao hayo zipo. Pili, kutambua maeneo yenye chakula kingi na kuhakikisha chakula kinafika maeneo yenye upungufu wa chakula.

Ripoti ya Hali ya Umaskini, Toleo la Mwaka 2007, inayotolewa na Wizara ya Fedha na Uchumi, inaeleza wazi kuwa malengo ya MKUKUTA na yale ya Ilani ya CCM, kupunguza umaskini wa kipato hadi kufikia 19% hayatafikiwa 2010. Hivyo, kuendelea kuweka mipango ya nchi kulingana na malengo ya MKUKUTA na Ilani ya CCM ni kupoteza fedha za walipa kodi bure. *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani ilitegemea kuwa, Serikali ingefuata ushauri uliotolewa katika taarifa hiyo na hivyo basi, mpango na mfumo wa bajeti ungejikita katika ushauri uliotolewa na taarifa hiyo, kwa kubadilisha mwelekeo wa vipaumbele na mbinu za kufikia malengo mapya. Lakini Serikali imeendelea na malengo yale yale ya MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, Sera za Uchumi, hazijatuwezesha tufikie malengo ya bajeti yetu ya mwaka 2008/2009, ambapo sasa tumebakiza miezi minne kipindi kimalizike. Japokuwa pamoja na mambo mengine, hali hii imechangiwa na hali halisi ya kuanguka kwa uchumi wa Dunia. Pamoja na sababu nyingine, ongezeko la mfumko wa bei wa hadi asilimia 13.5 mwezi Disemba, 2008, siyo tu ilichangiwa na ongezeko la bei ya mafuta,

lakini pia ni kutokana na uzalishaji wa chakula. Ukweli ni kuwa, hazikuwekwa juhudi za makusudi za kuzalisha chakula cha kutosha ili bei ya chakula ipungue.

Mheshimiwa Spika, urari wa biashara ya bidhaa za nje, unatisha na unaweza kupelekea nchi yetu kuathirika vibaya na mtikisiko wa uchumi duniani, kwani Tanzania ni moja ya nchi zenye urari mkubwa wa biashara ya nje unaochangia asilimia 13 ya Pato la Taifa *(13% of GDP)* na hivyo kuwa *high risk country*. Mpango wa bajeti unapaswa kuelekeza rasilimali kwenye uzalishaji na mauzo nje ili kusaidia kupunguza kwa hali ya urari wa biashara

.

Mheshimiwa Spika, wakati wa Hotuba ya Bajeti ya Mwaka 2008/2009 na Hotuba ya Rais Bungeni mwezi wa Agosti, Watanzania walielezwa kuwa, uchumi wetu unakua vizuri kwa wastani wa asilimia 7 na kwa hiyo maisha ya Watanzania yanaboreka mwaka hadi mwaka. Hata hivyo, hali halisi ya wananchi wengi inazidi kuwa mbaya. Uchunguzi wa Bajeti za Kaya (UBK) wa mwaka 2007 *(2007 Household Budget Survey)*, unaonyesha kwamba, umaskini umepungua kidogo sana toka asilimia 35.7 mwaka 2001 mpaka asilimia 33.3 mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa idadi ya Watanzania inaongezeka kwa asilimia 2.6 kila mwaka, idadi ya watu maskini imeongezeka toka watu milioni 11.7 mwaka 2001 na kufikia watu milioni 12.7 mwaka 2007. Izingatiwe kuwa kigezo kilichotumiwa na UBK 2007 cha mtu mzima kutohesabiwa kuwa siyo maskini ni kutumia shilingi 641 au zaidi kwa siku akiwa Dar es Salaam, shilingi 532 au zaidi kwa siku ukiwa katika miji mingine na shilingi 469 au zaidi kwa siku ukiwa vijijini. Ni wazi kuwa, kigezo hiki ni cha chini mno na bado idadi ya watu maskini imeongezeka. Kiwango cha ukuaji wa uchumi hakipelekei kupungua kwa umaskini, kwa sababu uchumi wa vijijini haukui *(rural economy).*

Mheshimiwa Spika, sasa yatupasa kuweka mpango wa kukuza uchumi vijijini na kuunganisha uchumi wa vijijini na ule wa mijini ili kushusha faida za ukuaji wa uchumi kwa jamii nzima ya Watanzania na si sehemu tu ya jamii ya Watanzania. Mpango wa Bajeti unapaswa kuonesha waziwazi juhudi za kusambazaa faida za ukuaji wa uchumi kwa wananchi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, malengo makuu ya Bajeti ya 2008/2009 yalikuwa ni mawili; Kuongeza mapato ya ndani; na kupunguza utegemezi wa wafadhili.

Hali ngumu ya uchumi, inapelekea kuvuruga vyanzo vya mapato vya Serikali na hivyo kuvuruga mipango ya Bajeti. Serikali inapaswa kuangalia vyanzo vingine vya mapato ili kuikabili hali ya uchumi. Kambi ya Upinzani, inapendekeza uuzwaji wa hisa za Serikali kwa mashirika yafuatayo ili kujihami na upungufu wa ukusanyaji mapato ya ndani; *Celtel* (hisa 25%), kadirio la Sh. 120bn; *NBC* (hisa 20%), kadirio la Sh.80bn; *BP* Tanzania (hisa 25%); *Kilombero Sugar* (hisa 15%); *Mbeya Cement* (hisa 15%); *TDFL;* na *Tanzania Standard Newspaper*.

Mheshimiwa Spika, uuzwaji wa hisa za Serikali kwenye soko la mitaji ukipangwa vizuri, utawawezesha Watanzania kumiliki uchumi kwa kutumia akiba zao na hivyo,

Serikali kupata fedha za kuziba pengo la upungufu wa mapato. Uuzwaji huu wa hisa utapelekea Serikali kuimarisha Utawala Bora kwa mashirika haya na kuongeza uwazi kwa masharti ya kuorodhesha hisa kwenye soko la mitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali, kuweka mkazo wa usimamizi katika uvuvi wa Bahari Kuu, ili kuhakikisha Sekta hii ya Maliasili inaiongezea mapato Serikali. Hivi majuzi, vyombo vya habari vimemnukuu Waziri wa Mifugo na Uvuvi akikiri kwamba, sekta hii ya uvuvi wa Bahari Kuu inaweza kuiongezea Serikali mapato kuliko yale yanayopatikana kutoka katika Sekta ya Madini.

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuandaa mikakati thabiti, ikiwa pamoja na kuwa na vifaa vya kisasa na vyenye uwezo, ambavyo vitaweza kukabiliana na maharamia wanaotoka nje ya nchi na kuja kuiba maliasili yetu. Mapato kutoka katika sekta hii, yanaweza pia kuongezeka kwa kuongeza ada za leseni za uvuvi na kutoza mrabaha wa mauzo ya samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iongeze mtaji kwa *TANESCO* na kupitia upya mikataba ya makampuni yanayoiuzia *TANESCO* umeme, ikiwa ni pamoja na kuondoa *capacity charges*. Aidha, kuanzisha *Grid* mpya ya Magharibi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuigawa *TPDC* kuwa Mamlaka na Kampuni. Mamlaka mpya itakayokuwa ya mafuta na gesi, itakuwa ni ya Muungano na itafanya kazi ya kugawa na kusimamia mikataba ya uchimbaji. Kampuni ya mafuta na gesi ambayo itawekeza kwenye sekta kibiashara, kwa kuchukua hisa za Serikali *BP* na *TIPER* na kwingine popote.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa *TPDC* inaendeshwa na Ruzuku ya Serikali, wakati Kampuni hiyo ina uwezo kabisa wa kujiendesha kibiashara na lengo letu ni kulifanya lijiendeshe na kuipunguzia mzigo Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na Ripoti ya Serikali inayohusu hali ya umaskini ya mwezi Disemba, 2007, imeainisha pamoja na maeneo mengine, maeneo mawili muhimu ambayo yangesaidia kukuza uchumi: Usafirishaji kutokana na jiografia ya Tanzania, ambayo imepakana na nchi ambazo hazina bandari *(landlocked countries)*, kama Zambia, Rwanda, Burundi, Kongo na Malawi. Kuwepo kwa huduma za usafiri kama vile reli na barabara zinazounganishwa na Bandari, zingesaidia sana kukua kwa uchumi wetu na hata kuongeza ajira kwa watu wetu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuifanya Sekta ya Usafirishaji kama sekta mkakati katika kukuza uchumi kwa kuimarisha mashirika kama *TPA, TRL, ATCL* na *TAA*. Aidha, ichague barabara chochezi ambazo ni kiunganishi kati ya hayo mashirika tajwa hapo juu na hivyo kuharakisha ujenzi wake. Vilevile ichague viwanja vya ndege chochezi ili kwenda sambamba na mashirika na barabara tajwa.

Madini ni mojawapo ya sekta ambayo inatakiwa ibadilishe hali ya uchumi wa nchi yetu, kwa kuwa sekta kiongozi katika kuliingizia Taifa mapato. Tume ya Jaji Bomani, imetoa mapendekezo ya kuiwezesha Serikali kupata mapato zaidi kutoka Sekta ya Madini. Nilieleza katika Bajeti ya 2008/2009 kuwa, ukaguzi uliofanywa na Kampuni ya *Alex Stewart*, kwa kipindi cha miaka mitatu, Serikali imepoteza shillingi 1.3 trilioni. Hii imetokana na Serikali kutokuwa makini katika kufuatilia nyaraka halali zinazotumiwa na makampuni ya kuchimba madini. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha mapato yake yanaongezeka toka sekta hii?

Mheshimiwa Spika, tatizo la Tanzania ni ukosefu wa mikopo na riba za juu. Mpaka hivi sasa mabenki yanatoa mikopo midogo kuliko akiba *(deposits*), wanazokusanya toka kwa wateja wao. Kwa mujibu wa taarifa ya Gavana aliyoitoa kwa Wabunge hivi karibuni, uwiano wa mikopo kwa amana ni asilimia 68 ukilinganisha na asilimia 80, ambayo ni kikomo. Kwa mfano, hadi kufikia Juni 30, 2008, thamani ya mikopo ya *NBC* ilikuwa asilimia 63 ya akiba zilizowekwa kwa wateja. Kwa uchumi unaoendelea, mikopo huwa mikubwa zaidi kuliko akiba zilizowekwa na kwa hiyo kuzifanya benki kuwa kichocheo cha uchumi na biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yetu ya mapato na matumizi ya mwaka ya Wizara ya Fedha, tuliishauri Serikali kuundwa kwa Tume ya Mipango, itakayoshughulikia mipango ya Serikali ya muda wa kati na muda mrefu. Hali iliyopo sasa ni kwamba, Wizara ya Fedha na Uchumi, inashughulikia matatizo ya kila siku ya bajeti kiuchumi, bila kuwa makini katika kubuni mipango thabiti ya utekelezaji wa bajeti hizo. Kambi ya Upinzani inaona huu ni upungufu na ni udhaifu mkubwa sana, unaotakiwa kurekebishwa ili Tanzania iweze kujitosheleza katika yale tunayopanga na kuyatengea fedha. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuwa na Tume ya Mipango inayoonekana na kutoa matarajio ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mashirika mengi ya Umma yanatumia fedha za Serikali kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali ni vyema basi, Serikali ikaanzisha Kitengo Maalum kwa ajili ya kufanya *Investment Appraisal* kwa maaana ya kuiwezesha Serikali kuweka vipaumbele sahihi katika ugawaji wa fedha katika miradi ile tu inayoonekana ina faida kwa wananchi; kuliko ilivyo sasa, miradi inapewa fedha tu bila kuzingatia wananchi wanafaidika vipi katika miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa utendaji wa mashirika ya umma, hautoi fursa nzuri kupima ufanisi wa mashirika hayo. Ni vyema basi, Bodi za Mashirika ya Umma zikaingia mikataba ya kiutendaji na menejimenti za mashirika hayo, kwa viwango vitakavyokubalika ili hatimaye kupima ufanisi wa kiutendaji na tija itakayopatikana katika mashirika hayo. Tanzania inatumia karibu zaidi ya asilimia 80 katika kufanya manunuzi ndani na nje. Kwa kuweka kumbukumbu sawa, katiba bajeti za Kambi ya Upinzani kwa miaka ya nyuma kuanzia bajeti ya mwaka 2004/2005, tumekuwa tukiishauri Serikali kuanzisha mfumo wa ununuzi kwa kutumia njia ya Mtandao *(e-procurement).*

Mheshimiwa Spika, inaonyesha kuwa, Serikali bado haijaelewa ni kwa jinsi gani utaratibu huu utaokoa ubadhirifu na ufisadi wa hali juu, unaotokea katika sekta nzima ya manunuzi yanayofanywa na Serikali. Kambi ya Upinzani, inaishauri Serikali ikubali kuelewa kutumia utaratibu huu wa *e-Procurement*. Wasiwasi wa kuwa wafanyabiashara wetu bado hawajaweza kutumia mtandao ni woga ambao unazidi kutoa mianya ya Serikali kuendelea kupoteza fedha za walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa uchumi wetu unachangiwa na sekta kadhaa, sekta ya kilimo ikiwa haiongozi ila ni muhimu sana. Kwa hali ya kawaida na kufuatana na nadharia za uchumi ni kwamba, kadiri uchumi unavyokua, Sekta ya Kilimo inatakiwa kupungua na kutoa mwanya kwa sekta nyingine za uchumi kama viwanda kushika kasi, lakini kwa Tanzania ni tofauti.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya Serikali yalenge katika kuzindua mapinduzi ya kilimo na hasa kuongeza uzalishaji wa chakula ili tuondokane na aibu na adha ya baa la njaa. Tujifunze kwa wenzetu wa Malawi, namna ruzuku ya mbolea ilivyoongeza uzalishaji wa mahindi. Ni muhimu mbolea na pembejeo za kilimo, ziwafikie wakulima kwa wakati. Mbolea husika iwe imefanyiwa majaribio. Wakulima wa Mbeya waliotumia mbolea ya minjingu, walipata hasara kwani mimea yao ilikauka. Bajeti ya Sekta ya Kilimo iongezwe na isiwe chini ya angalau asilimia 12 ya matumizi yote ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inaona katika kilimo kwa kulingana na hali ya uchumi ilivyo kwa sasa duniani; ni muhimu sana kuwekeza katika kilimo hasa cha chakula kama vile mahindi, mpunga, maharage, jamii ya kunde na mbegu za mafuta, kukidhi mahitaji ya ndani na kuuza masoko ya nje hasa nchi za jirani hususan Congo. Hili liende sambamba na upembuzi yakinifu wa Serikali ni mikoa ipi yenye *Potential* ya kuwa ghala la Taifa.

Mheshimiwa Spika, uchumi wa Tanzania na hali halisi ya uchumi wa dunia, mfumo wa fedha na mabenki ya Tanzania bado ni mchanga. Sekta ya Fedha ya Tanzania, kwa ujumla wake haikununua hisa, karadha na hatifungani zinazohusiana na mgogoro wa kifedha wa Marekani. Hata hivyo, Sekta ya Fedha inaweza kuathirika ikiwa benki mama ya benki tanzu za Tanzania, imeathirika na mgogoro huu wa fedha. *NBC* ndiyo benki kubwa kuliko zote nchini, kwa vigezo vya uwekaji wa akiba na amana, utoaji wa mikopo na rasilimali.

Mheshimiwa Spika, *NBC* ilibinafsishwa kwa *ABSA* ya Afrika ya Kusini. *ABSA* imenunuliwa na *Barclays. Barclays* ya Uingereza imekumbwa na matatizo ya Sekta ya Fedha na ilibidi itafute wawekezaji toka Abudhabi na Dubai wawekeze paundi bilioni saba kuinusuru isiombe msaada kutoka Serikali ya Uingereza. Mpaka hivi sasa, haujafahamika mpango wa *Barclays* kuunganisha shughuli za kibenki kati ya *Barclays* Tanzania na *NBC*. Je, Serikali imejihami vipi kuzuia matatizo ya *Barclays* Uingereza yasiathiri utendaji wa Barclays Tanzania na *NBC*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, City Bank ina tawi moja nchini pote. Wateja wake ni makampuni makubwa na mashirika ya misaada. City Bank imepata hasara kubwa katika

shughuli zake Marekani, hasa katika amana za mikopo ya nyumba na imebidi isaidiwe na Serikali zaidi ya dola bilioni 300 ya mikopo na dhamana (*guarantee*). Hivi sasa imo katika mchakato wa kuachisha wafanyakazi 50,000 na huenda ikafunga matawi yake katika nchi nyingi ikiwemo Tanzania. Je? Serikali imejiandaa kukabiliana na tukio hilo?

Mheshimiwa Spika, ni wakati muafaka kwa serikali kupitia upya sera ya mabenki. Sehemu kubwa ya huduma za benki, zinaendeshwa na mabenki ya nje. Mabenki haya yanapoyumba kwenye nchi zao, yanaweza kuathiri utendaji wake Tanzania. Taifa letu litafakari umuhimu wa kuwa na mabenki ya taifa ya Watanzania katika sekta binafsi au ambayo Serikali ni hisa na sauti katika uendeshaji wake.

Mheshimiwa Spika, tulipata hasara kubwa, zaidi ya dola milioni 30 wakati Benki ya Meridan Biao ilipofilisika Zambia na katika nchi za Afrika Magharibi. Meridian Biao Tanzania ilibidi ifungwe. Vilevile Greenland Bank ilipopata matatizo katika makao makuu yake Uganda, Ofisi na matawi yake Tanzania yalifungwa. Utandawazi katika Sekta ya Fedha na Mabenki una athari zake. Ni vizuri tukazichambua vizuri hizo na kuweka mkakati wa kuiimarisha Sekta ya Fedha na Mabenki, itakayowasaidia wajasiriamali wa Tanzania wakiwemo wadogo na wa kati, kuwekeza katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji wa vitega uchumi kutoka nchi za magharibi utapungua, kwa sababu ya matatizo ya upatikanaji wa mikopo na kupungua kwa ukubwa wa soko na bei za bidhaa. Uchumi wetu unategemea misaada ya nje. Mgogoro wa uchumi wa nchi tajiri, utapunguza misaada kutoka nje na hasa ikiwa mapambano dhidi ya ufisadi hayatafanikiwa kuwashtaki sangara wa rushwa na kufanikisha kesi hizo mahakamani, kwa watuhumiwa kupatikana na hatia na kuhukumiwa adhabu kali.

Serikali za nchi tajiri zitatumia kisingizio cha rushwa kupunguza misaada. Ni vizuri kuelewa kuwa, kutakuwa na ushindani mkubwa zaidi katika kupata misaada, hasa kutoka nchi ambazo hazina malengo ya kibeberu kama vile nchi za *Nordic*.

Mheshimiwa Spika, ikiwa Tanzania itaonyesha kuwa inatumia vizuri misaada inayopewa itaweza kulinda kiwango cha misaada hiyo. Hata hivyo, suala la kupambana na saratani ya rushwa si la kuwaridhisha wafadhili bali ni la kuleta haki katika nchi na la kutumia vizuri mapato, raslimali na mali ya asili ya taifa letu kwa manufaa ya wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bunge litakaa kama kamati ya Mipango, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa, mjadala huu utasaidia kurutubisha mpango ulioletwa na Serikali na hivyo sote kwa pamoja, tujenge Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyatoa hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Fatma Fereji, umeiwakilisha Kambi yako vizuri sana.

Waheshimiwa Wabunge, orodha niliyonayo ni ya wachangiaji 35, lakini ni dhahiri kwamba, isingefaa twende hivyo, kwa sababu tunakusudia kumaliza shughuli zetu keshokutwa jioni na bado kuna taarifa za utekelezaji, ambazo zitatolewa na Serikali na ziliahidiwa. Kwa hiyo, nimepanga mjadala huu tuweze kuufunga kesho mchana, sio siku mbili kamili ni kama siku moja na nusu. Nadhani inatosha na ni muhimu sana tuweze kupata tathmini ya yale tuliyoamua zamani, kuliko tuwe tunapendekeza mapya tu wakati wote. Kwa hiyo, nimetenga muda kuanzia saa kumi na moja hadi saa kumi na mbili jioni keshokutwa, kupokea taarifa zile za *Richmond, TRL* na kadhalika.

Baada ya kusema hayo, nitaanza na wachangiaji watatu. Orodha yangu ni kama ifuatavyo, kwa hawa wa mwanzo; Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Dkt. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Omar Kwaangw' na Mheshimiwa Abdulkarim Shah. Kwa hiyo, sasa tuanze na Mheshimiwa Devota Likokola, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Wilbrod Slaa, wakati huo Mheshimiwa Omar Kwaangw' ajiandae. Mheshimiwa Likokola.

MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuhusu Mpango wa Bajeti.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri na Wataalam wetu kwa kutuletea muongozo huu, ambao umeangalia vipaumbele mbalimbali ambavyo vitaweza kutusaidia katika kukuza uchumi wetu na kuleta maendeleo yetu. Pamoja na kuwashukuru wao, tunalishukuru sana Bunge hili, kwa kufanya Wabunge tuweze kushiriki katika kuchangia mwongozo huu. Hii itasaidia umiliki wa mwongozo huu na umiliki wa bajeti utakuwa ni umiliki wa wajumbe wote na hivyo sote kwa pamoja, tutashirikiana kujenga Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia katika maeneo ya vipaumbele, ambavyo tunategemea tuanze navyo. Naungana na Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri na Wataalamu wetu, kwa kutuletea kipaumbele cha kwanza katika Sekta ya Miundombinu. Kama tutaiimarisha miundombinu yetu, maana yake ni kwamba, uzalishaji wetu utakuwa na tija. Sasa hivi wananchi wanahangaika katika kuzalisha, lakini bado hakuna tija; barabara ni mbaya, reli hakuna, kwa hiyo ni tatizo kubwa sana. Utakuta katika uzalishaji, hata kupeleka pembejeo bado gharama zinakuwa ni kubwa kutokana na miundombinu hafifu.

Mheshimiwa Spika, kuna suala zima la miundombinu katika Ukanda wa Kusini. Kuna suala la *Mtwara Corridor,* hii sasa imekuwa ni tatizo. Ukanda wa Kusini, bado haujajifungua kabisa katika masuala ya miundombinu. Barabara ya kutoka Tunduru mpaka Songea, ina hali mbaya, hata wakulima wa Tunduru wakizalisha bado hawawezi kusafirisha mazao yao, hawawezi kupata bidhaa kutoka Songea, kwa sababu barabara ni mbaya na bei zinakuwa ni kubwa kupita kiasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara hii inaendelea, ikifika Songea inatakiwa iende Mbamba Bay. Ninaomba katika mwongozo huu, tutakapotengeneza bajeti yetu, tuweke kipaumbele katika suala zima la *Mtwara Corridor*. Kumekuwa na hadithi nyingi sana, mara *ADB* wametoa pesa, mara *Kuwait Fund,* mara *MCC,* lakini hakuna utekelezaji. Wananchi wa kule hawaelewi haya maneno yote, wanachoelewa wao ni kama wataiona barabara ya lami imepita kutoka Tunduru mpaka *Mbamba Bay,* hapo watayaelewa haya maneno *Kuwait Fund, MCC* na kadhalika. Ninaomba sana tutakapotoa bajeti yetu, tuzingatie suala la *Mtwara Corridor. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie changamoto ya miundombinu katika sekta ya umeme, bado Mkoa wa Ruvuma upo kwenye giza na sio Mkoa wa Ruvuma tu, tunasikia Mkoa wa Kigoma na Mikoa mingine. Kwa hiyo, tunaomba mwongozo huu pamoja na kwamba, umetaja maeneo ya kuwekeza katika suala zima la umeme, katika utekelezaji haya yatekelezwe ili tuweze kuleta maendeleo Tanzania. Ninashukuru sana Mheshimiwa Waziri na Wataalamu wake, wamekuwa ni wasikivu wakubwa mno; michango mingi ambayo Kamati ya Fedha na Uchumi tumeitoa, wameizingatia katika mwongozo huu. Suala la kilimo limepewa kipaumbele na tunashukuru sana. Wataalamu wetu, pamoja na Wizara hii, wamemuunga mkono Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye alitumia muda mwingi sana kufanya mkutano na kongamano kubwa la kuleta mageuzi ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, alikaa na Wajumbe kutoka Mikoa sita Tanzania, ikiwemo Mkoa wa Rukwa, Iringa, Mbeya, Morogoro, Kigoma na Ruvuma, kuzungumzia Mapinduzi ya Kilimo.

Kama kilimo kitajikita zaidi katika mikoa hii, matokeo yataonekana haraka kwa sababu mikoa hii ina hali ya hewa nzuri na kwa maana hiyo, tunaomba tusisitize suala zima la pembejeo. Pembejeo ziwahi katika maeneo husika na ziwafikie wananchi mapema. Mwaka huu wananchi wana masikitiko; watu wa Ruvuma wamehangaika sana na suala zima la pembejeo, zimechelewa kufika. Hata hivyo, Serikali imeanzisha utaratibu wa pembejeo, kama elimu haitatolewa kwa wananchi wakelewa vizuri ule utaratibu, hapatakuwa na matokeo mazuri katika kilimo. Naiomba Serikali itoe elimu na itoe hamasa ili wananchi waelewe utaratibu mzima wa upatikanaji wa pembejeo na matumizi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninaomba tuzungumzie suala zima la Benki ya Kilimo; ninaipongeza Serikali, ikianzisha Benki ya Kilimo itakuwa ni ukombozi wa Taifa hili. Asilimia kubwa sana ya wananchi wa taifa hili, wanategemea kilimo na kilimo chochote kinahitaji pesa na kama hakuna benki ya kilimo maana yake ni kwamba, wakulima hawawezi kupata pesa za kilimo. Ninashukuru sana, kwa vile Wizara imetamka kutakuwa na Benki ya Kilimo, tunategemea tutaiona hiyo Benki na itafanya kazi na wakulima watafaidika sana na hivyo tija katika kilimo itakuwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, katika suala zima la uzalishaji, pamoja na kwamba, tumezungumzia masuala ya kilimo, lakini katika mwongozo huu kuna vipaumbele vya viwanda. Kama patakuwa na kilimo na viwanda, maana yake ni kwamba, mazao ya

kilimo yataweza kusindikwa. Mazao yakisindikwa, tija itakuwa kubwa. Ninaomba Wizara iangalie, katika kila mkoa kuna zao ambalo wanazalisha na linahitaji kusindikwa. Tuna matatizo makubwa ya Kiwanda cha Tumbaku Songea na katika Mkoa wa Ruvuma, tumbaku inazalishwa pale inakwenda kusindikwa Morogoro. Wananchi wanasikitika sana kwa kitendo hicho. Wangependa tumbaku ile isindikwe palepale; kwanza, kile kiwanda kinazidi kuharibika ni lazima Serikali ichukue hatua ya haraka ili kuona kiwanda kile hakiendelei kuharibika lakini pia kinaleta ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vijana wengi wa Manispaa ya Songea hawana ajira, kwa sababu hakuna viwanda. Tunazalisha mahindi kwa wingi, lakini hakuna hata kiwanda cha kusaga unga. Ninaiomba Serikali itusaidie, pamoja na kiwanda cha tumbaku, lakini pia tunahitaji viwanda vingine. Ninaiomba Serikali isije ikasahau, tuna mpango wa *EPZ* katika Mkoa wa Ruvuma maeneo ya Ruiko. Kama kweli Serikali imeweka ile *EPZ* itakuwa ni ukombozi mkubwa sana kwa wakazi wa Mkoa wa Ruvuma, kwa sababu bidhaa nyingi zitazalishwa na hivyo zitaweza kuuzwa na tija itakuwa kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie sekta ya watu binafsi; tuna tatizo zima la utekelezaji wa maazimio yetu hapa. Mambo mengi tunayoyapanga kama Serikali ni mazuri sana, lakini yanakosa watekelezaji. Watekelezaji wakubwa wa mipango hii ya Serikali, hususan mipango ya uzalishaji ni sekta binafsi. Ipo haja ya Serikali kuiboresha sekta binafsi kwa kuwapa elimu, kuwasaidia na kukaa nao karibu ili kuangalia mipango yao na kuwapa msaada. Ukiiangalia sekta binafsi, bado haijaweza kuzalisha kwa makini sana, kwa sababu bado tuna masuala mengi yanayozuwia. Kwanza, tumeambiwa kuna ukiritimba mkubwa Serikalini na hivyo, sekta binafsi haiwezi ikachangamka na ikafanya biashara vizuri.

Mheshimiwa Spika, nimefurahi Mheshimiwa Waziri, ameleta hapa suala la kuboresha Sekta ya Fedha. Ukiizungumzia Sekta ya Fedha, ndiyo kiini hasa cha maendeleo haya yote. Watu wanahitaji mitaji waweze kuzalisha, mikopo yote iliyotolewa imeenda kwa wafanyabiashara kwa maana ya wachuuzi, haikwenda kwa wazalishaji, maana yake uchumi unazidi kudidimia. Yale mabilioni ya Kikwete, mengi yameenda Dubai, watu wameenda kununua bidhaa Dubai na kutuuzia hapa, hayajaenda vijijini katika uzalishaji. Tunaomba safari hii, Sekta ya Fedha ipanue miundombinu yake katika ngazi ya chini, katika maeneo ya Vijiji, katika maeneo ya Wilaya, hakuna Mabenki Vijijini, wala hakuna Mabenki katika Wilaya; kwa nini sasa kama tutatoa mikopo itazidi kukaa mijini na watu wa vijijini watazidi kuhangaika.

Mheshimiwa Spika, ninaomba wananchi wasaidiwe sana katika suala zima la kuoanisha maendeleo katika Ukanda wa Kusini. Historia inajionesha na hakuna asiyefahamu, mara nyingi Ukanda wa Kusini unakuwa na maendeleo hafifu. Ninaomba Tanzania, iiangalie Mikoa ya Kusini ili kuleta uwiano wa maendeleo. Mpango huu uweze kutoa jibu kwa Watanzania wote. Kama Mikoa ya Kusini haitaangaliwa, kutakuwa na malalamiko makubwa ya Wananchi wa Mikoa ya Kusini. Ninaomba mwongozo huu baada ya kuutekeleza na kutengeneza Bajeti yetu, uweze pia kutupa picha ambayo itaonesha umetengeneza bajeti ambayo imewasaidia Watanzania wote; wanawake na wanaume. Wanawake ni wazalishaji wakubwa sana na inapokuja kwenye bajeti

tunatengeneza, lakini safari hii tunamwomba Mheshimiwa Waziri, tungekuwa na *Gender Budget Statement*, ambayo itaonesha katika bajeti hii wanawake wamenufaika vipi. Tusije tukawa sisi tunashangilia tu uchumi na hatuumiliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi, lakini mimi binafsi ninawapongeza sana Wataalamu wetu; wametuletea mwongozo mzuri na tukiutekeleza sote kwa pamoja, hususan tukihamasisha upatikanaji wa mapato, tunaweza kuutekeleza vizuri na maendeleo yatakuja Tanzania. Nakushukuru kwa kunipa nafasi ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Devota Likokola. Wakati tukiendelea ni wajibu wangu nikiwa hapa kuainisha mambo muhimu, ambayo yanatokea humu ndani ya Ukumbi. Nilikuwa napenda mtambue kwamba, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, hivi sasa ndio anamwakilisha Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika kuongoza Shughuli za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dkt. Wilbrod Slaa, nadhani atakayefuata ni Mheshimiwa Omar Kwaangw' na itakuwa ni jioni tena.

MHE. DKT. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninapenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Kaimu Waziri Mkuu humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kusema kwamba, nashukuru sana mpango huu umewasilishwa na ni imani yangu kwamba, kama ilivyo *speed* na *standard*, ofisi yako itaendelea kusimamia zoezi hili, kwa miaka ijayo liwe bora zaidi ili tunapojadili tuweze kuwa na kitu ambacho ni *concrete*. Leo hata tukijadili hatimaye tukafanya maamuzi, baadaye wakati wa Bajeti tukaambiwa Wabunge mlipitisha, hatuna kitu tunachoweza kusema. Tufuate wenzetu wanaofanya *Budget Circle*, ambayo ndio hatua hii wanafanya nini ili kitu hiki kiwe kwa manufaa ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitajikita kwenye maeneo mawili kwa ajili ya muda na ili iwe na tija zaidi. Kwanza ni dhana ya awali kwamba, Tanzania hatuna sababu ya kuomba chakula nje ya nchi. Tunapaswa sisi kuzalisha chakula na kuwa nchi inayouza na kupeleka chakula nje. Chakula kinapaswa kutosha kwa nchi yetu na kuzalishwa kwa ajili ya kupelekwa kwa wengine. Tuna sababu za kutosha; tuna ardhi kubwa na mabonde makubwa sana, kwa hiyo, kinachotakiwa ni mipango.

Kwa hiyo, napenda nianzie kwenye ukurasa wa 14, anapozungumzia kwenye kilimo na umwagiliaji. Sasa nikishatoa hilo, nieleze ni nini kinafanyika na ni nini kinatofautiana kati ya tunayoyazungumza hapa Bungeni na tunachokitenda katika utendaji wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano wa suala dogo sana la mbegu, pamoja na mbolea. Kwa muda mrefu, tumezungumzia kwamba nchi yetu imeweka fedha nyingi kwenye mbegu na mbolea. Mwaka 2008, tulipata matumaini makubwa sana kwamba, labda sasa tutafanikiwa kuwa na chakula cha kutosha, kutokana na kuwekeza kwetu kwenye mbegu

na mbolea. Fedha tulizotenga tunazijua na juzi Bunge lako limeidhinisha pia fedha kwa ajili ya kwenda kwenye pembejeo ikiwemo mbegu.

Mheshimiwa Spika, sasa suala la kuandika ni kitu kimoja na suala la kutenda ni kitu kingine. Ningependa tunapozungumzia mipango, basi tuwe na mipango ambayo katika hali ya utendaji, inawiana na kile tunachokiandika. Natoa mfano, mwaka 2008 baada ya Bajeti, kwenye mwezi Novemba, tuliletewa *circular* nchi nzima; sina hakika kama Wabunge wanajua, wale tuliokuwa tunapita vijijini tulikumbana nayo. Tuliletewa *circular*, mimi katika Wilaya yangu imefika tarehe 6 Novemba, tukitakiwa tarehe 7 tupeleke majina ya wakulima watakaopewa mbegu na mbolea. Hawa wakulima wawe wamepitiwa kwanza na Kamati ya Serikali ya Kijiji au na Halmashauri ya Kijiji na baadaye Mkutano Mkuu. Ni dhahiri kuwa, barua kufika tarehe 6, tarehe 7 majina yasingeweza kurudishwa. Kwanza, kuna utata wa kutosha hapo. Sasa hili ni suala la je, tunachoamua na mipango yetu inaenda sawa au vipi?

Mheshimiwa Spika, la pili ni huo mchakato umeenda; hatukwenda tena kutekeleza jinsi ilivyopangwa. Kwa hiyo, wananchi hawakwenda kupiga kura ni nani hasa anahitaji. Mbegu ile na mbolea ile ilitakiwa ipatikane na wale wa kwenye kijiji ambao hawana uwezo kabisa wa kununua mbegu au pembejeo tuwasaidie. Kwa kila Kijiji, tulilenga idadi fulani ambayo ilikatwa tu; kwamba, sasa tunataka watu kadhaa. Kwa nchi nzima, tunatoa mbegu na mbolea kwa mtu mmoja kwa ekari moja. Kwa hiyo, sasa tuna jumla ya ekari 10,000 na mimi nafikiri hilo katika mpango ni jambo jema sana kwamba, tuna watu 10,000 tuna ekari 10,000 za uhakika, kama zingepata mbegu na mbolea, tungezalisha. Kwa hiyo, nina hakika, kimawazo ni jambo jema, lakini mpango na mawazo yasipooana na utekelezaji ndio tunapata athari, fedha zitapotea.

Ninasema zitapotea kwa sababu mwaka 2008, Mkoa wa Arusha kwa Wilaya ya Karatu tu, tulirudisha Kilimo zaidi ya tani sita ambazo zilitakiwa zitumike na wananchi na hazikutumika, kwa sababu hazikufika kwa wakati. Kwa hiyo, zile kimahesabu ni kwamba, hazipo na wala sizungumzii kwamba zilienda wapi au ni nani alitumia, lakini wananchi waliotakiwa kupata hawakuzipata.

Mheshimiwa Spika, tatizo ni nini? Tatizo la msingi ambalo bado naliona pale ni kwamba, leo hii tunapozungumza, nimecheki kwa Wilaya yangu ya Karatu, Wilaya ya Hanang na Wilaya ya Babati, ambayo bahati nzuri juzi tu Kamati ya *LAAC*, ilikuwa kule na nikaingia kwa undani sana kufanya tathmini kumetokea nini. Kuna maeneo mengi pia ya Tanzania, nimepigiwa simu kwamba, mbegu na mbolea bado ni tatizo na sasa ni wakati wa kupanda. Cha ajabu zaidi ni kwamba, kilichopelekwa ni mbolea ya kupandia. Sasa unapeleka mbolea ya kupandia, wakati mbegu hakuna; hivi wakati wa kupanda unapopeleka mbolea ya kupandia unaenda kupanda nini?

Mheshimiwa Spika, ni sawa na mama nyumbani anapeleka ugali mezani, lakini anatanguliza mboga ugali haupo. Ingekuwa ni mila ya kwetu Wairaki, huyo mama siku hiyo hiyo angefukuzwa, kwa sababu huwezi kupeleka mboga kabla ya chakula. Sasa unapeleka mbolea, lakini mbegu ya kupanda hakuna na mvua nazo ndio hizo za kuwinda,

hujui siku hizi hata msimu ni lini. Kwa hiyo, unapotaka kupanda kile cha kupanda hakipo, lakini cha kupandia kipo, hilo ni la kwanza. Kwa hiyo, nadhani ninachosema hapa ni kwamba, basi tunapopanga mipango ile iende kwenye utekelezaji pia. Wale Wataalamu wetu tunapoamua kitu, waende kwenye hatua ya utekelezaji ili tupate manufaa ya kile tunachokipanda.

Mheshimiwa Spika, la pili, mimi nilishtushwa kidogo, kwa sababu unapoambiwa kwamba hivi vitu vinapelekwa na tumeshaweka dhana kuwa tunapeleka kuwasaidia wale watu wa chini kabisa, ambao hawana uwezo wa kununua mbolea, hawana uwezo wa kununua mbegu wao wenyewe, lakini unapofika mahali sasa hao hao unaowapelekea unawawekea masharti magumu ya ajabu. Ninatoa mfano; hivi unapofika mahali unamwambia mwananchi ambaye katika eneo labda anajua kabisa ardhi yake haihitaji hata hiyo mbolea, anaponunua ile mifuko miwili ya mbegu ni lazima pia anunue mbolea. Umempa masharti, ukinunua mbegu ni lazima ununue mbolea, ukinunua mbolea ni lazima ununue yale mahindi. Huyu ni mwananchi ambaye hana kitu!

Mheshimiwa Spika, ninalisema hili kwa sababu wananchi wetu tunaowazungumzia tunawajua. Nilipofika mahali nilimwomba Afisa Kilimo, anifanyie mchanganuo wa kinachopelekwa akanifanyia. Huyu mwananchi, kwa heka moja anatakiwa achangie yeye mwenyewe kwenye mfuko wake, laki moja na arobaini na tisa. Huo ni mchanganuo niliopewa na Afisa Kilimo, sina hakika mimi sio Mtaalamu wa Kilimo.

Nilitaka kujua baada ya wananchi kulalamika, hivi mimi ambaye ninaambiwa nasaidiwa, napelekewa ili ninyanyuliwe, sasa natakiwa nitoe laki moja na arobaini na tisa, sijaandaliwa mapema, leo naenda kuitoa wapi? Kwa hiyo, hata ile vocha ninayopewa inapoteza maana, kwa sababu nitashindwa kuikomboa; na kwa sababu ninashindwa kuikomboa, hatimaye ninaiuza kwa wale matajiri ambao ndio walewale. Kwa hiyo, ninataka kusema kwamba, vitu vyetu vipo kinadharia, kwenye karatasi vinaonekana vizuri, lakini hatujaoanisha yale tunayoyapanga na yale ambayo tunataka kuyatenda.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, katika dhana hii ni suala zima la kuangalia kwamba, tunapotoa vitu hivi, kwa mfano, mbolea na mbegu, kuna msimu unaotakiwa kwa mbolea na mbegu. Leo ukinipelekea mimi Wilaya ya Karatu, kwa mfano, Bonde lote la Eyasi, ambalo linajulikana kwanza ni Bonde la umwagiliaji, lina wakati maalumu. Ukishapeleka mbolea wakati ambapo mvua zimeisha, *I mean* kipindi chao cha kupandia mazao kama ni ya chakula kimepita, sasa hiyo mbegu na mbolea unapeleka wapi tena na inaenda kusaidia nini? Kwa hiyo, unapoteza kwa maana ya uchumi, umeharibu hata zile nyenzo ulizopeleka, hazitatumika na yule mwananchi na baadaye sijui wataziuza au wafanye nini, lakini hutapata ile dhana ya mbolea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, *timing* ya vitu tunavyofanya ni lazima vioane. Kwa maana hiyo, labda nataka niisadie Wizara inayohusika, tunapozungumzia wakati wa Bajeti kwamba, Bajeti ile ya jumla inapita labda ni mwisho wa mwezi Juni, tarehe 01 Julai, tunaanza na Bajeti. Basi ni vyema yale mambo yanayokwenda kwa msimu ifikapo

tarehe 01 ya mwezi unaofuata, kwa maana ya Mwaka wa Fedha unapoanza, basi vile vitu navyo vipelekwe ili ndani ya msimu ule tuweze kuwa tumetekeleza yale tunayotakiwa kuyatekeleza. Tusipofanya hivyo, vile vitu vitarudi na vitafungua mianya ya rushwa, mianya ya wizi na mianya ya nini, mimi sijui leo nikiulizwa fedha zilizorudishwa, zile tani sita tulizoletewa za mbegu zimeenda wapi, siwezi kujua. Kwa ufuatiliaji si rahisi na hata kwa *Auditors* nayo si rahisi; kwa hiyo, tunachoomba basi kile kinachopangwa kirudi na kifanye kazi kinapotegemewa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, labda niseme katika suala hilo la mbegu, ningetoa wito; kwanza, chakula ni heshima ya nchi na ndio usalama wa nchi. Chakula ndio namna pekee, tunasema tunajitegemea, tunajitosheleza na hatuhitaji mtu wa nje; hata akifanya nini akitupa masharti tunaweza kumwambia ondoka, kwa sababu tunajua tuna uwezo wa kujilisha. Kwa hiyo, ningependa katika mipango yetu, chakula kiwe ni katika *pritority*, lakini tunachokipitisha nacho pia kiwe na mtiririko. Labda na Wabunge tupewe taarifa, maana nimekuta kule naanza kushangaa, hivi sasa hiki kitu kinachofanyika ni nini! Wananiambia Mbunge, ninyi mlipitisha Bungeni, lakini tunapitisha kumbe sisi Wabunge hatujui; kinachopitishwa na kinachotekelezwa ni kitu kingine. Kwa hiyo, ningependa tukikubaliana haya mambo makubwa ambayo tungependa kama Taifa twende tukayahamasishe, tushirikiane kupeana taarifa ili Mbunge naye anaposimama, aweze kuongea lugha ile ile ya yule mtaalamu tunayekuwa naye.

Mheshimiwa Spika, kwa haraka sana, nizungumzie suala la pili lilipo ukurasa wa saba. Tunazungumzia mafanikio katika sekta mbalimbali na hasa Sekta ya MKUKUTA. Mimi nadhani hatuna tatizo na kuna mambo mengi mazuri sana tumeyafanya. Tunapofanya mambo mazuri ni vizuri pia tuwe tunafanya tathmini ya kisayansi ya mambo hayo. Ukiniambia tu katika *paper* kama hii ndani ya Ukumbi wa Bunge kwamba, mafanikio hayo yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji mzuri wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM, nafikiri hapa tunafanya siasa; haya mambo yanatakiwa kufanyika kwenye jukwaa si mambo ya kusema ndani ya Ukumbi wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivi? Tunajidanganya na maneno mengi sana mazuri ya siasa, lakini yanatufanya tuweke blanketi, tusifanye tathmini ya wapi tumekwama na wapi tumeendelea. Kwa mfano, tunapozungumzia elimu; elimu haiwezi kuwa ni wingi wa madarasa tu. Tunachozungumzia hapa ni wingi wa madarasa na idadi ya watoto tuliowaingiza, hatujajaribu kuongea ni kwa kiwango gani elimu hii imefanikiwa.

Kwa mfano, jana nimetoka Karatu, leo usiku ndio nimefika hapa, lakini kulikuwa na kitu kimoja; kuna tathmini inafanyika nchi nzima kupitia TAMISEMI. Nadhani walikubaliana na Wahisani, kuna kitu kinachoitwa *PETS.* Unakwenda kwenye shule, walimu labda ni wawili tu, wengine wana kitu kinaitwa leseni. Mimi nakifahamu hiki kitu cha leseni, lakini najiuliza; hivi kumpa leseni mtu aliyemaliza *Form Six* labda, tena kafeli, unataka afundishe; anatoa nini? Hatujafanya tathmini ya vitu hivi… *(Makofi)*

(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria muda

wa mzungumzaji kwisha)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, kengele ya pili hiyo.

MHE. DKT. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika ni ya pili, nakushukuru.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, zimebaki dakika kama mbili, tatu, hazitoshi kuniwezesha kumwita mchangiaji anayefuata. Kwa ajili ya maandalizi, nitawatamka Waheshimiwa Wabunge sita, ambao watachangia jioni; atatangulia Mheshimiwa Omar Kwaangw', atafuatiwa na Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Ahmed Ali Salum na baada ya hapo Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, halafu na wengine ambao wapo katika orodha ya waliokwishaleta majina.

Kwa hiyo, baada ya kuwatamka hao …

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

Kufuatana na Kanuni ya 63(3) na (4); Mbunge atatakiwa kuthibitisha maneno aliyoongea hapa Bungeni. Ninasema hivi kutokana na msemaji aliyepita, kutamka hapa kwamba, anapewa leseni mtu aliyefeli. Nataka athibitishe ukweli huu au afute usemi wake. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Slaa, inaelekea mtu anayefeli hapewi leseni. Sasa wewe umesema hivyo au nikupe muda ili ulete ushahidi?

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, nafikiri ni vizuri aliyetoa hoja, ahakikishe kwamba nilisema, aliyepewa amefeli au anaelekea au anayedhaniwa; ni tofauti kusema kwamba, unaiona hivyo. Mimi nimeuliza jana kwenye Semina yangu na nimepewa taarifa hiyo. Kwa hiyo, hizi ni hisia ambazo wananchi wanazo; wananchi hawajui anayepewa wanaona ni kijana wao wa kijijini. Sasa tunapojadili ndani ya Bunge, tunajadili hisia na *perceptions* na mimi nawakilisha kauli ya wananchi. Kwa hiyo, kama kuna ambao hawakupewa, basi ni vyema tukaambiwa kwamba, waliopewa leseni ni hawa na sifa zao ni hizi na hizi; ndio Kanuni zetu pia zinavyosema.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Slaa, umekwepa kujibu. Mimi mwenyewe nimekusikia, umetamka bayana kwamba, huko Karatu yupo kijana aliyefeli na amepewa leseni ya kufundisha. Kwa hiyo, nakupa muda hadi kesho uweze kuleta uthibitisho huo; vinginevyo, utakuwa umeathiri Kanuni husika na unajua matokeo yake. *(Kicheko/Makofi)*

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nitaangalia *Hansard* halafu nitaleta.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 07.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Nashangaa, hakuna mtu yeyote kutoka Serikalini! Hii ni *scandal;* inakuwaje? Tupige kengele?

Haya, hiyo ni *scandal* ya kwanza. Kwa hiyo, naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 11.03 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,
Tarehe 10 Februari, 2009 Saa Tatu Asubuhi)